



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**



ISO 9001:2015 Certified


# **RIPOTI KUU YA MWAKA YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**



**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU  
WA HESABU ZA SERIKALI  
MACHI 2024**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma, Simu: 255(026)2161200, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz)

**Kumb.Na.CGA.319/421/01B**

**28 Machi 2024**

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
Ikulu,  
S.L.P 1102,  
1 Barabara ya Julius Nyerere,  
11400 Chamwino,  
**40400 DODOMA.**

**RE: KUWASILISHA TAARIFA KUU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA  
HESABU ZA SERIKALI YA MWAKA 2022/23 KUHUSU MIRADI YA  
MAENDELEO**

Ninayo furaha kuwasilisha taarifa yangu ya Jumla ya Mwaka kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, sura ya 418.

Taarifa hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi na kupendekeza hatua za kuboresha ambazo zinalenga kukuza uwajibikaji katika ukusanyaji na matumizi ya rasilimali za umma.


Nawasilisha,

**Charles E. Kichere**  
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**  
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# KUHUSU OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

## Mamlaka

Mamlaka na wajibu wa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418.



### Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo

Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo.

### Kufanya kazi kwa ushirikiano

Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje.

### Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo

Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi stahiki.



### Kufanya kazi kwa utaalum

Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora.

### Kufanya kazi kwa uadilifu

Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadili na sheria katika utoaji wa huduma za ukaguzi.

### Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi

Tunahimiza, kuvumbua, na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwa ajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

ORODHA YA MAJEDWALI .....	iv
ORODHA YA VIELELEZO .....	vi
ORODHA YA VIAMBATISHO .....	vii
ORODHA YA VIFUPISHO .....	viii
SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI .....	ix
MUHTASARI .....	x
SURA YA KWANZA .....	1
UTANGULIZI .....	1
SURA YA PILI .....	2
HATI ZA UKAGUZI .....	2
SURA YA TATU .....	6
UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA KAGUZI ZILIZOPITA .....	6
SURA YA NNE .....	8
UTENDAJI WA KIFEDHA NA USIMAMIZI WA MATUMIZI NA BAJETI .....	8
SURA YA TANO .....	18
USIMAMIZI NA UNUNUZI .....	18
SURA YA SITA .....	23
USIMAMIZI WA MIKATABA NA HALI HALISI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI .....	23
SURA YA SABA .....	36
UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA VIVUKO VIPYA VYA NYAMISATI - MAFIA, MV KILINDONI NA UKARABATI WA VIVUKO VYA MV KAZI NA MV NYERERERE .....	36
SURA YA NANE .....	44
UKAGUZI WA KIUFUNDI KATIKA UJENZI WA UWANJA WA NDEGE WA KIMATAIFA WA MSALATO .....	44
SURA YA TISA .....	52
UKAGUZI WA KIUFUNDI JUU YA UJENZI WA VIHENGE VYA CHUMA VYA KUHFADHI MAZAO CHINI YA WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA .....	52
SURA YA KUMI .....	61
UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA VYUO VYA MAFUNZO (VETA) KATIKA MIKOA NA WILAYA CHINI YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA .....	61
SURA YA KUMI NA MOJA .....	64
UKAGUZI WA KIUFUNDI WA NJIA YA KUSAFIRISHA UMEME KUTOKA BWAWA LA KUFUA UMEME LA JULIUS NYERERE HADI CHALINZE NA UJENZI WA KITUO CHA KUPOOZEA UMEME CHA CHALINZE .....	64
SURA YA KUMI NA MBILI .....	69
UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA MIUNDOBINU YA UMWAGILIAJI .....	69
SURA YA KUMI NA TATU .....	78
UKAGUZI WA KIUFUNDI JUU YA USIMAMIZI WA UBORA WA MAJI KWA MATUMIZI YA NYUMBANI .....	78
SURA YA KUMI NA NNE .....	86
UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UDHIBITI WA GHARAMA KATIKA UJENZI WA MIRADI YA BARABARA .....	86
SURA YA KUMI NA TANO .....	94
UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UDHIBITI WA GHARAMA KATIKA UJENZI WA MIRADI YA BARABARA .....	94

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Idadi ya miradi iliyokaguliwa kwa sekta 2022/23 .....	2
Jedwali 2: Ukaguzi wa kiufundi na uzingatiaji sheria 2022/23 .....	2
Jedwali 3: Muhtasari wa hati za ukaguzi mwaka 2022/23 kwa sekta .....	3
Jedwali 4: Mwenendo wa hati za ukaguzi .....	4
Jedwali 5: Hitimisho la uzingatiaji wa sheria ya Ununuzi .....	5
Jedwali 6: Maoni juu ya kuzingatia sheria ya bajeti .....	5
Jedwali 7: Utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita .....	7
Jedwali 8: Uchambuzi wa utendaji wa kifedha kwa kila sekta .....	9
Jedwali 9: Fedha zilizokopwa pasipo kurejeshwa .....	9
Jedwali 10: Watekelezaji wa miradi ambao hawakuwasilisha kodi ya zuio .....	10
Jedwali 11: Malipo yaliyofanywa bila vipimo vya kazi iliyofanyika .....	13
Jedwali 12: Fidia ambayo haijalipwa kwa Watu walioathirika na Mradi .....	14
Jedwali 13: Miradi iliyoidhinishwa haikufadhiliwa .....	16
Jedwali 14: Ucheleweshaji wa utoaji wa fedha za bajeti iliyoidhinishwa .....	16
Jedwali 15: Manunuzi ambayo yalipangwa lakini hayakutekelezwa .....	20
Jedwali 16: Ununuzi uliofanywa bila hati ya kuagiza bidhaa .....	22
Jedwali 17: Kutotozwa tozo za ucheleweshaji .....	24
Jedwali 18: Mikataba iliyosainiwa bila kupitiwa na wanasheria .....	25
Jedwali 19: Mikataba iliyosainiwa kabla ya kuwasilisha dhamana ya utendaji .....	28
Jedwali 20: Mradi lliyopangwa ambayo haijatekelezwa .....	35
Jedwali 21: Taarifa za mikataba kwa miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko .....	36
Jedwali 22: Kasoro katika usanifu wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko .....	38
Jedwali 23: Athari zilizosababishwa na kukosekana kwa vigezo vya majadiliano .....	40
Jedwali 24: Maombi ya kuongeza muda wa ukarabati wa MV Nyerere .....	42
Jedwali 25: Maelezo ya kufungiwa kwa M/s Beza Engineering Consulting PLC .....	47
Jedwali 26: Wafanyakazi muhimu wasiosajiliwa .....	50
Jedwali 27: Kiasi kilicholipwa kwa kazi ambazo hazijatekelezwa .....	55
Jedwali 28: Orodha ya maeneo na thamani ya vifaa vilivyolipwa bila kusimikwa .....	56
Jedwali 29: Miradi ambayo haijakamilika .....	59
Jedwali 30: Ongezeko la gharama kwa madirisha ya aluminiamu .....	63
Jedwali 31: Taarifa za mikataba ya ujenzi wa miradi ya umwagiliaji hadi tarehe 30 septemba 2023 .....	69
Jedwali 32: Matokeo ya vipimo vya zege kwa mradi wa Magulukenda -Sukuma na Mkombozi Skimu za umwagiliaji .....	73

Jedwali 33: Matokeo ya ushindiliwaji wa udongo katika skimu ya umwagiliaji ya mkombozi.....	74
Jedwali 34: Matokeo ya majaribio ya kushindilia udongo katika skimu ya umwagiliaji ya Magulukenda - Sukuma .....	74
Jedwali 35: Asilimia ya maendeleo ya kazi za miradi na hali ya kifedha dhidi ya muda uliopita .....	75
Jedwali 36: Ongezeko la gharama kutokana na mapungufu ya upembuzi yakinifu na usanifu .....	87
Jedwali 37: Gharama iliyozidi kwa sababu ya kuchelewa kukamilika kwa miradi .....	90
Jedwali 38: Ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi uliopelekea riba .....	91
Jedwali 39: Hali ya malipo ya washauri elekezi .....	92
Jedwali 40: Miradi ambayo upembuzi yakinifu haukufanyika kwa ufanisi na kusababisha gharama za ziada.....	95
Jedwali 41: Nyongeza za muda wa utekelezaji wa miradi na gharama zake .....	98
Jedwali 42: Gharama za ziada kwa makandarasi na washauri .....	99
Jedwali 43: Gharama za riba kutokana na malipo yaliyocheleweshwa .....	100

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 1: Uoni duni upande wa mbele wa feri ya MV Nyerere .....	39
Kielelezo 2: Mfuatano wa matukio ya mabadiliko ya eneo la ujenzi Sumbawanga .....	57
Kielelezo 3: Mfuatano wa matukio ya kubadilisha eneo la ujenzi Babati .....	57
Kielelezo 4: Vifaa vya ujenzi vilivyotelekezwa na kuharibika katika maeneo ya mradi	60
Kielelezo 5: Ujazaji duni wa vifusi kwenye misingi ya Minara/nguzo za umeme.....	68
Kielelezo 6: Barabara ya shambani iliyojengwa juu ya udongo dhaifu .....	76
Kielelezo 7: Kuharibika kwa Barabara ya Magulukenda - Sukuma .....	77
Kielelezo 8: Matope yaliyofurika kwenye mtambo wa kusafisha maji wa Magu .....	84
Kielelezo 9: Udogo asilia usio na ubora .....	96
Kielelezo 10: Maji yaliyotuama katika mitaro ya maji pembezoni mwa barabara .....	97

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho I: Msingi wa kuto hati zenye shaka .....	102
Kiambatisho II: Kuchelewa kusainiwa kwa mikataba ya miwili kwa zaidi ya siku 82 ..	102
Kiambatisho III: Utekelezaji wa shughuli za ujenzi wenye thamani ya Sh. bilioni 1.53 zilizofanyika bila kusaini mkataba .....	102
Kiambatisho IV: Kuchelewa kukamilika kwa miradi na kutokudai tozo ya kuchelewesha kazi za mradi.....	103
Kiambatisho V: Riba iliyotozwa kwa kuchelewesha malipo .....	103
Kiambatisho VI: Taarifa za shughuli ambazo hazikutekelezwa .....	104
Kiambatisho VII: Shughuli zilizolipwa bila kutekelezwa .....	105
Kiambatisho VIII: Vifaa vilivyopokelewa na kulipiwa lakini havijasimikwa .....	105

## ORODHA YA VIFUPISHO

ADF	Mfuko wa Maendeleo ya Afrika
AFD	Shirika la Maendeleo la Ufaransa
AfDB	Benki ya Maendeleo Afrika
AUWASA	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha
BADEA	Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Uchumi Afrika
BoQs	Makadirio ya Gharama za Ujenzi
CDC	Kituo cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa cha Marekani
COVID 19	Ugonjwa wa Virus vya Korona
DANIDA	Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Denmaki
DAWASA	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam
DFATD	Shirika la Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo
DFID	Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza
DLI	Viashiria vya Ugawaji wa Fedha
EASTRIP	Mradi wa kuleta Mabadiliko katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki
EIB	Benki ya Uwekezaji ya Ulaya
EU	Umoja wa Ulaya
EU-AITF	Mfuko wa Dhamana wa Miundombinu wa Umoja wa Ulaya Afrika
GAFFSP	Programu ya Kimataifa wa Kilimo na Usalama wa Chakula
GCC	Masharti ya Jumla ya Mkatoba
HEET	Mradi wa Kuchochea Mageuzi ya Kiuchumi kupitia Elimu ya Juu
IDA	Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza
IPC	Cheti cha Malipo ya Kazi za Ujenzi
JICA	Shirika la Maendeleo la Japani
KfW	Shirika la Misaada la Ujerumani
KOICA	Kanada, Ireland, Shirika la Uhusiano wa Kimataifa la Korea Kusini
NACP	Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi
NAVAIDS	Vifaa vya Kuongoza Njia
NM-AIST	Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela
PAP	Waathirika wa Miradi
PERFAR	Mpango wa Dharura wa Rais wa Kukabiliana na UKIMWI
OR-TAMISEMI	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
PPE	Vifaa vya Kinga
PSSN	Mpango wa Kususuru Kaya Maskini
RPM	Mzunguko kwa Dakika
TANROADS	Wakala wa Barabara nchini Tanzania
TARURA	Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini
TASAF III	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii
TPDC	Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania
UNDP	Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa
USAID	Shirika la Misaada la Watu wa Marekani
UWSSA'S	Mamlaka ya Maji Mijini na Usafi wa Mazingira
UVIKO	Ugonjwa wa Virusi vya Korona



## SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Juni 2023 ambayo inajumuisha miradi yote ya maendeleo. Napenda kutambua mipango ya Serikali inayoongozwa na Mh.Dkt.Samia Suluhu Hassan, Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma. Pia nashukuru kwa ushirikiano wa menejimenti za taasisi katika kutoa taarifa na ufafanuzi muhimu kwa ajili ya kuandaa ripoti ya ukaguzi.

Matokeo ya ukaguzi yanadhihirisha nyanja mbalimbali za usimamizi wa fedha kati ya miradi ya maendeleo. Ingawa baadhi wameonesha usimamizi mzuri wa fedha, wengine bado wanakabiliwa na changamoto katika kudumisha usimamizi wa kifedha na utendaji. Ni muhimu kwa Serikali kuingilia kati na kuhakikisha taasisi hizi zinafanya kazi kwa ufanisi na tija, kuchangia uchumi na kutoa huduma za hali ya juu kwa wananchi.

Ripoti hii inajumuisha sura 15, kila moja ikiangazia vipengele tofauti, ikiwa ni pamoja na sheria za ununuzi, usimamizi wa mapato na fedha, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa bajeti na kufuata sheria za kodi. Ripoti hii pia inabainisha maeneo ambayo taasisi hizi zinahitaji kuboresha utendakazi wao na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Katika ripoti hii, nimetoa mapendekezo ya jinsi ya kuimarisha utendaji kazi wa taasisi zilivyoripotiwa, kuongeza uwazi na uwajibikaji na kuimarisha utawala bora. Ninaamini mapendekezo haya yatakuwa na manufaa kwa Serikali na wadau wengine katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora.

Mwisho, natoa shukrani zangu za dhati kwa wakaguzi wote kwa juhudi zao za dhati katika kufanya ukaguzi na kuandaa ripoti hii. Kujituma kwao na bidii yao imekuwa muhimu katika utayarishaji wa ripoti hii, na ninashukuru kwa mchango wao.

Charles E. Kichere  
Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# MUHTASARI

Ripoti hii ina sura 15 zinazojumuisha ukaguzi wa fedha na ukaguzi wa kiufundi uliofanywa katika sekta mbalimbali kwa mwaka wa fedha wa 2022/23. Maeneo yafuatayo yamejadiliwa kwa kina katika ripoti hii:

## Hati za Ukaguzi

Kati ya hesabu 299 zilizokaguliwa, 296 (99%) zilipata hati inayoridhisha sawa na mwaka uliopita. Hata hivyo, taasisi moja (1%) iliyoipo katika sekta ya kijamii imepata hati isiyoridhisha kutokana na taarifa yao ya fedha kuwa na matumizi pungufu.

Pia, uchambuzi wa uzingatiaji wa sheria za ununuzi na usimamizi wa bajeti kwa taasisi 299 ulihitimisha kuwa taasisi 130 zilifuata sheria za ununuzi na ripoti 69 zilikuwa na upungufu; vivyo hivyo, taasisi 251 zilifuata sheria ya bajeti, wakati taasisi 48 zilifuata sheria zikiwa na mapungufu machache.

## Utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita

Uchambuzi wangu wa taarifa 299 za usimamizi wa miradi ya maendeleo kuna jumla ya mapendekezo 2,982. Kati ya hayo, 40% yalitekelezwa, 26% yalikuwa yanaendelea kutekelezwa, 29% hayakutekelezwa, 9% yamerudiwa, na 6% yalipitwa na wakati.

## Utendaji wa kifedha na usimamizi wa matumizi

Uchambuzi wa taarifa 299 za fedha za mwaka 2022/23 ulionyesha kuwa jumla ya fedha za miradi wa Sh. trilioni 6.50 zilipokelewa. Kati ya hizo, Sh. trilioni 4.19 zilitumika, na kuacha bakaa ya Sh. trilioni 2.31 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023.

Katika usimamizi wa matumizi, nilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST) ilikopa Sh. 4,549,015,746 kutoka katika miradi ya SEQUIP na LANES II, ambazo bado hazijarejeshwa. Pia, nilibaini kuwa TANROADS, MOEST na TASAF hawakutoza kodi ya zuio yenye thamani ya Sh. 1,118,230,367, wakati taasisi mbili (TASAF na TANROADS) zilitoza lakini hazikuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania Sh. 5,216,572,492. Jumla kodi za zuio ambazo hazijatozwa na hazijawasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ni Sh. 6,334,802,859.

Aidha, nilibaini kuwa miradi sita—mitano iliyotekelezwa na TANESCO na mmoja wa AUWASA—haikulipa fidia ya Sh. bilioni 13.69 kwa watu 567 walioathirika. Miradi mitano inadaiwa Sh. bilioni 12.67 na Mradi wa Maendeleo ya nishati ya jua ya Tanzania ulikuwa na nyongeza ya makadirio ya deni la Sh. bilioni 1.02 kama fidia. Licha ya kukaribia kukamilisha miradi (97% hadi 100%) bila malipo ya fidia kwa waathirika.

### **Usimamizi wa Ununuzi**

Nilibaini kuwa MWAUWASA ilitumia viwango vya ushindani vya kitaifa badala ya zabuni ya ushindani wa kimataifa katika upatikanaji wa huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 3.55 kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la maji katika Mji wa Kisesa, Mkoani Mwanza, unaotekelezwa chini ya Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (LVWATSAN). Hii ilipunguza ushiriki wa wazabuni wengine na kuzuia ununuzi kwa bei shindani.

Pia, nilibaini kuwa Mradi wa SEQUIP chini ya OR-TAMISEMI ulilipa Sh. 1,528,253,924 kwa mafundi ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya shule za sekondari katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, Halmashauri ya Wilaya ya Mtama, na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa bila ya kusaini mikataba.

### **Mkataba na utendaji wa miradi**

Niligundua kuwa Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini wa Arusha ulikamilisha visima virefu 15 vilivyogharimu Sh. bilioni 9.16, ambavyo vilikamilika Mei 2023. Pamoja na kukamilika huko, hakuna miundombinu ya usambazaji maji inayounganisha visima hivyo kwa watumiaji wa mwisho. Upungufu huu umeufanya mradi huo kutokufanya kazi.

OR-TAMISEMI iliagiza ujenzi wa shule za awali za mfano awamu ya I na II, ambapo Sh. 12,252,675,000 zimetengwa kwa shule 197 katika halmashauri 160 chini ya mpango wa LANES. Katika ziara yangu mwezi Agosti 2023, niligundua kuwa majengo yaliyokamilika yenye thamani ya Sh. 1,395,600,000 katika halmashauri 25 hayakutumika kutokana na kutokuwapo kwa samani muhimu na huduma ya maji kwa ajili ya vyoo vya shimo vilivyojengwa.

Aidha, muundombinu wa Awamu ya 2 ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) unaotekelezwa na TANROADS ulikuwa na gharama ya ziada ya Sh. bilioni 28.05 kutokana na mabadiliko ya muundo, upembuzi yakinifu usiotosheleza, na mapitio ya usanifu kabla ya kuanza kwa mradi.

Aidha, nilibaini tozo za riba kiasi cha Sh. bilioni 3.08 kutokana na kucheleweshwa kwa malipo ya wakandarasi na kutotumika kwa mkopo.

Uchambuzi wangu ulionesha kuwa TANESCO ilitozwa Sh 2,129,506,978 (69%) kwa ucheleweshaji wa kutumia mkopo wa Mradi wa Tanzania Zambia (TAZA), na TANROADS ilitozwa Sh. 874,996,553 (28.4%) kwa kuchelewesha malipo kwa wakandarasi na kwa kushindwa kutumia fursa za mkopo.

Wizara ya Maji na Wizara ya Maliasili na Utalii zilikabiliwa na tozo za kuchelewesha malipo Sh. 25,004,367 (0.8%) na Sh. 47,851,268 (1.6%) mtawalia. Tozo hizo zinahusiana na kuchelewa kulipa madai ya wakandarasi katika utekelezaji wa Mradi wa Pili wa Sekta ya Maji na Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali za Asili kwa ajili ya Utalii na Ukuaji mtawalia.

### **Ukaguzi wa Kiufundi**

Ukaguzi wa kiufundi ulifanywa katika maeneo yafuatayo:

- **Udhibiti wa gharama**

Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) uliingia gharama kubwa ya Sh. bilioni 130.51 katika miradi sita ya barabara kutokana na mapungufu katika upembuzi yakinifu, dosari katika usanifu, usimamizi wa mikataba na kucheleweshwa kwa malipo. Taarifa za upembuzi yakinifu zisizotosheleza ndiyo sababu kuu iliyopelekea Sh. bilioni 44.97 (34.5%) la ongezeko gharama, kwani hali za maeneo muhimu kama vile topografia, udongo na haidrolojia hazikupimwa kwa usahihi, na hivyo kuhitaji marekebisho makubwa wakati wa utekelezaji wa mradi.

Aidha, ucheleweshaji wa malipo ulisababisha limbikizo la riba la Sh. bilioni 42.8, wakati ucheleweshaji wa kukamilika kwa miradi ulihitaji kuwafidia wakandarasi Sh. bilioni 29.87 na washauri elekezi nyongeza ya Sh. bilioni 18.88. Pia, kiasi cha Sh. bilioni 3.99 kililipwa kwa Kitengo cha Ushauri wa Uhandisi (TECU) cha TANROADS bila mkataba rasmi. Ongezeko hili linaonesha hitaji la dharura la TANROADS kuboresha itifaki zake za upembuzi yakinifu, michakato ya mapitio ya usanifu, usimamizi wa mikataba, na mifumo ya malipo ili kupunguza kasoro za masuala haya ya kifedha katika siku zijazo.

- **Ujenzi wa barabara**

Uchambuzi wangu wa udhibiti wa gharama kwa barabara zinazotekelezwa na TANROADS na TARURA ulibaini kuwapo kwa ziada ya gharama ya Sh. bilioni 66.06. Gharama hiyo ya ziada ilitokana na mabadiliko makubwa ya miundo wakati wa utekelezaji wa mradi. Mabadiliko hayo yalisababishwa na upungufu katika upembuzi yakinifu ambao haukuweza kuonesha hali halisi za maeneo kama vile topografia, udongo, na haidrolojia.

Pia, nilibaini ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi katika miradi minne ya barabara na TANROADS na mradi mmoja wa TARURA, hivyo kusababisha riba jumla ya Sh. bilioni 44.25, ambapo Sh. bilioni 42.57 kwa miradi ya TANROADS na Sh. bilioni 1.68 kwa mradi wa TARURA.

- **Ujenzi na ukarabati wa vivuko**

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa injini za kivuko cha MV Kilindoni zilikuwa zinapata joto kupita kiasi zinapokuwa katika mwendo wa mizunguko 1800 kwa dakika (rpm). Licha ya matakwa ya kimkataba kwa TEMESA kukagua bidhaa kabla ya usafirishaji na kanuni za sekta zinazohitaji uthibitisho wa vipimo kwenye injini mpya, wataalamu wa TEMESA hawakushiriki katika jaribio la kupima injini ya kivuko iliyofanyika nchini Korea. Kwa hivyo, utendaji wa mfumo wa injini ya baharini haukuthibitishwa, kinyume na matakwa ya kabla ya usafirishaji.

Vilevile, majaribio yaliyofanyika katika karakana ya kutengeneza kivuko cha Kigamboni yalikosa kiwango kinachokubalika cha ubora wa majaribio. Ingawa mradi uliripotiwa kuwa umekamilika kwa asilimia 100, hakuna cheti cha kukamilisha kilichotolewa, na Sh. bilioni 5.07 kati ya jumla ya mkataba wa Sh. bilioni 5.31 za mkataba zililipwa. Aidha, TEMESA ilishindwa kumuagiza mkandarasi kurekebisha tatizo la injini kuongezeka joto licha ya kupata taarifa ya tatizo hilo kutoka kwa wahandisi wa TEMESA wakati wa majaribio ya baharini mwezi Aprili 2023 ambapo ilithibitishwa tatizo la kuongezeka kwa joto kupita kiasi inapokuwa katika mwendo wa mizunguko 1800 kwa dakika (rpm).

Aidha, nilibaini kwamba ujenzi wa MV Kilindoni na kivuko kipya kati ya Nyamisati na Mafia ulihitaji idhini ya TASAC, huku vipimo muhimu vya udhibiti wa ubora havikuzingatiwa. Aidha, mabadiliko katika muundo wa ukarabati wa kivuko cha MV Nyerere hayakuwasilishwa kwa idhini ya TASAC.

- **Ujenzi wa vihenge vya kuhifadhi nafaka na ujenzi wa majengo ya VETA**

Nilibaini kuwa NFRA ililipa Sh. 315,812,546 kwa mkandarasi kwa kazi za ujenzi ambazo hazikutekelezwa. Kazi hizo ni: ujenzi wa kuta, kazi ya zege, ufungaji wa nondo, na uchimbaji na ujenzi wa mfumo wa maji taka katika miradi ya Songea na Shinyanga.

Vilevile, NFRA ililipa dola za Marekani 4,853,039.42 (sawa na Sh. 10,856,249,183) kwa vifaa vilivyowasilishwa lakini bado havijafungwa kwa kuwa mkandarasi alitelekeza eneo hilo tangu Desemba 2020. Malipo yaliyofanyika hayakutoa ufafanuzi wa gharama kuonesha matumizi ya usambazaji, ufungaji, majaribio, na kukabidhi. Msimamizi wa mradi alithibitisha malipo bila ufafanuzi wa wazi.

Aidha, nilibaini ongezeko la gharama la Sh. bilioni 1.26 zilizolipwa na NFRA kwa wakandarasi kutokana na mabadiliko ya maeneo ya ujenzi Sumbawanga na Babati. Uamuzi wa kuhamisha eneo la Sumbawanga ulichangiwa na kuhamisha eneo la viwanda hadi Kanondo, wakati kwa upande wa Babati, kulikuwa na mwingiliano na laini ya usafirishaji wa umeme wa juu iliyopangwa na TANESCO.

Nilibaini kuwa michoro ya muundo wa vituo 25 ilionesha kuwa vifaa vya kuzima moto kama vile kengele za moto, vitambua-moto, na vitambua-moshi vilitakiwa kuwekwa jikoni na kwenye karakana. Hata hivyo, ratiba ya vifaa ilionesha kuwa, ni vifaa vya kuzima moto tu vilivyojumuishwa, lakini havikuwekwa katika vituo husika. Hii inamaanisha kuwa, hakukuwa na vifaa vya kuzima moto vilivyowekwa katika vituo 25 vilivyojengwa. Hii inamaanisha kwamba, Sh. bilioni 2.6 zilizowekezwa katika ujenzi wa kituo kimoja zitakuwa hatarini endapo janga la moto litatokea.

- **Miradi ya umwagiliaji na ubora wa maji kwa matumizi ya nyumbani**

Nilibaini kuwa utafiti uliofanywa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji huko Eyasi, Lyamalagwa, Mkombozi, na Magulukenda-Sukuma ulikuwa na upungufu ufuatao: kutokuwapo kwa uchunguzi muhimu wa geoteknolojia kwa ajili ya kazi za msingi na mifereji; utafiti wa hali ya maji ulitegemea sana mifano ya miaka 50 bila uthibitisho wa data halisi ya utoaji maji; na utafiti wa awali juu ya uchunguzi wa udongo ulikuwa na upungufu wa taarifa na mapendekezo.

Pia, nilibaini upungufu katika ujenzi na usimamizi wa barabara za shamba ndani ya miradi ya umwagiliaji ya Mkombozi na Magulukenda kwa kuwa barabara zilijengwa kwenye udongo usiofaa, wakati barabara za mradi wa Magulukenda-Sukuma zilikosa mifereji ya maji. Upungufu huu umesababisha Barabara kuharibika mapema, hivyo kutoweza kupitika nyakati za mvua.

Chini ya usimamizi wa ubora wa maji majumbani, nilibaini kulikuwa na Mpango wa Ufuatiliaji wa Ubona wa Maji usioridhisha katika mamlaka za maji. Hii ni kwa sababu programu zilizopo hazikufuata kikamilifu miongozo ya EWURA, kwani hakukuwa na vifaa vya ufuatiliaji wa utendaji. Licha ya kufanya ufuatiliaji wa kiutendaji, bajeti ya kipengele hiki haikujumuishwa katika Mpango wao wa Ufuatiliaji wa Ubona wa Maji (WQMP). Aidha, nilibaini kati ya mamlaka nane za maji zilizokaguliwa, 88% zilishindwa kufikia viwango vya mabaki ya klorini.

Kutokana na hatari kubwa za afya ya umma zinazohusishwa na kutofuata viwango vya mabaki ya klorini, mwaka 2022/23 na 2021/22 DAWASA na MWAUWASA zilibainika na changamoto hizi baada ya idadi kubwa ya watu kukabiliwa na viashiria za hatari hizo.



### 1.1 Maelezo ya awali

Ukaguzi huu ulitathmini usimamizi wa fedha, mfumo wa udhibiti na uzingatiaji wa sheria katika miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2023. Ukaguzi huu ni sehemu ya mamlaka na majukumu ya kisheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoelezwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na katika Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418. Lengo lilikuwa ni kuhakikisha taasisi zinazotekelza miradi zinafanya kazi kwa ufanisi, kuchangia katika uchumi na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Ripoti hii imeundwa katika sura 15 kila moja ikilenga kipengele tofauti, ikijumuisha utekelezaji wa sheria za ununuzi, usimamizi wa mapato na fedha, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa bajeti na kutekeleza sheria za kodi. Ripoti hiyo pia inatoa mapendekezo ya kuboresha katika utendaji kazi wa taasisi hizi, kuimarisha uwazi na uwajibikaji, na kukuza utawala bora.

### 1.2 Madhumuni ya Ukaguzi

Ukaguzi ulilenga kutoa maoni huru iwapo hesabu zilitayarishwa kwa mujibu wa mfumo unaokubalika wa utoaji taarifa za fedha, kwa kuzingatia mambo yote muhimu. Aidha, ulilenga kutathmini uzingatiaji wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma katika miradi ya maendeleo na Sheria ya Bajeti, Kanuni na miongozo. Ukaguzi pia ulilenga kutathmini tija na ufanisi wa miradi ya maendeleo katika kusimamia fedha za umma na kutoa huduma kwa wananchi.

### 1.3 Mawanda ya Ukaguzi

Katika mwaka wa fedha 2022/23, aina tatu za ukaguzi zilifanywa kwenye miradi ya maendeleo: ukaguzi wa hesabu, uzingatiaji wa sheria na ukaguzi wa kiufundi. Ripoti 299 za ukaguzi wa fedha zilitolewa, zikilenga mifumo ya usimamizi wa fedha, udhibiti na uandaaji wa hesabu. Aidha, kaguzi 12 za kiufundi zilifanywa kwenye miradi ya ujenzi katika sekta mbalimbali, kutathmini mipango, ununuzi na usimamizi wa mikataba, miongoni mwa vipengele vingine. Ukaguzi wa

uzingatiaji wa sheria ulitathmini uzingatiaji wa sheria za ununuzi wa umma na miongozo ya bajeti. Kwa ujumla, miradi 92 katika taasisi 248 ilikaguliwa, na kutoa ripoti 310 za ukaguzi, na matokeo ya utafiti yakihusisha sekta mbalimbali kama inavyooneshwa kwenye majedwali 1 na 2.

**Jedwali 1: Idadi ya miradi iliyokaguliwa kwa sekta 2022/23**

Na.	Sekta	Taarifa za kiufundi	Taarifa za ukaguzi wa fedha	Miradi iliyokaguliwa	Watekeleza miradi	Jumla ya taarifa za ukaguzi
1	Kilimo	2	6	6	5	9
2	Elimu	1	29	8	17	30
3	Nishati na Madini	1	16	16	4	17
4	Afya	0	198	14	189	198
5	Mawasiliano na Uchukuzi	6	13	13	5	19
6	Maji	1	9	9	8	10
7	Jamii	0	10	10	8	9
8	Miradi Mingineyo	0	18	16	12	18
<b>Jumla</b>		<b>11</b>	<b>299</b>	<b>92</b>	<b>248</b>	<b>310</b>

Chanzo: Taarifa za kaguzi wa fedha, kiufundi na uzingatiaji kama sheria ya mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2023

**Jedwali 2: Ukaguzi wa kiufundi na uzingatiaji sheria 2022/23**

Na.	Sekta	Jina la taarifa ya ukaguzi wa kiufundi	Marejeo ya Sura
1	Uchukuzi	Ujenzi wa vivuko vipya vya nyamisati - mafia, MV kilindoni na ukarabati wa vivuko vya MV kazi na MV Nyerere	7
2	Uchukuzi	Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Msalato	8
3	Kilimo	Ujenzi wa vihenge vya chuma.	9
4	Elimu	Ujenzi wa Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi katika Mikoa na Wilaya	10
5	Nishati na Madini	Ujenzi wa kituo kidogo na njia ya kusafirisha umeme kutoka Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere hadi Chalinze	11
6	Kilimo	Ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji	12
7	Maji	Usimamizi wa ubora wa maji kwa matumizi ya nyumbani	13
8	Uchukuzi	Mradi wa Ujenzi wa barabara	14
9	Uchukuzi	udhibiti wa gharama katika ujenzi wa miradi ya barabara	15

Chanzo: Tarifa za ukaguzi wa kiufundi kwa mwaka unaoishia 30 Juni 2023

#### 1.4 Mbinu za Ukaguzi

Ukaguzi ulifanywa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI) na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISAs).

Mbinu za ukaguzi zilizotumiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilijumuisha mjumuiko wa taratibu, kama vile kukagua kumbukumbu na nyaraka mbalimbali, kufanya usaili na wahusika na kutembelea miradi mahali inapotekelezwa. Ukaguzi pia ulihusisha kupima mifumo ya udhibiti wa ndani ya miradi ya maendeleo na kutathmini utekelezaji wa sheria, kanuni na sera husika.



### 2.1 Utangulizi

Sura hii ni muhtasari wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa na Taasisi za Umma katika mwaka wa fedha 2022/23, pamoja na mwenendo wa maoni niliyotoa katika hesabu kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo. Maoni yaliyotolewa yanatokana na tathmini ya vielelezo vilivyopatikana katika kipindi chote cha ukaguzi, kutathmini endapo hesabu zinazingatia mifumo husika ya utayarishaji wa hesabu kama vile Viwango vya Kimataifa vya hesabu (IFRSs), Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSASs), na Kiwango cha Taarifa za Fedha Tanzania Na. 1 (TFRS1) katika mambo yote muhimu. Tathmini hii inazingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) 1200.

### 2.2 Aina za hati za ukaguzi

**Aina za hati za ukaguzi** ni: hati inayoridhisha, hati ya mashaka, hati mbaya na hati ya kushindwa kutoa maoni.

**Hati inayoridhisha** hutolewa wakati mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango na mfumo unaokubalika wa utayarishaji wa hesabu.

**Hati yenye shaka** hutolewa pale hesabu zinapoonekana zimeandaliwa kwa usahihi isipokuwa uwepo wa suala/masuala ambayo yanaathiri usahihi kamili wa hesabu hizo. Hii inaweza kutokea baada ya mkaguzi kupata vielelezo vya kutosha na kuhitimisha kuwa kosa/makosa kwenye hesabu yakiwekwa pamoja yana athari, lakini hayaathiri kwa ujumla usahihi wa hesabu. Pia hati yenye shaka inaweza kutolewa pale Mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kumwezesha kuhitimisha ukaguzi lakini athari zinazotokana na kukosa uthibitisho huo kwa ujumla wake haziathiri maeneo yote ya taarifa za fedha.

**Hati mbaya** hutolewa pale mkaguzi anapokuwa amepata vielelezo vya kutosha kuthibitisha kuwa hesabu zina makosa na makosa hayo kwenye hesabu yakiwekwa pamoja yana athari kubwa na yanahusisha maeneo mengi katika hesabu.

**Kushindwa kutoa hati** hutokea pale mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu hesabu ambazo ni msingi wa kutoa hati, Hivyo mkaguzi kuhitimisha kuwa athari za makosa yanayoweza kuwa kwenye hesabu ambayo hayakubainika yanaweza kuwa makubwa na yenye athari kwa sehemu zote za hesabu hizo. Mkaguzi huwa anashindwa kutoa hati katika mazingira ya nadra sana yanayohusisha mashaka; hivyo, mkaguzi kuhitimisha kuwa athari za makosa yanayoweza kuwa kwenye hesabu ambayo hayakubainika yanaweza kuwa makubwa na yenye athari kwa maeneo yote ya taarifa hiyo. Hati za ukaguzi zilizotolewa katika mwaka wa fedha

Katika mwaka wa fedha 2022/23, nilikamilisha kaguzi 299 za miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Taasisi za umma ambapo nilitoa hati 299. Kati ya hati hizo, 298 zilikuwa hati zinadhoriidhisha an hati moja ilikua hati yenye shaka (Mradi wa Mpango wa Kuondoa Umaskini, Mazingira, Jinsia, na Mabadiliko ya Tabianchi uliotekelezwa na Taasisi ya Mipango ya Maendeleo Vijijini - Kanda ya Ziwa Mwanza). Kielelezo Na 1 kinaonesha kuwa hati yenye shaka ilitokana na uandaji wa taarifa ya fedha yenye matumizi pungufu. Hakukuwa na hati mbaya au hati ya kushindwa kutoa maoni kwa ukaguzi katika mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2023. Hati za ukaguzi zilizotelewa zimefafanuliwa kwenye **Jedwali 3**.

**Jedwali 3: Muhtasari wa hati za ukaguzi mwaka 2022/23 kwa sekta**

Sekta	Hati zilizotolewa				Jumla
	Hati zinazoridhisha	Hati zenye mashaka	Hati mbaya	Hati ya kushindwa kutoa maoni	
Kilimo	7	-	-	-	7
Elimu	29	-	-	-	29
Nishati na madini	16	-	-	-	16
Afya	198	-	-	-	198
Uchukuzi na Mawasiliano	13	-	-	-	13
Maji	9	-	-	-	9
Jamii	8	1	-	-	9
Miradi Mingine	18	-	-	-	18
<b>Jumla</b>	<b>298</b>	<b>1</b>	<b>0</b>	<b>0</b>	<b>299</b>

Chanzo: Taarifa za fedha za mwaka wa fedha 2022/23

### 2.3 Mwenendo wa hati za ukaguzi kwa miaka mitano

**Jedwali 4** linaonesha mwenendo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa watekelezaji wa miradi kwa miaka mitano mfululizo toka 2018/19 mpaka 2022/23. Ongezeko la hati zinazoridhisha kutoka 97% mpaka 99% inatokana na uboreshaji katika maandilizi ya taarifa za fedha zinazoendana mifumo ya uandaji hesabu (IPSAS and IFRS)

**Jedwali 4: Mwenendo wa hati za ukaguzi**

Mwaka wa fedha	Hati zilizotolewa						
	Hati inayoridhisha		Hati yenye mashaka		Hati mbaya		Jumla
	Na.	%	Na.	%	Na.	%	
2022/23	298	99	1	1	0	0	299
2021/22	287	99	3	1	0	0	290
2020/21	293	100	-	-	-	-	293
2019/20	275	95	15	5	-	-	290
2018/19	441	97	13	3	1	0.22	455

**Chanzo:** Taarifa za ukaguzi za mwaka wa fedha 2022/23 na taarifa kuu ya miradi ya maendeleo ya miaka iliyopita

Uchambuzi wa mwenendo wa hati za ukaguzi katika kipindi cha miaka mitano unaonesha kutawaliwa na kiwango kikubwa na hati zinazoridhisha (Hati Safi), huku asilimia kubwa zaidi ikirekodiwa mwaka 2020/21 (100%) ikifuatiwa kwa karibu na 2022/23 (99%), 2021/22 (99%), na 2018/19 (97%).

### 2.4 Hitimisho kuhusu usimamizi wa bajeti na ununuzi

Ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha 2022/23 ulijikita katika maeneo makuu mawili kuhusu utekelezaji wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma na sheria na mwongozo wa bajeti, ambapo nimetoa maoni yafuatayo:

#### 2.4.1 Mahitimisho ya ukaguzi kuhusu uzingatiaji wa sheria za ununuzi

Katika mwaka wa fedha 2022/23, yalitolewa mahitimisho 299 kuhusu utekelezaji wa sheria za ununuzi kwa watekelezaji wa mradi. Kati ya hayo, maoni 230 yanaonesha taasisi zilitekeleza kikamilifu sheria za ununuzi huku maoni 69 yanaonesha kulikuwa na upungufu katika utekelezaji wa sheria za ununuzi. Maelezo ya maoni ya utekelezaji wa sheria za ununuzi yameoneshwa katika **Jedwali 5**.

**Jedwali 5: Hitimisho la uzingatiaji wa sheria ya Ununuzi**

Sekta	Uzingatiwaji kikamilifu wa sheria ya ununuzi	Upungufu katika uzingatiaji wa sheria ya ununuzi	Jumla ya maoni ya sheria za Ununuzi
Kilimo	5	2	7
Elimu	19	10	29
Nishati na madini	15	1	16
Afya	152	46	198
Uchukuzi na Mawasiliano	11	2	13
Maji	6	3	9
Jamii	8	1	9
Miradi Mingine	14	4	18
<b>Jumla</b>	<b>230</b>	<b>69</b>	<b>299</b>

**Chanzo:** Taarifa za fedha za mwaka wa fedha 2022/23

#### 2.4.2 Maoni ya ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria za bajeti

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, nimetoa maoni kwa miradi 299 kuhusu uzingatiaji wa sheria na miongozo ya bajeti kwa watekelezaji wa miradi. Miradi 251 kati ya 299 yalifuata sheria za bajeti na 48 ilikuwa na upungufu katika utekelezaji wa sheria ya bajeti. Maelezo ya maoni yaliyotolewa yanaoneshwa kwenye Jedwali 6.

**Jedwali 6: Maoni juu ya kuzingatia sheria ya bajeti**

Sekta	Uzingatiwaji kikamilifu wa sheria ya bajeti	Upungufu katika uzingatiaji wa sheria ya bajeti	Jumla ya maoni ya sheria ya bajeti
Kilimo	7	0	7
Elimu	24	5	29
Nishati na madini	15	1	16
Afya	161	37	198
Uchukuzi na Mawasiliano	11	2	13
Maji	8	1	9
Jamii	9	0	9
Miradi Mingine	16	2	18
<b>Jumla</b>	<b>251</b>	<b>48</b>	<b>299</b>

**Chanzo:** Taarifa za fedha za mwaka wa fedha 2022/23

# SURA YA TATU

## UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA KAGUZI ZILIZOPITA



### 3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea maendeleo na hatua zilizochukuliwa na maafisa masuuli kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwa taasisi husika. Ninatambua juhudi zinazochukuliwa na maafisa masuuli katika kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi na kutengeneza mipango ya ushughulikiaji wa changamoto zilizoripotiwa.

### 3.2 Utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita

Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ni muhimu kwa kuwa unakuza uwajibikaji, huchochea uboreshaji, hupunguza hatari, huongeza utendajikazi kwa ujumla, huweka imani ya wadau, huhakikisha uzingatiaji wa sheria na maadili, huimarisha usimamizi wa rasilimali, na huimarisha utawala bora ndani ya taasisi.

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi, umebaini kuwa katika ripoti 299 za ukaguzi wa miradi ya maendeleo umebainimapendekezo 2,982 ambayo bado hayajatekelezwa.

Hata hivyo, maafisa wa uhasibu wanaonesha nia ya kuboresha usimamizi wa kifedha na udhibiti kupitia mipango ya hatua zilizoainishwa. Kati ya mapendekezo hayo 2,982 ya ukaguzi ambayo bado hayajatekelezwa kutoka kwa ripoti za miaka iliyopita, 1192 (40%) yalitekelezwa kikamilifu, 772 (26%) yako katika mchakato wa utekelezaji, 575 (19%) hayajatekelezwa, 276 (9%) yaliruudiwa kusisitizwa, na 167 (6%) yalipitwa na wakati. Hali ya jumla ya utekelezaji haikidhi viwango, kama ilivyoelezwa kwa kina katika Jedwali la 7.

huku maafisa masuuli wakionesha dhamira ya kuboresha usimamizi na udhibiti wa fedha kupitia mipango kazi waliyoainisha.

Kati ya Mapendekezo ya ukaguzi 2982 kutoka kwenye ripoti zangu za miaka iliyopita, mapendekezo 1192 (40%) yalitekelezwa kikamilifu, 772 (26%) yalikuwa yanaendelea kutekelezwa, 575 (19%) hayakutekelezwa, 276 (9%) yalijirudia na 167 (6. %) yalipitwa na wakati. Hali ya jumla ya utekelezaji hairidhishi kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali 7**.

**Jedwali 7: Utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita**

Sekta	Mapendek ezo ya Miaka ya Nyuma	Mapend ekezo yaliyote kelezwa	Mapendekezo yanayoendele a kutekelezwa	Mapendek ezo ambayo hayajatek elezwa	Mapendek ezo yaliyojiru dia	Mapend ekezo yaliyopi twa na wakati
Kilimo	33	11	16	2	3	1
Elimu	362	99	171	17	42	33
Nishati na Madini	75	32	27	4	6	6
Afya	2007	818	419	509	177	84
Jamii	114	82	20	6	2	4
Uchukuzi	156	57	39	28	17	15
Maji	129	35	49	5	20	20
Sekta mbalimbali	106	58	31	4	9	4
<b>Jumla</b>	<b>2982</b>	<b>1192</b>	<b>772</b>	<b>575</b>	<b>276</b>	<b>167</b>
<b>Asilimia</b>	<b>100</b>	<b>40%</b>	<b>26%</b>	<b>19%</b>	<b>9%</b>	<b>6%</b>

**Chanzo:** Taarifa za ukaguzi za mwaka 2022/23

Uchambuzi unaonesha hali halisi ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika kaguzi zilizopita. Sekta ya Afya inaonekana kuwa na idadi kubwa ya mapendekezo ambayo hayakutekelezwa (2007), ikifuatiwa na Elimu (362) na Uchukuzi (156). Hii inaonesha maendeleo na changamoto mbalimbali katika kushughulikia mapendekezo ambayo yalikuwa hayajatekelezwa katika sekta zote.

Kutokutekelezwa kwa mapendekezo ya ukaguzi kunaweza kuwa na athari mbaya, ikiwemo: kuhatarisha uadilifu kwenye eneo la usimamizi wa fedha; kuongezeka kwa vihatarishi katika utendaji; kudhoofisha ufanisi wa taasisi; kupoteza imani ya wadau wa miradi ya maendeleo; migogoro ya kisheria na udhibiti; na kudumisha udhaifu wa mfumo ambao unaweza kusababisha upungufu wa ufanisi na hasara za kifedha.

Ili kushughulikia mapendekezo yaliyosalia, ninapendekeza maafisa masuuli waweke vipaumbele kwenye rasilimali, kuimarisha juhudi za utekelezaji na kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani katika sekta zote.

# SURA YA NNE

## UTENDAJI WA KIFEDHA NA USIMAMIZI WA MATUMIZI NA BAJETI



### 4.1 Utanguluzi

Sura hii inatoa muhtasari wa kaguzi 299 za hesabu zinazohusu ufadhili wa miradi na matokeo muhimu ya ukaguzi kuhusiana na usimamizi wa fedha na bajeti. Inatoa taarifa muhimu kwa serikali ili kuboresha utendaji wa kifedha, kukuza uwajibikaji, na kuhakikisha uwazi katika kutoa taarifa za kifedha.

### 4.2 Ufadhili wa miradi

Ufadhili wa miradi ya maendeleo unatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wadau wa Maendeleo kama vile: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Mfuko wa Maendeleo ya Afrika (ADF), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Uchumi Afrika (BADEA), Kituo cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa cha Marekani (CDC), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Uingereza (DFID), Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo la Kanada (DFATD), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Jumuiya ya Ulaya (EU), Shirika la Kimataifa la Upatikanaji wa Chanjo Duniani (GAVI), Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF), Mfuko wa Afya wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI (Global Fund), Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA), Shirika la Maendeleo la Japani (JICA), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW), Shirika la Ushirikianao wa Kimataifa la Elimu ya juu la Uholanzi (NUFFIC), Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (OPEC), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA), Mfuko wa Suzan Thompson Buffet, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Pamoja (AGTF), Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP), Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), Serikali ya ufalme wa Norway, Serikali ya Marekani na Benki ya Dunia.

Mchanganuo wa taarifa za fedha 299 za mwaka 2022/23 ulionesha kuwa jumla ya Sh. trilioni 6.50 ambazo ni fedha za mradi zilipokelewa. Kati ya hizo, Sh. trilioni 4.19 zilitumika, na kuacha salio la Sh. trilioni 2.31 hadi 30 Juni 2023. Maelezo ya uchambuzi huu kwa kina kwa kila sekta ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 8**.

Jedwali 8: Uchambuzi wa utendaji wa kifedha kwa kila sekta

Sekta	Idadi ya Taarifa za Fedha	Fedha zilizopo (Sh./Mil)	Fedha zilizotumika (Sh./Mil)	Bakaa (Sh. /Mil)
Kilimo	7	42,935.71	32,573.34	10,362.37
Elimu	29	1,009,382.98	716,929.45	292,453.53
Nishati na Madini	16	992,137.56	423,789.97	568,347.59
Afya	198	1,017,268.29	701,165.17	316,103.11
Kijamii	13	634,260.06	491,220.47	143,039.59
Uchukuzi	9	1,456,118.53	1,192,982.02	263,136.51
Watu	9	1,048,820.71	525,543.93	523,276.78
Nyinginezo	18	302,574.21	107,249.73	195,324.47
<b>Jumla</b>	<b>299</b>	<b>6,503,498.03</b>	<b>4,191,454.11</b>	<b>2,312,043.92</b>

Chanzo: Taarifa za ukaguzi 2022/23

### 4.3 Usimamizi wa Matumizi

#### 4.3.1 Fedha za miradi zilizokopwa bila kurejeshwa Sh. bilioni 4.55

Miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo inahitaji kuzingatia makubaliano ya ufadhili wa kifedha ili kuhakikisha watekelezaji wa miradi wanatumia fedha katika shughuli zilizokusudiwa.

Nilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST) ilikopa Sh. 4,549,015,746 ambazo zilitengwa kwa ajili ya miradi miwili ya sekta ya elimu bila kurejeshwa. Hatua hii inakiuka sheria na masharti yaliyobainishwa katika mikataba ya fedha za mradi na miongozo ya utekelezaji wa miradi inayosimamia uendeshaji wa miradi hii. Maelezo kuhusu fedha zilizokopwa na kutorejeshwa yamebainishwa katika **Jedwali 9**.

Jedwali 9: Fedha zilizokopwa pasipo kurejeshwa

Na.	Jina la Mradi	Maelezo	Kiasi (Sh.)
1	Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)	Fedha zilitumika kutekeleza shughuli nyingine	388,045,000
2	Mradi wa Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu -Awamu ya II (GPE LANES II)	Malipo yalifanywa kwa wazabuni wa Programu ya Matokeo Makubwa sasa katika Elimu (EPforR)	4,160,970,746
<b>Jumla</b>			<b>4,549,015,746</b>

Chanzo: Hati za malipo na viambatisho vyake kwa mwaka 2022/23

Upungufu huu ulitokana na: uhibitaji wa ndani isiojitosheleza wa usimamizi wa fedha za mradi, pamoja na uhamishaji wa fedha kutoka Mradi wa Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu - Awamu ya II (GPE LANES II) kuwalipa wazabuni wa Programu ya Matokeo Makubwa sasa katika Elimu (EPforR) ili kuepusha malipo ya riba. Hata hivyo, kushindwa kurejesha fedha hizi zilizokopwa kwa miradi husika kunaleta kikwazo katika kufikia malengo ya mpango wa SEQUIP na LANES, jambo linaloweza kusababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.

Ninaishauri Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha fedha zilizokopwa zinarejeshwa kwenye miradi husika bila kuchelewa ili kuepuka kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

#### 4.3.2 Kodi ya zuio kutokatwa na kutowasilishwa Katika Mamlaka ya Mapato Tanzania - Sh. bilioni 6.33

Kifungu cha 83(1) (c) (i) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 (R.E 2019) kinataka kuzuiliwa kwa kodi ya mapato kutokana na malipo yanayofanywa kwa watu wasio wakazi kwa huduma zinazotolewa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, huku wakazi wakitowazwa ushuru wa 5% na wasio wakazi 15%. Pia, Kifungu cha 83 (A) na Aya ya 4(c) (v) cha Jedwali Na. 1 la Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332 kinataka kila taasisi kukatwa 2% kwa bidhaa na 5% kwa huduma zinazotolewa kwa taasisi za serikali; na kiasi kilichozuiliwa kinatakiwa kuwasilishwa kwa Kamishna wa Kodi ya Mapato.

Nilibaini kuwa watekelezaji watatu wa miradi hawakukata kodi ya zuio ya Sh. 1,118,230,367, wakati wawili walizuia kodi ya Sh. 5,216,572,492 lakini hawakuwasilisha Mamlaka ya Mapato Tanzania. Jumla ya kodi ambayo haikukatwa na ile ambacyo ilikatwa lakini hakikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ni Sh. 6,334,802,859. Maelezo yanaoneshwa kwenye **Jedwali 10**.

#### Jedwali 10: Watekelezaji wa miradi ambao hawakuwasilisha kodi ya zuio

Na.	Jina la Mradi	Sekta	Watekelezaji wa Mradi	Kiasi (Sh.)
<b>Watekelezaji ambao hawakukata na kuwasilisha kodi ya zuio</b>				
1.	Mradi wa Kuboresha Barabara ya Kimataifa: Rumonge - Gitaza (km 45) na Kabingo - Kasulu - Manyovu (km 260)	Uchukuzi na Mawasiliano	Wakala wa Barabara Tanzania	1,103,472,926
2.	Mradi wa Huduma za Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni (SWASH)	Maji	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	11,017,365
3.	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya III - Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN II)	Jamii	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii	3,740,076
<b>Jumla Ndogo</b>				<b>1,118,230,367</b>
<b>Watekelezaji wa miradi ambao walikata na kutowasilisha kodi ya zuio</b>				
Na.	Mradi	Sekta	Mtekelezaji	Kiasi (Sh.)
1.	Mradi wa Kuboresha Barabara ya Kimataifa ya Rumonge - Gitaza (km 45) na Kabingo - Kasulu - Manyovu (km 260.6)	Transport	Wakala wa Barabara Tanzania	5,172,142,866
2.	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya III - Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN II)	Jamii	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii	44,429,625
<b>Jumla Ndogo</b>				<b>5,216,572,491</b>
<b>Jumla Kuu</b>				<b>6,334,802,859</b>

**Chanzo:** Taarifa za ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23

Watekelezaji wa miradi kutokukata kodi ya zuio kutokana na njia inayoruhusu mkandarasi kulipwa fedha zote, ikiwamo kodi ya zuio iliyopaswa kuzuiwa na mkandarasi kuwa na jukumu la kuwasilisha kiasi hicho Mamlaka ya Mapato Tanzania, kumechangia kodi ya zuio kutowasilishwa. Sababu nyingine ni manejimenti za watekelezaji wa miradi kushindwa kuwasilisha kodi ya zuio kwa wakati Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Ninashauri menejimenti za taasisi husika zitekeleze utaratibu madhubuti wa kuhakikisha kuwa kodi ya zuio inakatwa kwa wakati na kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Kuwasilisha kwa wakati kodi ya zuio TRA kutarahisisha ukusanyaji wa kodi mapema. Pia, kunapunguza ukwepaji na gharama za ukusanyaji.

#### **4.3.3 Fedha ambazo hazikutumika katika akaunti ya masurufu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali - Sh. bilioni 1.29**

Aya ya 3.11 ya Waraka wa Uhasibu Na. 1 wa 2021/22 Ref EG.3/102/07/141 wa tarehe 7 Juni 2022 na Waraka wa Uhasibu Na. 7 wa mwaka 2020/21 iliyotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali kuhusu utayarishaji wa taarifa za fedha, inabainisha kuwa akaunti ya masurufu ni kwa ajili ya malipo kwa niaba ya watumishi na kwa shughuli maalumu. Aya hiyo inawataka maafisa masuuli kuhakikisha akaunti hiyo haibaki na fedha ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, akaunti ya masurufu ya miradi miwili ya sekta ya elimu ilikuwa na Sh. 1,295,955,000 ambazo hazijatumika, ambapo mradi wa BOOST ulikuwa na Sh. 1,046,585,000 na Mradi wa kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) ulikuwa na Sh. 249,370,000. Miradi hii inatekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Kuwapo kwa fedha ambazo hazijatumika kulitokana na kuweka fedha kwenye akaunti za masurufu kwa shughuli ambazo bado hazijaanza na kuchelewa kuanza kwa shughuli zilizopangwa kufanyika baada ya kutolewa kwa fedha hizo; hivyo, kusababisha uwezekano wa matumizi yasiyokusudiwa ya fedha hizo.

Ninashauri Menejimenti itenge fedha kwenye akaunti ya masurufu kwa ajili ya shughuli zilizo tayari kutekelezwa ili kuepuka akaunti hizo kubaki na fedha mwishoni mwa mwaka. Aidha, maafisa masuuli wanapaswa kushirikiana na Mhasibu Mkuu wa Serikali kuziagiza benki zihakikishe kuwa ifikapo mwishoni mwa mwaka wa fedha zirejeshe fedha ambazo hazijatumika katika akaunti ya masurufu kwenye akaunti ya makusanyo ya Benki Kuu ya Tanzania ili kuzihamishia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

#### 4.3.4 Ucheleweshaji uliosababishwa na Mfumo wa Malipo wa “D - Fund” kuidhinisha uhamisho wa fedha za Chuo Kikuu Mzumbe - Sh. bilioni 3.31

Kifungu cha 3(2)(vii) cha Mkataba wa Ruzuku, Juni 2022, kati ya Chuo Kikuu cha Mzumbe na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST) kinaeleza kuwa Chuo Kikuu kina jukumu la kutumia na kuomba fedha za mradi kwa wakati unaofaa kulingana na mizunguko ya utoaji fedha iliyoidhinishwa, kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Uwekezaji wa Kimkakati wa Chuo Kikuu ulioidhinishwa na Mpango Kazi wa Mwaka wa Chuo Kikuu cha Mzumbe. Mapitio ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) katika Chuo Kikuu Mzumbe yalionesha ucheleweshaji wa kuhamisha fedha kutokana na kutumia mfumo wa malipo wa “D-Fund” kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli 13 zenye jumla ya Sh. bilioni 3.31 ambazo ziliombewa fedha. Maombi haya yalicheleweshwa kwa siku 31 hadi 196, hivyo kuathiri ununuzi wa vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Sh. 1,058,994,534) na vifaa vya mawasiliano (Sh. 271,871,937.62), na kusababisha kucheleweshwa kwa malipo kwa mzabuni; pia ilisababisha ukiukwaji wa masharti ya mkataba.

Ucheleweshaji wa mradi ulisababishwa na mchakato mrefu wa kuidhinisha uhamishaji wa fedha kwa njia ya mfumo wa malipo wa “D - Fund” na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wizara ya Fedha. Ucheleweshaji huo uliathiri utekelezaji wa shughuli za mradi, hivyo kuwanyima walengwa kunufaika na huduma kwa wakati.

Ninashauri Menejimenti ya Chuo Kikuu Mzumbe kuwasiliana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wizara ya Fedha ili kushughulikia suala la ucheleweshaji wa uidhinishaji wa fedha za mradi kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa wakati.

#### 4.3.5 Malipo yaliyofanywa bila vipimo vya kazi na kuidhinishwa na Mhandisi Sh. milioni 582.53

Kanuni ya 243(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya 2013 inazitaka taasisi zinazofanya ununuzi ziidhinisha malipo kwa kuzingatia vipimo vilivyoidhinishwa katika vipindi maalumu vya mkataba. Aidha, Aya ya 25.3 ya Mwongozo wa kuendesha miradi kupitia Akaunti ya Nguvu Kazi (force account) uliotolewa na Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) Mei 2020 inahitaji vipimo vya pamoja vya kazi zilizokamilika kufanywa na Meneja wa Mradi kwa kushirikiana na taasisi inayotekeleza mradi.

Nilibaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ililipa jumla ya Sh. 582,529,629 kwa mafundi na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa

miundombinu ya shule na vyuo vya ualimu, ikiwa ni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, matundu ya vyoo, majengo ya utawala na majiko. Wizara ilifanya malipo katika miradi mitatu bila kutumia nyaraka za vipimo vya kazi ili kuthibitisha kazi zilizotekelezwa. Maelezo ya kazi ambazo zilifanywa bila nyaraka za vipimo vya kazi yameoneshwa kwenye **Jedwali 11**.

**Jedwali 11: Malipo yaliyofanywa bila vipimo vya kazi iliyofanyika**

Na.	Jina la Mradi	Sekta	Jina la Mtekelezaji	Kiasi (Sh.)
1	Programu ya Matokeo Makubwa sasa katika Elimu	Elimu	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	311,088,583
2	Mradi wa Huduma za Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni (SWASH)	Maji	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	160,957,067
3	Mradi wa Uwezesaji Kupitia Ujuzi (ESPJ)	Elimu	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	110,483,979
<b>Jumla</b>				<b>582,529,629</b>

**Chanzo:** Taarifa ya ukaguzi iliyowasilishwa kwa watekelezaji 2022/23

Pia, Mradi wa Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu - Awamu ya II unaotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ulifanya malipo ya Sh. 47,893,028 kwa mafundi bila kuhakikiwa na kuthibitishwa na meneja wa mradi.

Kutokusimamia ipasavyo kulikotokana na upungufu wa watumishi katika idara ya ujenzi kulisababisha kuidhinishwa kwa malipo bila kukagua, kutathimini na kupima kazi. Hii inaweza kusababisha malipo kufanyika kwa zaidi ya kiasi kilichopaswa kulipwa, au kufanya malipo ya kazi ambazo hazijakamilika. Pia, inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Ninawashauri wasimamizi wa miradi kuhakikisha kuwa kazi zinakaguliwa na kupimwa kabla ya kuidhinisha malipo ili kuzuia malipo ya ziada na malipo ya kazi zisizokamilika.**

#### 4.3.6 Fidia ambayo haijalipwa kwa Watu walioathirika na Mradi - Sh. bilioni 13.69

Kifungu cha 3(1) (g) cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, kinahitaji fidia kamili, ya haki, na kwa wakati kwa watu ambao haki zao za umiliki wa ardhi zimesitishwa au kumilikiwa na serikali. Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Utwaaji Ardhi, Sura ya 118 pia kinataka malipo ya fidia, pamoja na riba ya asilimia sita kwa mwaka kuanzia tarehe ya kumiliki ardhi hadi tarehe ya malipo, endapo ardhi itachukuliwa kabla ya malipo ya fidia kufanyika.

Mapitio ya miradi sita yalionesha kutolipwa fidia ya Sh. bilioni 13.69 kwa watu 567 walioathirika na miradi. Kati ya kiasi hicho, Sh. bilioni 12.67 kinahusisha miradi mitano. Mradi wa Maendeleo wa Nishati ya Jua Tanzania ulikuwa na

nyongeza ya fidia iliyokadiriwa kuwa Sh. bilioni 1.02. Licha ya miradi minne kukaribia kukamilika (97% hadi 100%), malipo ya fidia hayakufanyika kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 12**.

**Jedwali 12: Fidia ambayo haijalipwa kwa Watu walioathirika na Mradi**

Na.	Jina la Mradi	Sekta	Watekele zaji	Walioathirika na Mradi	Kiasi (Sh.)	Hali Halisi
1	Mradi wa Kuunganisha Umeme Kenya na Tanzania (KTPIP)	Nishati na Madini	Shirika la Umeme Tanzania	81	12,226,277,532	97.4
2	Mradi wa Maendeleo wa Nishati ya Jua - (TSDP)	Nishati na Madini		Hawakuta mbuliwa	1,016,626,298	Utekele zaji wa mradi
3	Mradi wa Kusafirisha Umeme Mkubwa na Uwekaji Umeme Vijijini - Geita- Nyakanazi kv 220	Nishati na Madini		328	333,420,965	100
4	Mradi Endelevu wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Jijini Arusha	Maji		18	63,452,923	100
5	Mradi wa Umeme wa Maporomoko ya Maji ya Mto Rusumo	Nishati na Madini		34	28,001,890	100
6	Mradi wa Kufua Umeme katika Mto Malagarasi	Nishati na Madini		106	22,819,084	Utekele zaji wa mradi
<b>Jumla</b>				<b>567</b>	<b>300</b>	

Chanzo: Taarifa ya Fidia, 2022/23

Mapungufu yalisababishwa na mawasiliano duni, ugumu wa kutambua wamiliki halali, kuwapo kwa migogoro ya ardhi, taarifa zisizojitoshesheza, pamoja na ucheleweshaji wa kutoa fedha kwa ajili ya malipo ya fidia. Changamoto hizi zinaathiri uhusiano na jamii. Pia, zinaweza kuhatarisha maendeleo endelevu ya miradi kwa siku zijazo, pamoja na kuongeza gharama ya fidia kutokana na mabadiliko ya kiuchumi.

Ninashauri menejimenti husika ziweke kipaumbele na kuharakisha malipo ya fidia. Pia, zifanye kazi na mamlaka za serikali za mitaa ili kuthibitisha umiliki, kutatua migogoro, na kuhakikisha malipo ya fidia yanafanywa kwa wakati.

#### 4.4 Usimamizi wa Bajeti

##### 4.4.1 Upungufu wa Sh. bilioni 16.28 ulioathiri malipo ya wakandarasi kwa wakati

Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), kupitia Mradi wa Kujenga Ujuzi na Ushirikano Afrika Mashariki (EASTRIP) inajihusisha na ujenzi wa Kituo cha Kikanda cha Umahiri wa TEHAMA (RAFIC) na majengo ya hosteli za wanafunzi. Mradi huo ulitarajiwa kukamilika tarehe 7 Februari 2024.

Kufikia tarehe 1 Agosti 2023, nilibaini kuwa ujenzi ulikuwa umefikia 13% ya ukamilishaji, ukikaribia hatua muhimu, ambapo fedha zinahitajika kwa kiasi kikubwa ili kulipa Hati za malipo kwa siku zijazo kwa kazi zitakazofanywa. Hata hivyo, nilibaini kuwapo kwa upungufu wa fedha katika utekelezaji wa mradi. Upungufu huo unaweza kusababisha malipo kufanywa kwa kuchelewa na kusababisha malipo ya tozo ya kuchelewesha malipo ambapo kunaweza kupelekea ongezeko la gharama za mradi.

Hadi kufikia Agosti 2023, mradi ulikuwa na kiasi cha Sh. 9,071,639,969 dhidi ya kiasi cha Sh. 15,871,200,000 ambacho kilikuwa hakijalipwa kulingana na kazi za kimkataba zilizokuwa zimefanywa, ikiashiria upungufu wa Sh. 6,799,560,032. Aidha, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) ilikadiria mahitaji ya fedha ya jumla ya Sh. 25,347,256,553 kwa kazi iliyobaki ya ujenzi; hivyo kufanya upungufu wa Sh. 16,275,616,584 (Sh. 25,347,256,553 - Sh 9,071,639,969).

Ninashauri kuwa Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam ijadiliane na Benki ya Dunia kwa lengo la kurekebisha viashiria vinavyohusishwa na utoaji wa fedha ili kiasi cha fedha cha Sh. bilioni 16.28 kitolewe kwa wakati kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa wa Kituo cha Kikanda cha Umahiri wa TEHAMA (RAFIC).

#### 4.4.2 Kutofadhili miradi midogo ya jamii iliyoidhinishwa yenye thamani ya Sh. bilioni 6.71

Aya ya 2.5.3 (iii) na (iv) ya Kitabu cha Mwongozo wa Miundombinu iliyopangwa kutekelezwa pamoja na majukumu mengine ya Kitengo cha Usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TMU) kuhusu miundombinu iliyokusudiwa kutekelezwa inaeleza kuwa Kitengo kinapaswa kuhakikisha kuwa miradi yote midogo inapitishwa na kamati ya uendeshaji ya kitaifa kabla ya kutolewa kwa fedha. Pia, kinapaswa kuhakikisha kuwa fedha zinatolewa kwa wakati kwenye miradi midogo ambayo imeidhinishwa kutekelezwa.

Ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF III-PSSN II) katika mamlaka 10 za Maeneo ya Miradi (PAAs) umebaini kuwa Kamati ya Uongozi ya Taifa (BMT) iliidhinisha miradi midogo ya Miundombinu Lengwa, Shughuli za Kuzalisha Mapato (IGAs) na Mpango wa Ujenzi wa Miradi (PWP) wenye thamani ya Sh. bilioni 6.71. Hata hivyo, shughuli hizo za mradi hazikufadhiliwa na TMU hadi Agosti 2023. Maelezo zaidi yametolewa katika Jedwali 13.

**Jedwali 13: Miradi iliyoidhinishwa haikufadhiliwa**

Na.	Eneo la utekelezaji	Kiasi (Sh.)	Na.	Eneo la Watekelezaji	Kiasi (Sh.)
1	Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema	1,041,706,841	7	Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba	605,926,418
2	Halmashauri ya Wilaya ya Monduli	1,039,573,692	8	Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro	588,217,625
3	Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa	957,910,516	9	Halmashauri ya Mji wa Geita	66,927,303
4	Halmashauri ya Wilaya ya Longido	925,517,196	10	Halmashauri ya Wilaya ya Karatu	53,930,000
5	Halmashauri ya Jiji la Mwanza	813,370,338	<b>Jumla</b>		<b>6,712,213,799</b>
6	Halmashauri ya Manispaa ya Ilemele	619,133,868			

Chanzo: Taarifa za utekelezaji wa miradi, 2022/23

Ukosefu wa fedha kutoka TMU kwa ajili ya miradi midogo ulitokana na utoaji wa fedha usiopangwa na ufinyu wa bajeti, hivyo kupelekea uwezekano wa ucheleweshaji wa malengo ya mradi.

Ninapendekeza Kitengo cha Usimamizi cha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TMU) kutoa fedha kwa wakati ili kugharamia miradi midogo iliyoidhinishwa.

#### 4.4.3 Ucheleweshaji wa utoaji wa fedha za bajeti iliyoidhinishwa Sh. bilioni 301.78

Utoaji wa fedha za mradi unatarajiwa kuendana na mzunguko wa bajeti na ratiba ya utekelezaji wa shughuli za mradi, kama ilivyoidhinishwa katika Mpangokazi wa Mwaka (AWP) wa kila mradi.

Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa ucheleweshaji wa utoaji wa fedha za miradi unaokiuka mzunguko wa bajeti uliyoidhinishwa na mpango kazi wa mwaka. Wizara ya Fedha ilichelewa kuhamisha Sh. bilioni 301.78 kwenda kwenye miradi iliyo chini ya Wizara ya Maji, Wizara ya Afya, na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela-Afrika. Ucheleweshaji huo ulikuwa wa miezi miwili hadi minane toka tarehe iliyopangwa fedha kutolewa hadi tarehe halisi za kupokea kama ilivyobainishwa kwenye Jedwali 14.

**Jedwali 14: Ucheleweshaji wa utoaji wa fedha za bajeti iliyoidhinishwa**

Na.	Mradi	Tarehe ya kupokea fedha	Tarehe fedha zilipopokelewa	Ucheleweshaji (Miezi)	Kiasi (Sh. Milioni)
1	Programu ya Usambazaji wa Huduma ya Majisafi Vijijini (SRWSSP) - Kitengo cha Uratibu	Octoba 2022	Juni 2023	8	296,200.49
2	Mradi wa kuimarisha Utoaji wa Huduma za Afya ya Uzazi na Mama	Septemba 2022	Novemba 2022	2	4,880.31

Na.	Mradi	Tarehe ya kupokea fedha	Tarehe fedha zilipopokelewa	Ucheleweshaji (Miezi)	Kiasi (Sh. Milioni)
	na Mtoto wa Taasisi ya "Susan Thomson Buffet Foundation Support"				
3	Kituo cha Umahiri cha Utafiti wa Kilimo, Sayansi ya Chakula na Usalama wa Lishe	Januari 2023	Septemba 2023	8	698.46
		Machi 2023	Agosti 2023	5	
<b>Jumla</b>					<b>301,779.28</b>

Chanzo: Mpangokazi wa Mradi na kitabu cha fedha

Ucheleweshaji wa utoaji wa fedha ulisababishwa na taratibu za usajili, vikwazo vya kiutawala, na ucheleweshaji wa kupata hati muhimu na ripoti za uhakiki. Sababu hizi ziliathiri utekelezaji wa shughuli kwa wakati na uwezekano wa kuathiri mafanikio ya jumla ya miradi.

**Ninashauri Watekelezaji wa Miradi kufanyia kazi vikwazo zinavyosababisha ucheleweshaji wa fedha; hivyo kuhakikisha fedha za bejeti iliyoidhinishwa zinapokelewa ndani ya muda uliokubaliwa ili kuwezesha utekelezaji wa mradi kufanyika kwa ufanisi kwa lengo la kufikia malengo yaliyokusudiwa.**



### 5.1 Utangulizi

Usimamizi wa ununuzi katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa nchini Tanzania unasimamiwa na Sheria ya Ununuzi ya Umma, Sura ya 410, Kanuni zake za Mwaka 2013 (zilizofanyiwa marekebisho mwaka 2016) na miongozo ya ziada ya ununuzi, ambayo huandaliwa na Serikali ikishirikiana na Washirika wa Maendeleo. Sura hii inaeleza upungufu uliobainika katika usimamizi wa ununuzi katika miradi ya maendeleo.

### 5.2 Kuchelewa kusainiwa kwa mikataba miwili yenye thamani ya Sh bilioni 6.24 kwa kipindi cha kuanzia siku 82 hadi 86

Kanuni ya 233 (1) ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016 na (Tangazo la Serikali namba 333 la tarehe 30/12/2016) vinitaka taasisi nunuzi na mzabuni au mtoa huduma husika kuingia mkataba wa ugavi wa bidhaa, utoaji wa huduma au utekelezaji wa miradi ndani ya siku kumi na nne za kazi baada ya kutimiza masharti yote kabla ya kusainiwa kwa mkataba.

Nilibaini kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) lilichelewa kusaini mikataba miwili yenye jumla ya Sh. 6,238,603,988 kwa kipindi cha kuanzia siku 82 hadi 86. Rejea **Kiambatisho Na. II**.

Kuchelewa huku kulisababishwa na mchakato wa utaratibu wa kupata idhini kutoka kwa wafadhili. Wazabuni walitumia muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa kuwasilisha hati ya dhamana ya utendaji kazi kulingana na matakwa ya mkataba na upekuzi wa mikataba kuchukua muda mrefu. Kuchelewa kusaini mkataba kuliathiri kuleta kwa wakati bidhaa na kutoa huduma kwa umma; hivyo, kuchelewa kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Ninapendekeza kuwa uongozi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania uhakikishe kuwa michakato ya ununuzi na kusaini mikataba katika miradi ijayo vinafanyika ndani ya muda unaokubaliwa kwenye kipindi cha zabuni kama inanavyoelezwa katika kanuni za ununuzi.

### 5.3 Matumizi ya zabuni ya ushindani ya kitaifa kupitia wazabuni maalumu katika kutoa huduma zenye thamani ya Sh bilioni 3.55

Sehemu ya 1.6.1 ya Mwongozo wa Ununuzi kwa Mikataba inayofadhiliwa na AFD (Shirika la Maendeleo la Kifaransa) katika nchi za kigeni unamtaka mnufaika kufanya ushindani katika ununuzi wa kimataifa katika kutekeleza mpango wa ununuzi ulioidhinishwa na AFD kulingana na barua ya idhini.

Katika ukaguzi wa mkataba Na. AE/042/2022-2023 uliosainiwa tarehe 16 Mei 2023, kati ya MWAUWASA na Ursino Ltd JV pamoja na M/S. RJR Construction Co. Ltd, wenye thamani ya Sh. 3,549,714,315, kwa ajili ya ujenzi wa tanki la zege la kuhifadi maji katika mji wa Kisesa, Mkoa wa Mwanza, uliofanyika chini ya Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (LVWATSAN), nilibaini kuwa MWAUWASA ilichagua zabuni ya kitaifa ya ushindani kupitia wazabuni maalumu (*restricted tendering*).

Menejimenti ya MWAUWASA ilieleza kuwa uchaguzi wa zabuni kupitia wazabuni maalumu badala ya zabuni za ushindani wa kimataifa ulisababishwa na ongezeko la mahitaji ya maji jijini Mwanza pamoja na uhaba wa vifaa vya kuhifadhia maji. Ni maoni yangu kuwa sababu hii haitoshelezi ukiukaji wa taratibu za ununuzi. Matumizi ya zabuni kupitia wazabuni maalumu huzuia wazabuni wengine kushiriki katika ununuzi, hivyo kuzuia mradi kufaidika na bei zitokanazo na ushindani.

Ninapendekeza kuwa uongozi wa MWAUWASA uhakikishe na utoe kipaumbele katika uzingatiaji wa masharti ya wafadhili na kutumia utaratibu wa zabuni za ushindani wa kimataifa katika miradi ya baadaye. Njia hii itanufaisha umma kwa upatikanaji wa bei za ushindani na upatikanaji wa bidhaa na huduma zenye ubora.

### 5.4 Kutotekelezwa kwa manunuzi yaliyopangwa yenye thamani ya Sh bilioni 13.74

Kanuni ya 69(3) ya kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013 inahitaji taasisi nunuzi kuandaa mpango wa ununuzi wa kila mwaka kwa ufanisi na kufanya makisio sahihi ya ununuzi na yanayotekelezwa.

Nilibaini kuwa miradi mitatu haikutekeleza mpango wa ununuzi wa huduma na bidhaa za jumla ya kiasi cha Sh 13,736,761,745, sawa na 57% ya mpango wa mwaka, licha ya kuwa na bajeti zilizoidhinishwa. Maelezo zaidi yametolewa katika **Jedwali 15**.

**Jedwali 15: Manunuzi ambayo yalipangwa lakini hayakutekelezwa**

Na	Jina la Watekelezaji mradi	Jina la Mradi	Bajeti ya mwaka iliyoidhinishwa (Sh)	Shughuli zilizotekelezwa (Sh)	Shughuli zisizotekelezwa (Sh)
1	Ofisi ya Waziri Mkuu	AFDP	14,192,639,312	3,057,928,368	11,134,710,944
2	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	HEET	2,468,970,000	1,549,650,000	919,320,000
3	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	SEQUI P	6,245,258,771	5,606,258,771	639,000,000
4	Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania	HEET	1,043,730,801	0	1,043,730,801
<b>Jumla (Sh)</b>			<b>23,950,598,884</b>	<b>10,213,837,139</b>	<b>13,736,761,745</b>

**Chanzo:** Mipango ya Ununuzi wa Mwaka na Ripoti ya Utekelezaji wa Ununuzi, 2022/23

Ukosefu wa ujuzi wa kutosha katika kuandaa mpango wa ununuzi na kuchelewa kutolewa kwa fedha na mamlaka husika ni sababu zilizochangia kutotekelezwa kwa ununuzi uliopangwa.

Hii inaweza kusababisha kutofautiana kati ya malengo ya mradi na hatua zilizopangwa kwenye bajeti. Pia, inaweza kuzuia kufikiwa kwa malengo na kuathiri mafanikio ya jumla ya miradi.

**Ninapendekeza kuwa uongozi wa miradi husika utambue na kuandaa mkakati utakaopunguza hatari zinazokwamisha kukamilika kwa kazi zilizopangwa za ununuzi, ikiwamo kuimarisha uwezo na kufanya mipangilio yenye ufanisi kwa ajili ya mtiririko wa fedha kwa utekelezaji unaofaa wa kazi zote za ununuzi zilizosalia.**

**5.5 Utekelezaji wa kazi za ujenzi zenye thamani ya Sh. bilioni 1.78 bila kusaini mkataba**

Kifungu cha 60 (7) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410, kinataka taasisi nunuzi na mzabuni kuingia mkataba wa ununuzi wa bidhaa, huduma au kazi baada ya ofa au pendekezo la ununuzi kukubaliwa.

Nilipitia taarifa za ununuzi ya Mpango wa kuboresha elimu (SEQUIP) unaotekelezwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) na kubaini malipo ya jumla ya Sh 1,528,253,924 yaliyolipwa kwa mafundi kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya shule za sekondari katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, Mtama, na Kilwa bila kuingia mikataba na mafundi hao (Kiambatisho Na. II kinatoa maelezo zaidi).

Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania, wanaotekeleza Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi (AFDP) na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN II) walilipa Sh 39,692,190 na Sh 213,000,000 matawaliwa kwa wazabuni mbalimbali bila kuingia nao mkataba rasmi.

Hii ilitokana na kutozingatiwa ipasavyo kwa sheria za ununuzi na watekelezaji wa miradi. Hali hii inaleta hatari ya kupatiwa bidhaa, huduma au kazi zenye viwango duni. Aidha, huenda ikasababisha matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Ninapendekeza kuwa uongozi husika uandae na kuingia mikataba na wazabuni kabla ya malipo kufanyika ili kulinda maslahi ya pande zote mbili.**

### **5.6 Ucheleweshaji wa malipo ya wazabuni ya Sh. bilioni 1.26**

Kifungu cha 19 cha Masharti Maalumu ya Mikataba Na. PA.13/WB-HEET-P166415/261505/2022/23/G/02, 04 na 05 kati ya Chuo Kikuu Mzumbe na M/S Freedom Incredible Connections Limited na PA.13/WB-HEET-P166415/261505/2022/23/G/05 kati ya Chuo Kikuu Mzumbe na M/S Kenel Business Holdings Company Limited kwa ajili ya usambazaji na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA kilihitaji malipo ya 100% ya bei ya mkataba yafanywe kwa wazabuni ndani ya siku 30 baada ya ombi la zabuni kukubaliwa.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwapo kwa ucheleweshwaji wa malipo ya kiasi cha Sh 1,261,244,180 kati ya siku 51 hadi 85 katika ununuzi wa vifaa vya TEHAMA na uhabarishaji. Ucheleweshwaji huu ulisababishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuchelewa kutoa kibali cha uhamisho wa fedha za HEET kutoka Benki Kuu kwenda katika akaunti ya mradi wa HEET ya Chuo Kikuu Mzumbe.

Mradi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe - HEET haukuwalipa wazabuni mara moja baada ya kuleta bidhaa au kutoa huduma. Hali hii inaweza kusababisha migogoro ya kimkataba, madai ya riba na kuharibu sifa ya serikali.

**Ninapendekeza kuwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe uhakikishe malipo kwa wazabuni yanafanyika kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya mkataba ili kuzuia migogoro inayoweza kujitokeza kutokana na ucheleweshaji wa kutimiza masharti ya mkataba.**

### 5.7 Malipo ya bidhaa yaliyofanyika bila hati ya kuagiza bidhaa Sh 2.51 bilioni

Kanuni ya 164(2)(j) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inahitaji ununuzi unaofanywa kwa kutumia nukuu za bei uambatanishwe na hati ya uagizaji bidhaa (LPO) iliyotolewa kwa mzabuni.

Ukaguzi wa ununuzi ulibaini kuwa miradi minne chini ya Sekta ya Elimu ililipa Sh. 2,514,199,890 kwa wazabuni mbalimbali wa bidhaa na huduma bila ya kuwa na hati ya kuagiza bidhaa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 16**.

**Jedwali 16: Ununuzi uliofanywa bila hati ya kuagiza bidhaa**

Na.	Jina la Mradi	Sekta	Watekelezaji wa mradi	Kiasi (Sh.)
1.	Programu ya Kuboresha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP)	Elimu	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	2,223,039,886
2.	Kukuza uwezo wa kujifunza kwa Wanafunzi wa Msingi (BOOST)	Elimu	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	132,264,375
3.	Matokeo Makubwa Sasa (BRN) katika Mpango wa Elimu kwa Matokeo (EPforR I)	Elimu	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	89,000,000
4.	Programu ya Elimu na Ujuzi kwa Ajira za Uzalishaji (ESPJ)	Elimu	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	69,895,629
<b>Jumla</b>				<b>2,514,199,890</b>

Chanzo: *Faili za Ununuzi 2022/23*

Hii ilitokana na kukosekana kwa mpangilio mzuri wa shughuli za ununuzi, hasa kwa mahitaji ya dharura. Hatua hii inaweza kuleta hasara kubwa ikiwa wauzaji hawatatoa bidhaa kama walivyoagiza kutokana na kukosekana kwa mikataba ya kisheria kati ya pande mbili husika.

Ninapendekeza watekelezaji wa mradi husika wahakikishe ununuzi wa bidhaa, vifaa au huduma unapangwa na kutekelezwa kwa kuandaa na kutumia hati ya kuagiza bidhaa.

# SURA YA SITA

## USIMAMIZI WA MIKATABA NA HALI HALISI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI



### 6.1 Utangulizi

Sura hii inafanua mambo muhimu kuhusu matokeo ya ukaguzi wa usimamizi wa mikataba na utendaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2023.

### 6.2 Usimamizi wa Mikataba

#### 6.2.1 Kuchelewa kukamilika kwa miradi ya Sh. bilioni 5.38 na kutotoza tozo ya kuchelewa kukamilisha miradi kwa wakati Sh. bilioni 3.1

Kanuni ya 114 (a) (b) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kuwa na jukumu la usimamizi madhubuti wa ununuzi, ikijumuisha gharama za ufuatiliaji, na kuhakikisha bidhaa na huduma zinapokelewa kwa wakati na kwa kiwango sahihi na ubora uliobainishwa katika mkataba. Pia, inaelekeza taasisi nunuzi zinafuatilia maendeleo na ukamilishaji wa kazi kwa wakati kulingana na masharti ya kila mkataba.

Katika ziara ya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ya miradi na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa mradi kati ya Oktoba na Novemba 2023, nilibaini kuwa miradi saba yenye thamani ya Sh. bilioni 4.51 ilichelewa kukamilika kwa kipindi cha kuanzia mwezi 1 hadi 7. Ucheleweshaji huu ulitokana na kukosekana kwa vifungu vya malipo ya fedha zilizopokelewa; uhamisho wa fedha mwishoni mwa mwaka; usimamizi na ufuatiliaji duni wa menejimenti; na kuchelewa kwa ujenzi wa miundombinu muhimu kwa ajili ya kufanya uhakiki uliopangwa.

Pia, nilibaini kuwa Wizara ya Afya ilichelewa kwa miezi mitano kupokea bidhaa za kuokoa maisha za SRH/MNCAH zenye thamani ya Sh. 878,308,245 kutoka Bohari ya Dawa (MSD) chini ya ufadhili wa Susan Thomson Buffet Foundation. Bidhaa hizo ambazo awali zilitarajiwa kupokelewa tarehe 28 Februari 2023 zilipokelewa Agosti 2023 kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na. IV**.



## Usimamizi wa Mikataba na Hali Halisi ya Utekelezaji wa Miradi

Aidha, ucheleweshaji mkubwa ulibainika katika miradi mitatu ambayo haikutoza tozo ya jumla ya Sh. 3,151,780,196 kwa kuchelewa kukamilisha miradi kwa wakati. Ucheleweshaji huu ulitokana na ongezeko la gharama ambalo hazikutarajiwa kutokana na marekebisho katika mikataba ya washauri elekezi pamoja na uwezo duni wa wakandarasi katika kutimiza majukumu yao ya kimkataba. Maelezo zaidi yanapatikana katika **Jedwali 17**.

### Jedwali 17: Kutotozwa tozo za ucheleweshaji

Walioingia mkataba	Mtekelezaji wa Mradi	Jina la Mradi	Tarehe iliyotarajiwa mradi kukamilika	Tarehe ya mradi kukamilika	Muda wa Kuchelewa	Tozo ya ucheleweshaji lsiyotozwa
TANESCO, Sterling & Wilson Pvt. Ltd, Electromontaj SA. UJV (SWE)	TANESCO	Ujenzi wa 220KV	30-Nov-20	18-Okt-23	Miezi 35	2,824,303,694
DAWASA, M/S Helpdesk Engineering Tanzania Ltd	Wizara ya Maji	Ujenzi wa vyoo vya umma Jijini Dar es Salaam	30-Apr-23	15-Sep-23	Siku 138	327,476,502
<b>Jumla</b>						<b>3,151,780,196</b>

**Chanzo:** Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23

Ninapendekeza kwamba serikali, wizara, idara na wakala wa serikali husika zihakikishe zinakuwa na vifungu vya matumizi ya fedha zote ili kuongeza uwazi na ufuatiliaji wa fedha. Aidha, mikakati ya utekelezaji wa miradi inapaswa kuwa ya uhakika ili kupunguza athari za uhamisho wa fedha mwisho wa mwaka. Pia, TANESCO na Wizara ya Maji zitekeleze adhabu za tozo za kimkataba kwa wacheleweshaji wa utekelezaji wa miradi. Vilevile, zichukue hatua madhubuti kuzuia ucheleweshaji wa miradi inayoendelea.

### 6.2.2 Mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 2.77 haikupitiwa na wanasheria

Kanuni ya 59 na 60 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kama zilivyofanyiwa marekebisho na kanuni ya 2 na 3 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2016 zinaeleza kuwa mkataba wowote ambao thamani yake ni chini ya shilingi bilioni moja unatakiwa kuhakikiwa na mwanasheria wa taasisi nunuzi.

Tathmini ya mchakato wa utoaji zabuni na usimamizi wa mikataba kwa mwaka wa fedha 2022/23 ilibaini kuwa mikataba ya miradi sita yenye thamani ya Sh. bilioni 2.77 ilitekelezwa bila kupitiwa na wanasheria, kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 18**. Hii inaashiria ongezeko la asilimia 10 kutoka thamani ya mikataba ambayo haikupitiwa mwaka uliopita, ambayo ilikuwa Sh. bilioni 2.51.

**Jedwali 18: Mikataba iliyosainiwa bila kupitiwa na wanasheria**

Jina la Mradi	Jina la Mtekelezaji wa Mradi	Kiasi (Sh.)
Programu ya BOOST ya Wanafunzi wa Elimu ya Msingi Kujifunza kusoma	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	147,972,745
Mradi wa Pili wa Kusaidia Sekta ya Maji	Wizara ya Maji	295,943,293
Mradi wa usafi wa maji shuleni (SWASH)	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	440,654,579
Programu ya BOOST ya Wanafunzi wa Elimu ya Msingi Kujifunza kusoma	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI)	717,156,500
Matokeo Makubwa Sasa katika Elimu (BRNed) Mpango wa Matokeo (EPforR I)	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	847,478,627
Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu - Msaada wa Elimu ya Kusoma na Kuhesabu (LANES) II PROGRAMME	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (KURA 46)	317,716,500
<b>Jumla</b>		<b>2,766,922,244</b>

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23

Chanzo kikuu cha ukiukwaji huu unatokana na ukosefu wa mifumo ya udhibiti wa ubora wakati wa maandalizi na uhakiki wa mikataba. Hali hii inaweza kusababisha migogoro ya kisheria, hasara za kifedha, pamoja na kuharibu sifa ya taasisi.

Ninapendekeza kwamba wizara, idara na wakala husika ziteue wanasheria katika miradi mahususi kwa ajili ya ukaguzi wa mikataba na mwongozo wa kisheria, hivyo kupunguza hatari ya kutokea kwa migogoro ya kisheria na upotevu wa fedha.

### 6.2.3 Gharama za ziada za mradi kutokana na mabadiliko ya usanifu wa mchoro wa kituo cha mabasi - Sh. bilioni 28.05

Tarehe 10 Disemba 2018 TANROADS iliingia mkataba na SINOHYDRO Corporation Ltd kwa ajili ya Awamu ya 2 Sehemu ya 1 ya Miundombinu ya BRT Dar es Salaam yenye urefu wa kilomita 20.3 za ujenzi wa barabara, ikijumuisha barabara za juu mbili na vituo 29 vya mabasi. Mkataba wa awali ulikuwa Sh. 189,433,784,506; baadaye ulirekebisha na kuwa Sh. 217,480,899,399. Hii inamaanisha kulikuwa na ongezeko la gharama la Sh. 28,047,114,893 kutokana na marekebisho ya usanifu.

Mabadiliko haya yalisababishwa na upungufu katika upembuzi yakinifu na mapitio ya awali ya usanifu, ukijumuisha usanifu upya wa kituo cha mabasi, kuta za ziada za kuhifadhi barabara za Kilwa na Kawawa, na ujenzi wa daraja la juu la Bandari na mizunguko ya njia-panda. Haya yaliathiri gharama za mradi na muda wa kukamilika. Hapo awali mradi ulipangwa kukamilika ifikapo tarehe 5 Mei 2022, tarehe ya kukamilika iliongezwa hadi 9 Oktoba 2023. Tatizo hilo liliathiri gharama na kuchelewesha kukamilika kwa mradi.

Ninapendekeza TANROAD ifanye upembuzi yakinifu wa kina na mapitio ya usanifu wa kina kabla ya kuanzisha miradi kama hiyo kwa siku za usoni ili kuzuia gharama kubwa za usanifu mpya; hivyo kupunguza gharama na ucheleweshaji wa kukamilisha mradi.

#### 6.2.4 Riba ya Sh. bilioni 3.08 iliyotozwa kutokana na kucheleweshwa kwa malipo ya wakandarasi na kutotumika kwa mkopo

Kifungu cha 14.7 (c) na 14.8 cha Masharti ya Mikataba kinabainisha kwamba wakandarasi wanastahili kulipwa riba ambayo huongezeka kila mwezi kwa malipo yanayochelewa kwa zaidi ya siku 56 baada ya meneja wa mradi kupokea nyaraka za malipo yao. Kifungu cha 2.03 cha Mikataba wa Mkopo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na TANESCO kuhusu mradi wa Tanzania Zambia Interconnection Project (TAZA) kinataka kutozwa riba ya hadi 0.5% kwa mwaka kwenye salio la mkopo ambalo halijalipwa, kuanzia siku 120 baada ya makubaliano na tarehe ya malipo.

TANESCO, TANROADs, Wizara ya Maji, na Wizara ya Maliasili na Utalii zilitozwa tozo ya jumla ya Sh. 3,077,359,166 kutokana na ucheleweshaji wa malipo ya madai ya wakandarasi na tozo za ahadi kutokana na kutozingatiwa kwa mikataba ya mikopo. TANESCO ilikuwa na tozo za riba ya Sh. 2,129,506,978 (sawa na asilimia 69) kutokana na ucheleweshaji wa kutumia mkopo katika Mradi wa TAZA.

TANROADS ilipata tozo ya riba ya jumla ya Sh. 874,996,553 (asilimia 28.4), ambapo Sh. 817,694,357 zilitokana na kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi na Sh. 57,302,196 kama tozo ya kutotumia salio la mkopo katika kutekeleza shughuli zilizopangwa za mradi. Wizara ya Maji na Wizara ya Maliasili na Utalii zilikabiliwa na tozo ya riba ya Sh. 25,004,367 (asilimia 0.8) na Sh. 47,851,268 (asilimia 1.6) mtawalia. Zote zilihusiana na ucheleweshaji wa madai ya wakandarasi katika utekelezaji wa miradi mahususi ambayo ni Mradi wa Pili wa Kusaidia Sekta ya Maji na Usimamizi Endelevu wa Maliasili na Utalii na Ukuaji. Maelezo zaidi yanapatikana katika **Kiambatisho V**.

Gharama za riba zilitokana na utendaji hafifu wa taasisi za serikali katika kutoa fedha pamoja na utumiaji wa mikopo; hivyo kusababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi. Usimamizi huu mbaya wa fedha za umma unadhoofisha ufanisi na ufasaha wa taasisi husika. Ni muhimu kufanya malipo kwa wakati na kuzingatia masharti ya mkopo ili kuzuia matumizi mabaya ya rasilimali za umma.



## Usimamizi wa Mikataba na Hali Halisi ya Utekelezaji wa Miradi

Ninapendekeza kwamba serikali ihakikishe fedha zinatolewa kwa wakati ili kupunguza ucheleweshaji wa malipo na kutekeleza usimamizi na ufuatiliaji thabiti wa miradi ili kuhakikisha inafuata makubaliano ya kifedha, hivyo kuzuia utozwaji wa riba ya kuchelewesha malipo ya wakandarasi na kutofuata masharti ya matumizi ya mikopo.

### 6.2.5 Ukosefu wa dhamana ya utendaji ili kufidia wigo wa nyongeza ya mkataba wa Sh. bilioni 1.54

Kanuni ya 29 (5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inataka iwapo mkataba unarekebisha baada ya kusainiwa, na kusababisha ongezeko la gharama la zaidi ya 10%, mkandarasi atatakiwa kutoa dhamana ya ziada ya utendaji kazi ili kufidia ongezeko la mkataba la zaidi ya asilimia 10.

Mnamo tarehe 23 Mei 2023, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) chini ya mradi wa SEQUIP iliingia mikataba na M/s Mbese Books Distributors Limited na M/s Nyambari Nyangwine Group of Companies kwa ajili ya uchapishaji na usambazaji wa vitabu vya kiada. Awali, mikataba hiyo ilikuwa na thamani ya Sh. 3,700,000,000 na Sh. 5,300,867,250 mtawalia. Mikataba yote miwili iliongezeka kwa asilimia 15 kupitia nyongeza ya mkataba Na. 1 ya tarehe 7 Juni 2023. Hii ilisababisha thamani ya mkataba kuongezeka hadi Sh. 4,255,000,000 na Sh. 6,095,997,338 mtawalia. TET pia iliingia mkataba na M/s Mbese Books Distributors Limited mnamo tarehe 23 Juni 2023 kwa ajili ya vifaa ya kuchapishla vitabu vya maandishi ya nukta nundu vyenye thamani ya Sh. 1,288,000,000. Mkataba uliongezeka kwa asilimia 15 kupitia nyongeza ya mkataba Na. 1 na kufanya thamani ya mkataba kuwa Sh. 1,480,000,000.

Uchambuzi wa nyongeza zote za mikataba unaonesha kuna ongezeko la Sh. 1,543,330,088. Licha ya ongezeko hilo la gharama za uchapishaji, hakuna dhamana ya ziada iliyotolewa kutokana na udhibiti duni wa mikataba. Kupwaya kwa udhibiti wa nyongeza ya mawanda ya kazi katika mikataba kunaiweka serikali katika hatari ya hasara ya kifedha.

Ninapendekeza TET iimarisha udhibiti wake ili kuhakikisha upatikanaji wa dhamana ya ziada ya utendaji kazi ya uchapishaji kwa mujibu wa marekebisho ya kandarasi, ikiwamo wigo mzima wa mikataba.

### 6.2.6 Mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 81.13 ilisainiwa kabla ya kuwasilishwa kwa dhamana ya utendaji

Aya ya 11.2 ya Mwongozo wa Dhamana katika Ununuzi wa Umma ya Februari 2022 inataka uwasilishaji wa dhamana ya utendaji kwa taasisi nunuzi kabla ya kusaini mkataba.



## Usimamizi wa Mikataba na Hali Halisi ya Utekelezaji wa Miradi

Katika ukaguzi wa Mradi wa HEET uliotekelezwa na Chuo Kikuu cha Dodoma na mradi wa REGROW unaotekelezwa na TANAPA, nilibaini kuwa ilitolewa mikataba ya Sh. bilioni 1.15 na Sh. bilioni 79.98 mtawalia. Mikataba hiyo ilisainiwa bila kuwasilishwa kwa dhamana ya utendaji. Maelezo zaidi yanapatikana katika Jedwali 19.

**Jedwali 19: Mikataba iliyosainiwa kabla ya kuwasilisha dhamana ya utendaji**

Na.	Jina la Mtekelezaji Mradi	Na. ya Zabuni	Kiasi cha Mkataba Sh.	Tarehe ya kusaini mkataba	Tarehe ya Uwasilishaji wa dhamana
1	TANAPA	TZ-TANAPA-316214-CW-RFB-Lot 1	15,560,000,000	16-Aug-23	18-Okt-23
2	TANAPA	TZ-TANAPA-316214-CW-RFB-Lot 2	20,070,000,000	15-Apr-23	12-Mei-23
3	TANAPA	TZ-TANAPA-303898-CW-RFB	4,210,000,000	15-Apr-23	21-Jun-22
4	TANAPA	TZ-TANAPA-303894-CW-RFB Lot 2	35,280,000,000	15-Apr-23	14-Jun-23
5	TANAPA	TZ-TANAPA-316214-CW-RFB-Lot 4	4,860,000,000	15-Apr-23	22-Mei-23
6	UDOM	PA/041/WB/HEET/P166415	438,034,880	30-Jun-23	18-Jul-23
		346124/2022/2023/G/04 LOT 1			
7	UDOM	PA/041/WB/HEET/P166415	716,269,594	30-Jun-23	12-Sep-23
		346124/2022/2023/G/04 LOT 2			
Jumla			81,134,304,474		

**Chanzo:** Majalada ya mikataba mwaka wa fedha 2022/23

Tatizo hili lilisababishwa na upungufu katika udhibiti na linatia shaka kuhusu uwazi, uwajibikaji, na uzingatiaji wa sheria za manunuzi, hivyo kusababisha usumbufu katika utekelezaji wa miradi na dhima ya kisheria.

Ninapendekeza kwamba uongozi wa UDOM na TANAPA ushughulikie suala hili kwa kuweka udhibiti imara ili kuhakikisha kuwa wazabuni wanatoa dhamana ya utendaji kazi kabla ya mikataba kusainiwa.

### 6.3 Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mikataba

#### 6.3.1 Kutokuwapo kwa miundombinu ya mtandao wa usambazaji maji kwa visima 15 vilivyokamilika vilivyogharimu Sh. bilioni 9.16

Sehemu 1 hadi 3 ya kifurushi Namba W011 cha Zabuni Namba AUWSA/AfDB/W/001/2019 iliyotekelezwa na Kampuni ya Shanxi Construction Engineering Corporation and Minerals Company ilihusisha kandarasi yenye thamani ya Sh. bilioni 9.16 kwa kazi za uchimbaji, upimaji, tathmini na kukamilisha visima 15 virefu katika eneo la Usa River - Makumira - Tengeru mkoani Arusha. Kazi hiyo ilikamilishwa tarehe 15 Mei 2023.

Licha ya kukamilika kwa Mradi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira endelevu wa Jiji la Arusha, hakukuwa na miundombinu ya usambazaji maji inayunganisha visima hivyo kwa watumiaji. Kwa hiyo, mradi bado haufanyi kazi, licha ya uwekezaji wa Sh. bilioni 9.16.

Tatizo lilijitokeza kutokana na upungufu katika awamu ya awali ya upangaji na ufinyu wa bajeti ambao ulizuia ufadhili wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji. Kutokuwapo kwa mtandao wa usambazaji maji kumesababisha matumizi duni ya visima, hivyo kuzuia kufikiwa kwa lengo lililokusudiwa la kutoa maji safi na salama kwa jamii.

**Ninapendekeza menejimenti ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha itenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mtandao wa usambazaji maji. Mgao huu ni muhimu ili kufikia malengo ya mradi wa kutoa huduma za majisafi na salama, ya uhakika, na endelevu kwa jamii.**

### 6.3.2 Upembuzi yakinifu usiotosheleza kuhusu udongo uliosababisha gharama za ziada za mradi kwa Sh. bilioni 3.41

Mnamo Julai 2020, TANROADS iliingia mkataba na Kampuni ya M/s China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) kutoka China kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya kwanza ya Barabara ya mzunguko wa nje ya Jiji la Dodoma. Mkataba huu ulihusisha sehemu ya Bandari Kavu ya Nala-Veyula-Mtumba-Ihumwa yenye urefu wa kilomita 52.3. Bei ya mkataba ya bila kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ni Sh. 100,840,778,592. Mradi huo ulipangwa kukamilika ndani ya miezi 39, ikijumuisha muda wa miezi 3 ya maandalizi ya vifaa, kuanzia tarehe 8 Septemba 2021 na kukamilika tarehe 7 Desemba 2024.

Ukaguzi wangu wa nyaraka za miradi ulibanini kuwa TANROADS ilitumia nyezo zisizofaa hususani udongo wa pamba nyeusi na ukaribu wa maji chini ya ardhi, iliyozingira urefu wa kilomita 5.5 za eneo la mradi. Pia, wakati wa kutembelea eneo la mradi, tarehe 2 Novemba 2023, nilibani uwepo wa nyenzo hizi zisizofaa ulionekana kwa urahisi bila kuhitaji vifaa maalum. Kwa kuzingatia uchunguzi huu, ninaweza kuhitimisha kwa kufaa kwamba kutokuwepo kwa taarifa hizi muhimu katika upangaji wa mradi kunachangiwa na upembuzi yakinifu usiotosheleza.

Kutokuwapo kwa taarifa muhimu katika usanifu wa mradi kumeonesha upungufu katika upembuzi yakinifu na kusababisha ongezeko la gharama ya ziada ya Sh. 3,413,010,286 ambazo hazikujumuishwa katika gharama za makadirio ya ujenzi (BOQ)

**Ninapendekeza Wakala wa Barabara Tanzania ufanye upembuzi yakinifu wa kina kwa miradi ijayo. Upembuzi yakinifu huo uhishe utafiti wa miamba, upimaji wa udongo, na tafiti za athari ya mazingira. Kisha, waweke bajeti yenye gharama halisi za mradi ili kuepuka ongezeko la gharama za mkataba na kuepuka kuchelewa kwa mradi.**



### **6.3.3 Miundombinu ya shule yenye thamani ya Sh. bilioni 1.39 ambayo haitumiki**

Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilitoa waraka wa maelekezo kwa makatibu tawala wa mikoa ukitaka shughuli za ujenzi kukamilika ndani ya miezi mitatu baada ya kupokea fedha. Waraka mmoja ni wenye nambari ya kumbukumbu DA.291/297/108'C'/20 wa tarehe 18 Januari 2022 na mwingine wenye nambari ya kumbukumbu DB.118/291/01/218 wa tarehe 07 Machi 2023.

Jumla ya shule 197 katika halmashauri 160 zilipokea Sh. 12,252,675,000 kupitia mpango wa LANES kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule ya awali kama vile vyumba vya madarasa, vyoo vya shimo, ununuzi wa kifaa cha kutambua moshi, vizima moto, usawazishaji wa ardhi, maandalizi ya bustani ya maua, mifereji ya maji, vifaa vya michezo ya watoto, na makabati ya rangi mbalimbali. Vilevile, fedha hizo zilikuwa kwa ajili ya ununuzi wa mikeka tano na ununuzi wa matenki wawili ya maji.

Ziara yangu ya mwezi Agosti 2023 ilibaini kuwa majengo yenye thamani ya Sh. 1,395,600,000 katika halmashauri 25 yalikuwa bado hayajaanza kutumika kutokana na kutokuwapo kwa samani kama vile meza na viti, mikeka, na vifaa vya kuchezea watoto. Pia, majengo hayo yalikuwa maji kwa ajili ya matumizi katika vyoo vya shimo vilivyojengwa. Hali hii inasababisha kuchelewa kunufaika na mradi kwa wakati. Kadhalika, inasababisha kutotimia kwa malengo ya mradi yaliyokusudiwa kwa wanafunzi.

**Ninapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iwasiliane na OR - TAMISEMI ili kuharakisha ununuzi wa samani na upatikanaji wa maji ili majengo yaliyokamilika yaanze kutumika bila kuchelewa zaidi.**

### **6.3.4 Ujenzi wa shule mpya 94 zenye thamani ya Sh. bilioni 39.52 katika maeneo ambayo hayajapimwa**

Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatekeleza mradi wa BOOST kwa shule za msingi. Mradi huo unalenga kuboresha upatikanaji sawa wa elimu bora katika elimu ya awali na msingi Tanzania Bara. Katibu Mkuu TAMISEMI, kupitia barua yenye nambari ya kumbukumbu DB.291/297/04/51 ya tarehe 22 Machi 2023 alielekeza halmashauri kuhakikisha maeneo mapya ya ujenzi wa shule yamepimwa. Pia, hati-miliki ziwe zimepatikana ndani ya miezi mitatu kuanzia tarehe ya barua hiyo ilipotolewa.



## Usimamizi wa Mikataba na Hali Halisi ya Utekelezaji wa Miradi

Ukaguzi wangu wa ujenzi wa shule mpya 94 za msingi zenye thamani ya Sh. 39,517,700,000 umebaini kuwa ujenzi ulifanywa katika maeneo ambayo hayajapimwa na kuwa na hati miliki.

Hii ilitokana na ufuatiliaji duni wa maafisa masuuli katika kuhakikisha upatikanaji wa hati miliki, jambo ambalo linaibua wasiwasi kuhusu umiliki na halali wa maeneo hayo. Ujenzi wa miundombinu ya shule katika maeneo ambayo hayajapimwa na kuwa hati-miliki unaziweka Halmashauri katika hatari ya kukabiliana na migogoro ya ardhi.

**Napendekeza uongozi wa halmashauri husika uongeze juhudi za kufuatilia ili kuhakikisha maeneo yote mapya ya ujenzi wa shule yanapimwa na kupatiwa hati-miliki, hatimaye kupunguza hatari za migogoro.**

### 6.3.5 Marambo ya kunyweshea ng'ombe yaliyokamilika ambayo bado hayajatumika katika Bonde la Ziwa Tanganyika - Sh. Milioni 107

Jedwali la I Sehemu ya A 3 (V) kuhusu Usimamizi Jumuishi wa Rasilimali wa Mkataba wa Fedha (Mradi wa Pili wa Kuunga Mkono Sekta ya Maji) uliosainiwa tarehe 20 Machi 2017 kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) linalenga kutekeleza miradi midogo ya kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya maji, uhibitaji wa mafuriko, na kuzuia mmomonyoko wa udongo katika ngazi ya jumuiya ya watumiaji wa maji na jamii.

Mpangokazi wa Wizara ya maji na bajeti iliyoidhinishwa ya mwaka wa fedha 2021/22 unaonesha kuwa Wizara ya Maji ilitenga Sh. 107,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa marambo mawili ya kunyweshea mifugo nje ya hifadhi ya bwawa la maji la Igombe. Ziara yangu ya tarehe 8 Agosti 2023 katika maeneo ya Igombiro na Misha katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ilibaini kuwa kazi ya ujenzi wa marambo mawili ya kunyweshea mifugo ilikamilika mwezi Septemba 2022 na sehemu hizo bado hazijaanza kutumika.

Hii ilitokana na muswada wa sheria ya maji uliopendekezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora ambayo ulizuia wafugaji wa eneo hilo kuunganisha mabirika kwenye mabwawa hayo. Malengo ya mradi yaliyokusudiwa hayakuweza kufikiwa kutokana na kutotumia marambo ya kunyweshea mifugo.

**Ninapendekeza kwamba Bodi ya Maji ya Bonde la Tanganyika ishirikiane na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Tabora ili kuhakikisha kuwa marambo ya kunyweshea mifugo yaliyojengwa yanatumika ipasavyo.**

### 6.3.6 Utendaji usioridhisha wa DLI 7 uliosababisha benki ya dunia kuidhinisha kiasi kidogo cha fedha Sh. bilioni 2.85

Utekelezaji wa mradi wa SWASH unaofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia (MoEST) unahusisha Viashiria Viwili Vinavyounganishwa na Utoaji Pesa (DLIs): DLI Na. 4 kuhusu upatikanaji wa huduma bora za usafi wa mazingira na usafi wa mazingira shuleni na DLI Na. 7 kuhusu utoaji wa taarifa usahihi na kamili. za tathmini na usimamizi kwa mamlaka za halmashauri kwa kutumia vigezo vya kuripoti vilivyobainishwa na mradi wa SWASH.. Aya ya 117 ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Mradi wa 2021 inahimiza kila Halmashauri kutoa taarifa kwa Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Elimu ya Msingi (BEMIS) ndani ya siku 15 baada ya mwisho wa kila robo. Kwa DLI namba 7, Halmashauri zinazokidhi vigezo hupokea zawadi ya dola 23,000 kwa kila halmashauri yenye sifa, jumla ya dola 1,978,000 kwa halmashauri zote 86 zinazoshiriki.

Uchambuzi wangu wa taarifa za mradi kwa mwaka 2022/23 umebaini kuwa halmashauri 31 tu zilifanikiwa kufikia lengo la DLI 7, hivyo kupokea dola za Marekani 713,000 (Sh. 1,604,250,000). Kinyume chake, halmashauri 55 hazikufanikiwa kufikia lengo la DLI 7, hivyo kusababisha kukosa tuzo kiasi cha dola za Marekani 1,265,000 (Sh. 2,846,250,000).

Nilibaini kuwa fedha zilizowekwa kwa ajili ya ufuatiliaji na usimamizi zilitengewa DLI 4 kama kipaumbele, hivyo kusababisha utoaji mdogo wa fedha za DLI 7. Hii ilitokana na ufuatiliaji duni wa utendaji wa halmashauri katika kuwasilisha takwimu kwa BEMIS. Jambo hili lilizuia tathmini ya maendeleo na hatua za kurekebisha kufanyika kwa wakati, hivyo kuzuia marekebisho ya upungufu yaliyojitokeza katika utendaji wa mradi dhidi ya viwango vinavyotarajiwa, ikionesha umuhimu wa ufuatiliaji na kufanya tathmini inayofaa ili kubaini kasoro na kuchukua hatua za kurekebisha kwa haraka.

Ninapendekeza kwamba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iandae mpango wa kusaidia halmashauri zinazokabiliwa na changamoto katika kufikia viwango vya Utoaji wa Fedha (DLIs) namba 7 vinavyokubalika, kama vile kuwezesha fedha za mradi kutolewa kabla ya kufungwa kwa dirisha la ufadhili wa mradi.

### 6.3.7 Kutokuwepo kwa uchunguzi wa udongo kabla ya kuanza usanifu wa muundo

Aya ya 15.1 ya viwango ya Uingereza vya 5930-2015 inataka pawe na uchunguzi wa maeneo ya miradi mipya kwa lengo la kutoa taarifa muhimu za kuwezesha kuchagua eneo linalofaa zaidi kwa ujenzi. Pia, uchunguzi huo utawezesha ubunifu wa vipengele vya kijiografia kwa ajili ya kazi hiyo.



## Usimamizi wa Mikataba na Hali Halisi ya Utekelezaji wa Miradi

Mapitio yangu ya usanifu wa muundo wa jengo jipya la maendeleo lenye thamani ya Sh. 1,296,730,889 katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni unaotekelezwa na Wizara ya Afya chini ya mpango wa ESPJ ulibaini kuwa usanifu wa muundo ulifanywa bila kufanya vipimo muhimu vya udongo. Hali hiyo ilisababishwa na usimamizi duni wa mradi wa ujenzi, kinyume na viwango ya usimamizi wa ubora na usalama.

Uchunguzi huu ni muhimu katika kubaini aina ya msingi unaofaa na kina kinachohitajika kuhakikisha uthabiti wa muundo wa jengo. Kwa hiyo, kutokuwapo kwa uchunguzi huu kunaleta hatari kubwa katika uthabiti wa muundo wa jengo.

Ninapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ishirikiane na wataalamu na washauri wa kijiolojia katika awamu ya kupanga mradi, ili kufanya uchunguzi wa kina wa eneo na kutoa taarifa muhimu katika kipengele cha kijiolojia. Pia, nahimiza pawe na ushirikiano wa karibu kati ya timu za usimamizi wa mradi na wataalamu wa kiufundi ili kuunganisha mapendekezo yao katika kupanga na kutekeleza mradi.

### 6.3.8 Kazi ambazo hazijakamilika katika shule 225 chini ya mradi wa BOOST

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, kupitia barua yenye nambari ya kumbukumbu DB.291/297/04/51 ya tarehe 22 Machi 2023, aliziagiza halmashauri kuhakikisha kuwa miradi ya BOOST inakamilika ifikapo tarehe 30 Juni 2023.

Katika uhakiki wa maeneo ya mradi wa BOOST kati ya Agosti na Oktoba 2023, nilibaini kuwa shule za msingi 225 katika halmashauri tofauti zilizopokea Sh. 73,917,800,000 hazikukamilisha ujenzi wa miundombinu ya madarasa, jengo la utawala, vyoo, ununuzi wa madawati, meza, na viti. Ujenzi wa miundombinu ulikuwa katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji.

Hii ilitokana na: fedha kidogo zilizotolewa ambazo hazikutosha kukamilisha kazi zilizokuwa zimepangwa; kasi ndogo katika kutekeleza miradi na kutowiana kwa maendeleo ya ujenzi kulikosababisha ucheleweshaji wa ukamilishwaji wa mradi; kuongezeka kwa gharama; na masuala ya ubora yanayoweza kutokea na hivyo kusababisha usumbufu katika utoaji wa huduma za elimu.



Napendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ishirikiane na Wizara ya Fedha ili kutekeleza taratibu madhubuti za kusimamia miradi ambayo haijakamilika, ikiwamo kutathmini miradi na rasilimali muhimu toshelevu kwa ajili ya kukamilisha miradi kwa wakati.

### 6.3.9 Kuchelewa kwa upanuzi wa mabwawa ya kuhifadhi majitaka, ya llemela kwa miezi 21

Mnamo tarehe 24 Agosti 2021, Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwanza pamoja na M/s Skyline Properties Limited, na White City International Contractors Ltd waliingia Mkataba Na. AE/042/2015/2016/W/03b kwa ajili ya upanuzi wa mabwawa ya kuhifadhi majitaka katika Wilaya ya llemela, jijini Mwanza. Mkataba huo ulitarajiwa kukamilika ndani ya siku 365 kuanzia tarehe ya kupewa taarifa ya kuanza kwa kazi za ujenzi iliyotolewa na mhandisi.

Nimebaini utekelezaji wa mradi umechelewa kwa zaidi ya miezi 21, kuanzia tarehe ya kusaini mkataba hadi tarehe 30 Juni 2023. Maendeleo ya utekelezaji wa mkataba yalikuwa 74%. Sababu za msingi za ucheleweshaji huu ni mchakato mrefu wa kupata msamaha wa kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC) kuchelewa kutoa tope kwenye bwawa la kuchakata maji machafu, pamoja na uhaba wa fedha za kigeni. Ombi la msamaha wa kodi wa kwanza liliwasilishwa mara tu baada ya kusainiwa kwa mkataba (24 Agosti 2021), lakini msamaha huo ulitolewa tarehe 26 Januari 2022. Msamaha wa kwanza uliisha Desemba 2022. Ombi la msamaha wa pili liliwasilishwa mara moja; hata hivyo, msamaha huo ulitolewa tarehe 26 Aprili 2023.

Hili limekuwa na athari ya moja kwa moja na mbaya katika utekelezaji wa mkataba. Muda wa mradi uliongezeka kwa kiasi kikubwa na kusababisha kuongezeka kwa gharama za mradi, kama vile kuongezeka kwa gharama za ufundi, gharama za uendeshaji, na hasara kutokana na kubadilisha fedha za kigeni ambazo hazikuwa zimepangiwa bajeti.

Ili kurahisisha mradi na kupunguza ucheleweshaji, menejimenti ya MWAUWASA inashauriwa kufanya yafuatayo: kuboresha mawasiliano na mamlaka ili kupata idhini ya haraka; kutathmini fedha za mradi kwa ajili ya marekebisho au ufadhili wa ziada ili kufidia gharama zinazosababishwa na ucheleweshaji; kuchunguza upya mikataba kwa ajili ya mabadiliko; na kuandaa mikakati ya kupunguza kuchelewa kwa miradi siku zijazo kutokana na ucheleweshaji wa idhini kupitia kuwasiliana na mamlaka mapema na kutafuta njia mbadala za idhini.

**6.3.10 Shughuli za miradi za gharama ya Sh. 9.78 bilioni ambazo hazijatekelezwa**

Ukaguzi wa mpangokazi na taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ulibaini kuwa watekelezaji watatu wa miradi walikuwa wameshindwa kutekeleza shughuli 25 zilizopangwa zenye jumla ya makadirio ya gharama ya Sh. 9,783,474,763.4 kama inavyoonekana katika Jedwali 20 na Kiambatisho VI.

Kutotekelezwa kwa shughuli hizi kulichangiwa na kuchelewa kwa utoaji wa fedha pamoja na usimamizi usioridhisha wa menejimenti. Kushindwa kutekeleza shughuli zilizopangwa kulingana na bajeti iliyoidhinishwa kumeathiri ukamilishwaji wa shughuli za mradi kwa wakati, hali ambayo imesababisha kutofikiwa kwa malengo ya miradi.

**Jedwali 20: Mradi Iliyopangwa ambayo haijatekelezwa**

Na.	Jina la Mradi	Jina la Mtekelezaji mradi	Idadi ya shughuli ambazo hazijatekelezwa	Gharama (Sh.)
1	Mradi wa Kusaidia Sekta ya Maji	Wizara ya Maji	14	5,084,474,501
2	Barabara ya Kimataifa: Rumonge - Gitaza (45 km) na Kabingo - Kasulu - Manyovu (260 km)	Wakala wa Barabara	8	3,710,525,000
3	Taasisi ya Susan Thomson Buffet	Wizara ya afya	3	988,475,262
<b>Jumla</b>			<b>25</b>	<b>9,783,474,763</b>

Ninapendekeza kuwa menejimenti iimarishe usimamizi wa miradi ili kuhakikisha miradi inakamilika kwa muda uliokubaliwa na kutumika ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

# SURA YA SABA

## UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA VIVUKO VIPYA VYA NYAMISATI – MAFIA, MV KILINDONI NA UKARABATI WA VIVUKO VYA MV KAZI NA NYERERE



### 7.1 Utangulizi

Ukaguzi ulihusisha usimamizi wa miundombinu ya vivuko vya TEMESA nchini Tanzania kutoka mwaka 2019/20 hadi 2022/23. Ukaguzi uliangalia ujenzi na ukarabati wa vivuko, ikiwamo miradi mipya kama vile ujenzi wa kivuko cha Nyamisati-Mafia, MV Kilindoni, na ukarabati wa MV Kazi na MV Nyerere, chini ya Mpango Mkakati wa 2016/17 hadi 2020/21.

Jukumu la TASAC katika kuhakikisha usalama wa baharini kupitia ukaguzi wa meli pia lilipitiwa. Lengo lilikuwa kutathmini ikiwa juhudi za TEMESA na TASAC katika kuhakikisha miundombinu ya vivuko na hatua za usalama zilifanikiwa kuleta thamani kwa pesa zilizotumika. Taarifa za mikataba kwa miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko iliyokaguliwa inaoneshwa katika **Jedwali 21**.

**Jedwali 21: Taarifa za mikataba kwa miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko**

Jina la Mradi	Maendeleo ya Mradi (%)	Muda wa Mradi		Gharama za makadirio ya ujenzi (Sh. Bilioni)	Fedha Zilizolipwa (Sh. Bilioni)
		Muda wa Kuanza	Muda wa Kumaliza		
Ujenzi wa kivuko kipyaa Nyamisati-Mafia	30	22/10/2022	29/07/2023	9.50 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani	2.85 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani
Ujenzi wa kivuko cha MV Kilindoni	100	15/04/2019	20/01/2020	5.31 bila kodi ya ongezeko la thamani	5.07 bila kodi ya ongezeko la thamani
Ukarabati wa kivuko cha MV Kazi	95	24/06/2022	13/09/2022	4.43 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani	3.69 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani
Ukarabari wa kivuko cha MV Nyerere	77	Not availed	31/01/2024	1.74 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani	0.76 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani

**Chanzo:** Nyaraka za Mikataba kwa miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko

## 7.2 Upangaji na usanifu

### 7.2.1 Ukosefu wa wazo la mradi na kufanya mchujo wa awali wa miradi ya vivuko

Kifungu cha 3.1.2 cha Mwongozo wa Uendeshaji wa Maandalizi ya Miradi ya Uwekezaji wa Umma wa mwaka 2015 kinahitaji taasisi zote za serikali na sekta binafsi ambazo zinaanzisha mradi wowote kuandaa "wazo la mradi" ili kuruhusu mchujo wa awali wa mradi kufanyika.

Nilibaini kuwa TEMESA haikuandaa wazo katika miradi yake ya vivuko. Hali hii ilisababisha kutofanyika kwa mchujo wa mawazo ya miradi kwa kuzingatia malengo na faida za miradi hiyo. Licha ya kuidhinishwa kwa bajeti, hakukuwa na ushahidi wa uchunguzi wa awali wa mradi uliofanywa na wizara husika.

Nilibaini kutokuwapo kwa uelewa kuhusu umuhimu wa wazo la mradi, hivyo kukosa tathmini kamili ya mradi.

Kutokuwapo kwa wazo la mradi kwa mradi wa vivuko vya TEMESA kunadhihirisha kuwapo kwa pengo kubwa katika kufuata taratibu na usimamizi wa mradi, na uwezekano wa kuathiri uwiano, mkakati na mafanikio ya mradi.

### 7.2.2 TEMESA haikufanya upembuzi yakinifu wa miradi ya ujenzi wa vivuko

Kifungu cha 4.2 (iii) cha Mwongozo wa Uendeshaji wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa mwaka 2015 kinahitaji taasisi inayofanya utekelezaji wa mradi kuandaa upembuzi yakinifu kwa miradi muhimu au yenye hatari kubwa au yenye teknolojia ya hali ya juu.

Nilibaini kuwa TEMESA haikufanya upembuzi yakinifu kwa ujenzi wa vivuko kutokana na uhaba wa wataalamu wa ndani, hasa mhandisi wa bahari na usanifu wa majini.

Ukosefu wa upembuzi yakinifu uliathiri tathmini ya mradi katika nyanja za kiufundi, kiuchumi, na kifedha, pamoja na tathmini ya soko, utafiti wa njia ambayo vivuko hivyo vinatakiwa vipite, na tathmini ya miundombinu. Yote haya ni muhimu kwa miradi ya ujenzi wa vivuko; na yangelisaidia kufanya maamuzi kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo.

Upembuzi yakinifu ni muhimu ili kutathmini mahitaji ya kivuko kwa usahihi. Ukosefu huu wa upembuzi yakinifu unaweza kuathiri faida na uendelevu wa mradi na kuwanyima washikadau taarifa kuhusu mahitaji ya kifedha, makadirio ya mapato, na gharama zinazotarajiwa kujitokeza katika utekelezaji wa mradi.

### 7.2.3 Mchakato duni wa usanifu katika miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko

Kanuni ya 21(3) na 20(2) Kanuni za Meli za Kibiashara (vivuko) ya mwaka 2004 kinataka vifaa vipya au mabadiliko makubwa kwenye vivuko yahakikishe uwapo wa ubora wa kutosha utokanao na usanifu uliofanyika. Aidha, taasisi zinazojenga vivuko lazima ziwasilishe malighafi za ujenzi na ramani ya umbo la kivuko kwa ajili ya kuidhinishwa na TASAC.

Katika mapitio yangu ya nyaraka za miradi, nilibaini tofauti kati ya usanifu na matokeo ya ujenzi na ukarabati wa vivuko, kama inavyoelezwa katika **Jedwali 22**.

#### Jedwali 22: Kasoro katika usanifu wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko

Jina la Mradi	Kasoro zilizobainishwa katika usanifu wa Miradi
Ujenzi wa kivuko cha MV Kilindoni	Usanifu haukuidhinishwa na TASAC
Ujenzi wa kivuko kipy cha Nyamisati-Mafia	TEMESA ilipuuza vipimo muhimu vya udhibiti wa ubora wakati wa ujenzi wa kivuko kipy, kama vile vipimo vya msukumo, vipimo vya mashine, na vipimo vya uchochoteaji. Pia, haikutoa mchanganuo wa usanifu wa wa kiuhandisi, mipango ya awali, na wazo la mradi. Ukosefu wa vipimo hivi unaweza kusababisha ubora duni.
Ukarabati wa kivuko cha MV Nyerere	Kulikuwa na mabadiliko ya usanifu wa kivuko katika urefu wa kivuko kwa mita 1 na mabadiliko ya umbo la kivuko, mabadiliko hayo yamefanya Nahodha wa kivuko kuwa na ukomo wa kuona sehemu ya mbele na kutoweza kuona sehemu ambazo anatakiwa kuziona ususa ni uwekaji wa nanga kama inavyooneshwa kwenye <b>Kielelezo 1</b> .  Vile vile mabadiliko ya usanifu wa kivuko yalitakiwa kuwasilishwa kwa TASAC kwa ajili ya kuidhinishwa. Lakini TASAC haikufanya uhakiki kama mabadiliko ya usanifu huo yalilikidhi viwango vya usalama, viwango na kanuni.
Ukarabati wa kivuko cha MV Kazi	Kukosekana kwa michoro kwa kazi za ukarabati na mchanganuo wa vipimo vilivyohusisha ukaguzi na majaribio.

**Chanzo:** Uchambuzi wa Nyaraka kwa miradi iliyokaguliwa.

**Kielelezo 1: Uoni duni upande wa mbele wa kivuko cha MV Nyerere**

Kasoro zilizobainika katika usanifu wa ujenzi wa vivuko na ukarabati zilitokana na TEMESA kukosa wataalamu wa uhandisi wa vyombo vya bahari na kukosekana kwa tathimini ya hali ya vivuko kabla ya utekelezaji wa miradi. Hii ilisababisha kazi zenye ubora duni, kutokuwapo kwa mchanganuo wa kina wa gharama za makadirio ya ujenzi, na usanifu ambao haikuidhinishwa na TASAC, hali inayoleta wasiwasi juu ya usalama na kufuata kanuni.

TEMESA inapaswa kuajiri wahandisi wa vyombo vya baharini wenye sifa kwa ajili ya usimamizi wa miradi na kufanya uchunguzi wa kina kabla ya kufanya ukarabati wa vivuko, na kuhakikisha usanifu wake unakidhi viwango vya TASAC kwa kufuata kanuni za usalama. Aidha, wafanye mafunzo ya usimamizi wa miradi, ikiwamo wazo la mradi na upembuzi yakinifu, pamoja na kuwekeza katika mafunzo maalumu ya uhandisi wa bahari na usanifu wa majini ili kuziba pengo la utaalumu na kuboresha viwango vya ubora.

### 7.3 Usimamizi wa ununuzi

#### 7.3.1 Kutokubainishwa kwa masuala ya kujadiliana wakati wa kupatana na Mkandarasi

Kanuni ya 226(6) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kinahitaji timu ya majadiliano kuandaa mpango wa majadiliano utakaobainisha masuala ya kujadili kama ilivyoelezwa katika ripoti ya tathmini ya wazabuni na malengo yanayotakiwa kufanikishwa na, pale inapowezekana, kufafanua malengo na kuweka vigezo vya juu na vya chini vya masuala ya majadiliano.

Nilibaini kwamba timu ya majadiliano iliandaa mipango ya majadiliano bila kubainisha masuala ya kujadiliwa katika majadiliano kwa ajili ya ukarabati wa MV Nyerere, ujenzi wa kivuko kipya kinachofanya safari kati ya Nyamisati na Mafia, na ukarabati wa MV Kazi.

Hii ilitokana na tathmini ya zabuni na majadiliano na mzabuni aliye kidhi vingezo kufanyika pasipo mhandisi mzoefu wa masuala ya vyombo vya majini. Pia gharama za makadirio ya ujenzi zilikuwa zimewekwa kwa ujumla bila mchanganuo, na kusababisha timu ya majadiliano kutoweza kufanya majadiliano ya mchanganuo wa gharama za makadirio ya ujenzi na hii iliadhiri majadiliano ya gharama za makadirio ya ujenzi kama ilivyo ainishwa kwenye **Jedwali 23**.

**Jedwali 23: Athari zilizosababishwa na kukosekana kwa vigezo vya majadiliano**

Jina la Mradi	Athari zilizojitokeza
Ukarabati wa MV Nyerere	65% (sawa na Sh. 1,136,100,000) ya kazi za mkataba wote hazikujadiliwa kutokana na kutobainishwa kwa masuala ya kujadiliana katika mradi huo
Ukarabati wa MV Kazi	Mkandarasi alitoa punguzo la jumla ya asilimia tatu ya gharama za makadirio ya ujenzi (sawa na Sh. 88,624,200). Hata hivyo, haikuwa wazi ni katika kazi gani bei zilipunguzwa na kusababisha mkandarasi kushindwa kupunguza gharama hizo katika hati mbili zilizolipwa zenye jumla ya Sh. 1,962,551,892.

**Chanzo:** Mipango ya majadiliano kwa ajili ya ukarabati vivuko na uchambuzi wa hati za malipo ya wakandarasi

Kutobainisha masuala ya kujadiliana kwenye mpango wa majadiliano kulifanya TEMESA kukubali gharama za makadirio ya ujenzizilizopendekezwa na wakandarasi bila marekebisho wala majadiliano.

Ninapendekeza kuwa TEMESA iboreshe ujuzi wa timu za tathmini na majadiliano kwa kuwa na ujuzi wa uhandisi wa baharini na ununuzi, na iwe na maandalizi ya mipango ya majadiliano inayobainisha wazi mipaka ya majadiliano na malengo yanayopimika.

## 7.4 Usimamizi wa mikataba

### 7.4.1 Kupanda kwa joto katika injini ya MV Kilindoni inapokuwa katika mwendo wa 1800 rpm

Kifungu cha 9(i) cha Masharti Maalumu ya Mkataba Na. AE/006/2018-2019/HQ/G/CN-36 wa ujenzi wa MV Kilindoni kinahitaji TEMESA kufanya ukaguzi wa ubora na idadi ya bidhaa kabla ya kusafirisha kwa gharama ya muuzaji/wakandarasi; na kuhakikisha bidhaa imefuata maelezo ya kiufundi. Aidha, kanuni za ununuzi wa vyombo vya baharini zinataka wanunuzi kutuma wataalamu kufanya vipimo vya injini mpya kiwandani na kuthibitisha utendaji kazi wake kabla ya kutumika katika vyombo hivyo vya baharini.

Nilibaini kwamba wataalamu wa TEMESA hawakushiriki katika uhakiki na majaribio ya injini ikiwa kiwandani huko Korea, hivyo kushindwa kuthibitisha ubora wa injini na vifaa vyake dhidi ya vigezo vya usanifu na utendajikazi uliokusudiwa katika injini hiyo kabla ya kusafirishwa kuja Dar es Salaam. Nyaraka za mkataba zilionesha kuwa kutofanyika kwa uhakiki wa majaribio wa injini kiwandani huko Korea kulitokana na pendekezo la TEMESA kufanya majaribio katika kiwanda cha boti cha mkandarasi kilichopo Kigamboni, Dar es Salaam.

Mradi umetekelezwa kwa 100% na jumla ya Sh. bilioni 5.07 kati ya Sh. bilioni 5.31 zimelipwa kwa mkandarasi, lakini hakuna hati inayoonesha kukamilika kwa mradi, wala TEMESA haijatoa maagizo yoyote kwa mkandarasi kuifanyia marekebisho injini hiyo.

Hata hivyo, katika mapitio yangu ya ripoti kutoka TEMESA nilibaini kwamba majaribio ya kivuko yaliyofanywa na TEMESA baharini mnamo tarehe 7 Aprili 2023 yalionesha matatizo makubwa ya injini mpya kuchemka sana inapokuwa katika mwendo wa mizunguko 1800 kwa dakika (rpm), licha ya jitihada za kusahihisha hili kupitia kubadilisha propela na kuboresha mfumo wa baridi katika injini hiyo.

Nilibaini kwamba injini haikukidhi mahitaji ya utendaji ulioelekezwa wa mapigo ya noti 9.5 katika mwendo wa mizunguko 1800 kwa dakika (rpm), ikionesha kuwa matatizo haya yangeweza kugunduliwa mapema ikiwa TEMESA ingehudhuria katika uhakiki na majaribio huko Korea.



#### **7.4.2 Uvujaji wa mafuta kwenye Injini ya MV Kazi kutokana na injini kutokufanya kazi kwa ufanisi**

Kifungu cha 301.1 cha mkataba wenye nambari ya kumbukumbu AE/006/2021-2022/HQ/W/CN-25 wa mwaka 2022 kinachohusiana na viwango vya ubora wa kiufundi, michoro, na picha kinahitaji mitambo yote iliyopo baharini na mifumo ya usukumaji kubadilishwa na mitambo ya injini za dizeli yenye uniti ileile au inayofanana kama inavyohitajika.

Nilibaini kuwa MV Kazi ilikuwa na injini nne zilizowekwa wakati kivuko hicho kilipojengwa mnamo mwaka 2017; na injini hizi nne zilibadilishwa na TEMESA mwaka 2022. Hata hivyo, ripoti za ukaguzi wa TASAC za tarehe 29 Desemba 2022 zilibainisha uvujaji katika injini namba 4 na injini namba 3 ambazo hazikushughulikiwa.

Pia, ukaguzi wangu katika mradi wa ukarabati wa MV Kazi niliufanya tarehe 31 Oktoba 2023 ulibaini matatizo yafuatayo kwenye injini zilizobadilishwa: Injini Na. 4 ilikuwa na uvujaji kutokana na hitilafu katika pampu-jeti Na. 1 na Na. 2 ya boksi la gia, wakati injini Na. 3 ilikuwa haifanyi kazi kutokana na hitilafu ya pampu ya mafuta.

Nilibaini kwamba waendeshaji wa mashine hawakufuata ratiba sahihi ya matengenezo ya injini. Hii ilichangiwa na kukosekana kwa miongozo ya uendeshaji wa injini kutoka kwa mtengenezaji. Upungufu huu umesababisha matengenezo yasiyofaa, yaliyoongoza kwa hitilafu za mara kwa mara za injini. Nina wasiwasi kama ubora wa injini unatosha kudumisha operesheni endelevu ya kivuko kama inavyohitajika.

#### **7.4.3 Kuchelewa kukamilika kwa Ukarabati wa MV Nyerere**

Nilibaini kwamba hadi Novemba 2023, muda wa utekelezaji wa mradi ulikuwa umeongezwa kwa miezi 16 zaidi ya muda wake uliopangwa kukamilika kwa miezi sita. Katika mapitio yangu ya mawasiliano kati ya TEMESA na Kampuni ya Songoro Marine Limited, nilibaini kwamba kulikuwa na maombi manne ya kuongeza muda wa kazi kama ilivyoelezwa katika **Jedwali 24**.

**Jedwali 24: Maombi ya kuongeza muda wa ukarabati wa MV Nyerere**

Nambari ya Kumbukumbu ya barua	Muda uliopangwa kukamilisha mradi	Ongezeko la Muda (Miezi)
Kumb.Na.TMS/ADM.3/PRJ/2022/20/06	31 Machi 2023	6
Kumb.Na.STM/TMS/EOT/2023/03/17	30 Mai 2023	2
Kumb.Na.SMT/TMS/EOT/2023/05/74	30 Septemba 2023	4
Kumb.Na.SMT/TMS/EOT/2023/09/14	31 Januari 2024	4

**Chanzo:** Barua za ombi la kuongezewa muda kutoka kwa mkandarasi.

Kucheleweshwa kwa mradi kulitokana na kupungua kwa uzalishaji wa chuma katika soko kutokana na UVIKO-19 mwishoni mwa 2019. Hii iliathiri upatikanaji wa chuma cha daraja A ambacho hutumika katika kutengeneza vyombo vya baharini; taratibu za usafirishaji; na kucheleweshwa kwa malipo kwa mkandarasi.

Kucheleweshwa kwa miradi si tu kunachelewesha manufaa ya miradi kwa wananchi kutumia kivuko hicho, bali pia huongeza gharama za makadirio ya ujenzi, ikiwamo gharama za usimamizi na uwezekano wa kuzidi bajeti na kudhuru afya ya kifedha ya mradi na kuikoshesha TEMESA mapato.

#### **7.4.4 Kuchelewa kwa ujenzi wa kivuko cha Nyamisati kwenda Mafia**

Katika mapitio yangu ya nyaraka, nilibaini nyongeza ya muda wa miezi minane ya muda wa kukamilisha kazi bila ongezeko la gharama kwa mkandarasi kupitia barua yenye nambari ya kumbukumbu BA.90/188/03/03 ya tarehe 28 Juni 2023 kutoka TEMESA. Muda wa mkataba wa ujenzi wa kivuko kipya cha Nyamisati-Mafia ulikuwa kuanzia tarehe 22 Oktoba 2022 hadi tarehe 29 Agosti 2023, lakini mkandarasi hakutimiza muda huo wa mkataba uliosababisha ombi la kuongezewa muda.

Hadi wakati wa ukaguzi huu, tarehe (30 Novemba 2023), maendeleo ya kazi yalikuwa 30%, na kiasi cha Sh. 2.85 milioni kati ya kiasi cha mkataba cha Sh. 9.50 milioni, sawa na 30% ya fedha zote za mkataba, kilikuwa tayari kimelipwa kwa mkandarasi. Mradi ulichelewa kufikia muda wa kimkataba kutokana na sababu kama vile kuchelewa kwa idhini ya michoro kutoka TASAC, kuchelewa kwa maandalizi ya chuma inayotumika ujenzi wa kivuko, na mabadiliko ya mpango mkuu wa mradi. Kuchelewa kukamilika kwa mradi kulifanya wananchi kukosa fursa ya huduma ya usafiri kupitia kivuko.

Ili kuongeza ufanisi na ubora wa miradi, TEMESA inapaswa kuandaa makadirio ya kila kazi kwenye mkataba; kuthibitisha uhalisi wa bei kwa kurekebisha kasoro za bei ya kazi; kuzingatia vipimo muhimu katika maelezo, kufanya uhakiki wa majaribio na tathmini za bidhaa; kupitia usanifu wa kivuko kabla ya utekelezaji; na kuimarisha mafunzo kwa waendeshaji wa vivuko na makapteni. Aidha, TEMESA ihakikishe inazingatia muda wa utekelezaji mkataba kwa wakati.

# SURA YA NANE

## UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA UWANJA WA NDEGE WA KIMATAIFA WA MSALATO



### 8.1 Utangulizi

Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato ni sehemu muhimu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Tanzania. Unalenga kuimarisha miundombinu ya Uwanja wa Ndege wa Dodoma ili kuchochea ukuaji wa kiuchumi. Mradi huu unafadhiliwa na mkopo wa dola za Marekani milioni 271.63 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na fedha kutoka serikalini dola za Marekani milioni 57.84. Mradi huo unatekelezwa na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS). Mradi umeanza mwaka 2022 na unatakiwa kukamilika mwaka 2026. Mradi huu una hatua mbili ambazo ni pamoja na miundombinu kama vile njia za kuruka na kutua ndege, pamoja na majengo ya abiria na mnara wa kuongoza ndege.

Ukaguzi ulilenga kutathimini ufanisi wa TANROADS katika kusimamia mawanda ya kazi ya ujenzi wa uwanja huo. Mambo yaliyoangaliwa ni muda, gharama, na ubora wa mradi huo. Ukaguzi ulijikita katika mwaka wa fedha wa 2019/20 hadi 2023/23. Ukaguzi ulifanya tathimini ya kuanzishwa kwa mradi, mipango, na utekelezaji, ikiwa ni pamoja na upembuzi yakinifu, usanifu, manunuzi na usimamizi wa mikataba.

### 8.2 Hatua ya mipango na usanifu

#### 8.2.1 Ujenzi wa majengo bila hatimiliki na vibali vya ujenzi

Kanuni ya 4 (1) ya Kanuni za Ujenzi wa Mipango Miji ya mwaka 2018 inahitaji ujenzi wowote kupata kibali cha ujenzi kinachotolewa na mamlaka ya mipango miji kulingana na michoro ya ujenzi iliyoidhinishwa na mamlaka ya mji husika.

Nilibaini kuwa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato unaotekelezwa na TANROADS ulifanyika bila kuwa na kibali cha ujenzi kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma. Mradi huo pia ulikosa hatimiliki inayoonesha uhalali wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) kumiliki ardhi hiyo. Licha ya madaai ya fidia kwa wamiliki wa awali wa ardhi hiyo kulipwa, bado hatimiliki ya kiwanja hicho haikupatikana kutoka Wizara ya Ardhi, hivyo



## Ukaguzi Wa Kiufundi Wa Ujenzi Wa Uwanja Wa Ndege Wa Kimataifa Wa Msalato

kusababisha kukosekana kwa nyaraka za umiliki wa ardhi pamoja na kibali cha ujenzi kinachohitajika. Ukosefu huu wa nyaraka rasmi za umiliki na idhini ya ujenzi wa kiwanja hicho unaweza kusababisha hatari ya migogoro ya ardhi siku za usoni. Pia, unahatarisha uhakikisho wa ubora kwa mahitaji ya mipango ya ardhi, kwani usimamizi kutoka kwa mamlaka ya usimamizi wa ardhi unakosekana.

**Ninapendekeza kwamba TANROADS, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), ihakikishe inapata hatimiliki na kibali cha ujenzi wa mradi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato ili kuepuka migogoro ya ardhi siku za usoni. Pia, ihakikishe inazingatia viwango vya kisheria na pamoja na ubora.**

### 8.2.2 Kukosekana kwa upembuzi yakinifu wa kina hadi kusababisha ongezeko la gharama Sh. Bilioni 3.04

Sehemu ya 3.3 ya Mwongozo wa Usanifu wa Kijiometri wa Barabara wa Wizara ya Ujenzi wa mwaka 2011 unasisitiza umuhimu wa kuzingatia maswala ya athari za mandhari ya ardhi katika eneo la mradi na kiwango cha mteremko kwenye usanifu wa barabara, gharama za ujenzi, na uchaguzi wa njia ya kupitisha barabara wakati wa kufanya upembuzi yakinifu na matengenezo.

Nilibaini kwamba vipimo vya mwinuko wa usawa wa ardhi kwa mujibu wa usanifu vilitofautiana na hali halisi ya mwinuko wa ardhi katika maeneo mbalimbali kutokana na njia iliyotumika katika kufanya upembuzi yakinifu. Tofauti katika vipimo hivi ilitokana na mbinu iliyotumika wakati wa upembuzi yakinifu, ambapo ndege zisizo na rubani zilitumika kupima mwinuko wa usawa wa ardhi bila kusafisha eneo la mradi, hivyo kutafsiri kimakosa kuwa usawa wa vichaka kama vile ndio usawa wa ardhi.

Utekelezaji wa mradi huo uliathiriwa na tofauti kati ya viwango halisi vya ardhi na viwango vya muundo, na kusababisha kuongezwa kwa idadi kubwa ya kazi za ardhini. IPC Na. 8 ilibaini tofauti nyingi chini ya kipengele cha udongo, hasa katika ujazaji wa nyenzo zilizochimbwa zaidi ya Miamba, na kusababisha kuongezeka kwa gharama ya TZS 3,037,248,684.91 hadi 30 Septemba 2023..

Utekelezaji wa mradi huo uliathiriwa na tofauti kati ya viwango halisi vya ardhi na viwango vya usanifu, na kusababisha kuongezwa kwa kazi za kukata tabaka la ardhi. Cheti cha malipo ya gharama za kazi Na namba nane iliyoonesha kwamba ardhi ilihitaji kujazwa kifusi kwa zaidi ya mita za ujazo 278,728, sawa na 715% katika kipengele cha kazi za vifusi. Hii ilisababisha gharama kuongezeka kwa Sh 996,948,879 hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2023. Tofauti



zilizorekodiwa zilizidi 166%, 325%, 325%, 325% na 615% kwa njia za kukimbilia ndege, sehemu za kushushia abiria, njia za kupitia ndege kwa mwendo dogo, barabara za magari na maegesho ya magari mtawalia.

**Ninapendekeza TANROADS watumie njia sahihi za kufanya tathmini ya viwango vya utofauti na usawa wa kimo cha ardhi kutoka sehemu moja hadi nyingine ili kuzuia mabadiliko katika usanifu na kudhibiti gharama zinazoongezeka.**

### 8.3 Usimamizi wa ununuzi

#### 8.3.1 Taarifa zisizokamilika katika nyaraka za ombi la pendekezo

Aya ya E3.2.4 ya Mwongozo wa Uendeshaji wa AfDB wa mwaka 2018 inataka maandalizi ya Maombi ya Pendekezo (RFP) kufanyika kabla ya kutolewa kwa idhini ya mradi ya kuingia mkataba wa awali na kutenga fedha baada ya matumizi ili kuwezesha shughuli zilizoanzishwa kabla ya kupatikana kwa ufadhili, wazabuni kuwasilisha zabuni zao na kuimarisha ushindani.

TANROADS iliidhinisha Maombi ya Pendekezo la mradi (RFPs) ambayo hayakukamilika, yakikosa maelezo muhimu kama vile mawanda ya kazi, michoro ya mradi, na vipengele vya ongezeko la thamani na viwango vya ubora vya mradi. Hii ilisababisha zaidi ya maombi 50 ya ufafanuzi kutoka kwa wazabuni, ambapo nusu yake hayakujibiwa. Wazabuni 47 waliwasilisha mashaka yao yaliyohitaji ufafanuzi karibu na tarehe 21 Mei 2020 ambayo ilikuwa ndio siku ya mwisho ya kuwasilisha zabuni zilizojazwa kikamilifu. Upungufu huo ulitokana na kutumia nyaraka za zabuni za zamani pasipo mapitio ya uboreshaji.

Kwa sababu ya upungufu katika pendekezo la mradi (RFPs), ni zabuni nane tu kati ya zabuni 47 zilizowasilishwa ndizo zilifuzu; na zabuni tano tu zilifikia hatua ya mwisho ya tathmini. Ukosefu wa uwazi katika nyaraka za zabuni ulisababisha kupwaya kwa ushindani na uwazi katika mchakato wa zabuni.

**Ninapendekeza TANROADS ifanye mapitio ya kina kwenye nyaraka za Maombi ya Pendekezo la mradi (RFPs) ili kuhakikisha kuwa yanajumuisha taarifa zote zinazohitajika ili kuongeza ushindani miongoni mwa wazabuni.**

#### 8.3.2 Mshauri elekezi kutekeleza majukumu ya ushauri wakati amefungiwa

Kanuni ya 102 ya Kanuni za Manunuzi za Umma za mwaka 2013 inatoa utatuzi unaosababishwa na vitendo vya ulaghai vilivyothibitishwa ambavyo vinaweza kuathiri kandarasi zilizoingwa kati ya mzabuni na shirika lolote la umma kabla ya kuondolewa.



Nilibaini kuwa M/s Beza Consulting Engineers PLC, mbia na kiongozi wa ushirikiano (association) wa kampuni za ushauri elekezi, aliyesaini Mkataba Namba TRD/HQ/1025/2021/22 na TANROADS tarehe 10 Novemba 2021 kwa ajili ya kutoa huduma za ushauri elekezi alikuwa amefungwa na AfDB kuanzia tarehe 21 Agosti 2023 hadi 20 Novemba 2024 kutokana na vitendo vya udanganyifu. Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ilionesha kwamba wakati wa kipindi alichokuwa amefungwa, M/s Beza Consulting Engineers PLC na washirika wake hawakustahili kushiriki katika shughuli zilizofadhiliwa na AfDB. Pia, nilibaini kuwa wafadhili wengine wanne waliifungia M/s Beza Consulting Engineers PLC, kama ilivyooneshwa katika Jedwali 25.

**Jedwali 25: Maelezo ya kufungwa kwa M/s Beza Engineering Consulting PLC**

Mamlaka iliyotoa Adhabu ya Kufungwa	Hali ya Kufungwa	Tarehe ya kuanza Kufungwa	Tarehe ya mwisho Kufungwa	Sababu ya kufungwa
AfDB (moja kwa moja imesababisha kufungwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika)	Kufungwa ikiwa ni Pamoja na masharti ya kutimiza kabla ya kuachiliwa	2023	2024	Udanganyifu
Benki ya Dunia	Imesababishwa na kufungwa na AfDB	2023	2024	Haikuwekwa wazi
Kikundi cha Benki ya Maendeleo ya Afrika	Imefungwa	21 Agosti 2023	20 Novemba 2024	Kufungwa na AfDB
Benki ya Maendeleo ya Asia	Imefungwa	5 Septemba 2023	20 Novemba 2024	Imesababishwa na kufungwa na AfDB

**Sources:** <https://www.afdb.org/en/projects-operations/debarment-and-sanctions-procedures>  
ambayo ilitembelewa tarehe on 10 Februari 2024

M/s Beza Engineering Consulting PLC iliendelea kusimamia ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato licha ya kufungwa. Maafisa wa TANROADS walidai kwamba hawakuarifiwa rasmi kuhusu kufungwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), jambo ambalo lilizuia uwezo wao wa kusitisha mkataba. Pia nilibaini kuwa ombi la Kutokuwa na Kipingamizi liliombwa na kukubaliwa na AfDB kabla ya kuingia mkataba na BEZA.

Kushindwa kusitisha mkataba, licha ya matukio ya udanganyifu yaliyobainika, kunatia shaka kuhusu uwazi na uwajibikaji, huku ikileta hatari ya kuharibu uhusiano na mfadhili.

Ninapendekeza kwamba TANROADS ihakikishe mara moja hali ya kufungwa kwa M/s Beza Consulting Engineers PLC na AfDB na wafadhili wengine. Iwapo itathibitika, TANROADS lazima itii masharti ya vikwazo kwa kusimamisha miradi yoyote inayoendelea chini kampuni na kutafuta washauri elekezi mbadala ili kudumisha uwazi, uwajibikaji na hadhi nzuri na mfadhili.

#### **8.4 Usimamizi wa mikataba**



#### **8.4.1 Kutokuwapo kwa vipimo vya kuthibitisha ubora wa kazi kwenye eneo la ujenzi**

Aya ya 1.5.1.7 ya Maelezo ya Kiufundi kwa Kazi za Miundombinu kinamtaka mkandarasi kuweka maabara iliyoithinishwa na mshauri elekezi kwa ajili ya vipimo vya udhibiti wa ubora kwenye eneo la ujenzi, huku mshauri elekezi akiwajibika kusimamia vipimo hivi, kufanya majaribio ya vipimo vya uhakiki huru kwenye maabara yake, na kutoa ushauri kuhusu mbinu za ujenzi.

Nilibaini kuwa hakukuwa na kipengele maalumu cha malipo kwa mkandarasi kwa ajili ya kufanya vipimo vyote muhimu vya ubora wa kazi ambavyo wakandarasi walihitajika kuwasilisha matokeo yake kwa mshauri elekezi kwa ajili ya uhakiki. Gharama za vipimo hivyo vya ubora zilijumuishwa katika makadirio ya gharama za mradi kipindi cha zabuni ya mkandarasi kama inavyohitajika katika Kifungu 1205 cha Maelezo ya Viwango vya Ubora wa Kazi za Barabara ya mwaka 2000.

Hata hivyo, vipimo vyote vya mikataba ya kazi vilifanywa katika Maabara ya Mhandisi na Mshauri na Mkandarasi. Nilibaini kuwa maabara ya mkandarasi ilikuwa na vifaa na wafanyakazi wachache. Kutokana na utekelezaji wa mradi huo kwa wakati mmoja, timu ya washauri ilipata majaribio ya kujitegemea kwa kila mkataba kuwa hayafai, huku Mhandisi wa vifaa vya ujenzi mmoja tu akisimamia zote mbili, na hivyo kusababisha majaribio ya vipimo ya pamoja.

Hali hii ilihatarisha uhuru unaohitajika kwa udhibiti wa ubora, na kuruhusu wakandarasi kutegemea rasilimali za Mhandisi, na hivyo kusababisha uchakavu wa vifaa na gharama kwa mwajiri.

**Ninapendekeza kwamba maabara za washauri elekezi na wakandarasi wa TANROADS za mikataba fungu la 1 na 2 ziwe na vifaa kamili na vyenye wafanyakazi wa kutosha ili kuwezesha kufanyika kwa majaribio muhimu ya kupima ubora wa malighafi za ujenzi na kazi za ujenzi kwa kujitegemea na kumuwezesha mshauri kufanya majaribio ya uthibitisho na uhakikisho kwa ufanisi.**

#### **8.5 Usimamizi wa fedha**

##### **8.5.1 Malipo ya Sh 5,728,520,301 kwa kazi ambazo bado hazijaidhinishwa na mkandarasi**

Kanuni ya 110(5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 (kama ilivyofanyiwa marekebisho na Kanuni ya 36 ya GN 333 ya mwaka 2016) inahitaji idhini ya maandishi kutoka kwa bodi ya zabuni kabla ya ongezeko la gharama linalohusiana na mabadiliko baada ya kuanza kwa mkataba. Aidha, Kifungu cha



17 cha Maelezo ya Jumla ya Masharti ya Mkataba (GCC) kinafafanua kwamba marekebisho yanayoongeza gharama za mkataba zilizokubaliwa yanahitaji idhini kutoka kwa mwajiri.

Mapitio ya cheti cha malipo ya kazi za ujenzi namba tisa kwa mkataba wa kwanza kwa ajili ya kazi za miundombinu, ambayo ilihusisha malipo ya hati zilizopita (hati namba moja mpaka hati namba nane), yalionesha malipo ya Sh. 5,728,520,301.09 kutokana na mabadiliko ya kazi katika vipengele vya makadirio ya gharama za ujenzi wa mradi bila kupata idhini kutoka kwa bodi ya zabuni. Mabadiliko haya yalitokana na usanifu duni na makosa ya vipimo vya usawa wa ardhi wakati wa upembuzi yakinifu wa topografia.

Kwa kuongezea, nilibaini kuwa mwajiri na mshauri elekezi walishindwa kufuata masharti ya mkataba katika kuhakikisha wanapata idhini ya bodi ya zabuni kwa ajili ya mabadiliko yaliyoongeza gharama za mradi. Hali hii inatia shaka kuhusu gharama ya mwisho za mradi kuzidi kiasi cha mkataba. Pia, ilisababisha upungufu wa bajeti bila kuwa na chanzo cha fedha kilichothibitishwa kwa ajili ya kukamilisha mradi.

Ninapendekeza TANROADS iimarisha taratibu za mawasiliano na kufuata taratibu za kuidhinisha ongezeko la kazi. Pia, ihakikishe uidhinishaji wa ongezeko la kazi na mabadiliko ya usanifu unakamilika kabla ya kufanyika.

### 8.5.2 Kucheleweshwa kwa Malipo ya mkandarasi wa kazi za miundombinu hadi kusababisha malipo ya riba ya - Sh. 303,814,088

Aya ya 14.7.1 (b) na 14.8 ya Maelezo ya Jumla ya Masharti ya Mkataba (GCC) inamtaka mwajiri kulipa kiasi kilichothibitishwa katika kila hati ya malipo ndani ya siku 56 baada ya mshauri elekezi kupokea taarifa na nyaraka za kuthibitisha<sup>1</sup>. Kushindwa kufanya hivyo kunasababisha mkandarasi alipwe riba kutokana na malipo yaliyochelewa.

Nilibaini kuwa malipo ya mradi yalicheleweshwa kwa muda kati ya siku nane hadi 70, na kusababisha riba ya Sh. 303.81 milioni. Serikali ya Tanzania ikitakiwa kulipa riba hizi kulingana na makubaliano yake na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Mfumo wa malipo wa *D-Fund* unaonesha kwamba TANROADS ina siku tano za kufanya uhakiki wa hati za malipo, ikifuatiwa na siku saba kwa Wizara ya Ujenzi,

---

<sup>1</sup> Hesabu huanza tarehe ambayo Mkandarasi anawasilisha hati ya malipo iliyokubaliwa au kuidhinishwa na Mshauri. Kisha mshauri ana siku 28 kuthibitisha IPC, wakati mwajiri ana siku 28 kuidhinisha na kufanya malipo, jumla ya siku 56.



## Ukaguzi Wa Kiufundi Wa Ujenzi Wa Uwanja Wa Ndege Wa Kimataifa Wa Msalato

na siku kumi na mbili kwa Wizara ya Fedha kabla ya kuwasilishwa hati hiyo kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), ambayo ina siku 14 za kazi kufanya ukamilifu wa malipo. Mfululizo huu unasababisha jumla ya karibu siku 24 katika hatua za kuidhinisha malipo, AfDB ikiachiwa siku nne tu za kufanya malipo. Tathmini ya ufuatiliaji wa malipo ya mkataba namba 1 ilionesha kwamba, mara nyingi, Benki ya Mandeleo ya Afrika (AfDB) ilizidisha siku nne zaidi ya siku 14 za kazi; hivyo kuchangia kuchelewesha malipo kwa mkandarasi.

Wakati huo, Mkataba wa Ufadhili kati ya Serikali ya Tanzania na AfDB unabainisha kuwa ingawa serikali inawajibika kwa riba inayotokanayo na malipo yaliyochelewesha, AfDB haitolewi jukumu hili, jambo linaloonesha tofauti isiyo ya haki.

Ninapendekeza TANROADS ishirikiane na Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Fedha ili kuweka mchakato wa kuidhinisha katika mpangilio mzuri. Lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha malipo kwa wakandarasi na mshauri elekezi yanafanyika kwa wakati uliopangwa. Hatua hii itapunguza kuchelewesha kwa malipo, kuzuia gharama zaidi kama za riba na fidia kwa mkandarasi kutokana, na mradi kuchelewa kukamilika.

### 8.5.3 Kutumia wahandisi wasiosajiliwa katika utekelezaji wa mradi

Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Usajili wa Wahandisi ya mwaka 2007 kinahitaji wahandisi waliosajiliwa tu kufanya kazi za uhandisi za kitaalamu u; na, kwamba, wafanyakazi wote wanaofanya kazi kama wahandisi wataalamu u wajandikishe kwenye Bodi ya Usajili wa Wahandisi.

Katika mapitio ya wafanyakazi wanaofanya kazi, nilibaini kwamba kuna wafanyakazi wanatekeleza kazi za uhandisi bila kusajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi kama ilivyooneshwa katika **Jedwali 26**.

**Jedwali 26: Wafanyakazi muhimu wasiosajiliwa**

Mkataba	Jukumu katika Eneo la Kazi	
Mkataba Na 1: Kazi za Ujenzi wa Miundombinu	1. Mkadiraji Majenzi	7. Kaimu Mwakilishi wa Nchi
	2. Mpimaji Ardhi	8. Mtaalamu wa Matabaka ya Barabara
	3. Msimamizi wa Mahali pa Kazi	9. Mkaguzi wa Eneo la Kazi
	4. Mtaalamu wa Mwanga katika Ardhi ya Uwanja wa Ndege (AGL)	10. Mhandisi wa Umeme
	5. Mtaalamu wa Vifaa vya Uongozi wa Ndege (NAVAIDS)	11. Mhandisi wa Malighafi za Ujenzi
	6. Mkaguzi wa Eneo la Kazi	12. Meneja wa Eneo la Mradi
Mkataba Na. 2: Kazi za	1. Mhandisi wa Mradi	9. Mhandisi wa Mradi
	2. Mhandisi wa Mradi	10. Mhandisi wa Mradi
	3. Mhandisi wa Miundo - Kazi za Zege	11. Mhandisi wa Miundo - Kazi za Zege



## Ukaguzi Wa Kiufundi Wa Ujenzi Wa Uwanja Wa Ndege Wa Kimataifa Wa Msalato

Mkataba	Jukumu katika Eneo la Kazi	
Ujenzi wa Majengo	4. Mhandisi wa Mifumo Maalumu ya Uwanja wa Ndege, Mfumo wa Kamera za Video & Mawasiliano	12. Mhandisi wa Mifumo Maalumu ya Uwanja wa Ndege, mfumo wa Kamera za Video & Mawasiliano
	5. Mhandisi wa Mtandao	13. Mhandisi wa Mtandao
	6. Mtaalamu wa Vifaa vya Uongozi wa Ndege (NAVAIDS)	14. Mtaalamu wa Vifaa vya Uongozi wa Ndege (NAVAIDS)
	7. Mhandisi wa Udhibiti wa Ubora	15. Mhandisi wa Udhibiti wa Ubora
	8. Meneja wa Modeli ya Taarifa za Jengo	16. Meneja wa Modeli ya Taarifa za Jengo
Huduma za Ushauri	1. Mhandisi wa Uwanja wa Ndege	

**Chanzo:** *Mapitio ya Ukaguzii wa Vyeti vya Usajili (2023)*

TANROADS haikumsimamia kikamilifu mshauri elekezi kwa sababu hawakufuatilia kuhakikisha mshauri elekezi anatimiza wajibu wake wa kuwasajili wafanyakazi muhimu, kama ilivyoelezwa katika Mahitaji ya Mwajiri (ToR) Kifungu Na.5.0 na 5.2 (c) cha mkataba wa huduma za ushauri, kuhakikisha wafanyakazi wote wanaofanya kazi za uhandisi wa kitaalamu wanasajiliwa.

Ushiriki wa wahandisi wasiosajiliwa unaweka hatarini ubora wa kazi iliyosimamiwa au kutekelezwa. Pia, kuajiri wafanyakazi wasiosajiliwa kunazuia uwezo wa mwajiri kuchukua hatua za kinidhamu katika kesi za makosa ya kitaaluma wakati wa utekelezaji wa mradi.

**Ninapendekeza kwamba TANROADS ihakikishe wafanyakazi muhimu wa washauri na wakandarasi wana sifa stahiki na wamesajiliwa na bodi za kitaaluma za ndani ya nchi.**

# SUTA YA TISA

## UKAGUZI WA KIUFUNDI JUU YA UJENZI WA MAGHALA YA KUHFADHI MAZAO YA CHAKULA



### 9.1 Utangulizi

Sura hii inaangazia ukaguzi wa kiufundi wa ujenzi wa vihenge na ukarabati wa maghala. Lengo kuu la ukaguzi wa kiufundi lilikuwa ni kutathmini kama Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ulizingatia matakwa ya usanifu, ugavi, ujenzi, majaribio ya ufungaji, makabidhiano ya vihenge, maghala na ukarabati wa miundombinu na vifaa vilivyopo kwa lengo la kuongeza uwezo wa kuhifadhi na kupunguza hasara zinazojitokeza baada ya mavuno nchini.

Taasisi iliyokaguliwa ilikuwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), chini ya Wizara ya Kilimo. NFRA ilikuwa mtekelezaji mkuu wa Mradi wa Upanuzi wa Hifadhi, ambao ulilenga kuongeza uwezo wa kuhifadhi ili kuhakikisha usalama wa chakula kwa taifa. Aidha, ukaguzi ulihusisha miaka ya fedha inayonzia 2015/16 hadi 2021/22. Kipindi hiki kilihusu mradi mzima, kuanzia kuanzishwa hadi kukamilika.

Mapitio ya nyaraka, mahojiano na uhakiki wa hali halisi, ukaguzi ulibaini matokeo yafuatayo ya ujenzi wa maghala na vihenge vya chuma kama ifuatavyo:

### 9.2 Upangaji na usanifu wa vihenge vya chuma

#### 9.2.1 Ongezeko la bajeti iliyopangwa kwa Sh. bilioni 208.3, sawa na 68% ya gharama ya mkataba

Wakala wa kuhifadhi chakula (NFRA) ulikuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa upembuzi yakinifu na wa kina unafanyika, na unakidhi vigezo vya kifedha, kiuchumi na kijamii kabla ya kuanza kwa kazi za ujenzi. Bajeti iliyopendekezwa katika upembuzi yakinifu wa vihenge na maghala ilikuwa dola za Marekani milioni 184 (sawa na Sh. bilioni 303), wakati hati iliyofuata ya tathmini ya mradi ilipendekeza dola za Marekani milioni 57.5, na kusababisha mabadiliko ya dola milioni 126.5 (pungufu ya 68%) ya bajeti. Kiasi kilichopendekezwa katika upembuzi yakinifu wa dola za Marekani milioni 184, sawa na Sh. bilioni 208.3, kinatokana na makadirio ya gharama zisizokuwa uhalisia.



## Ukaguzi Wa Kiufundi Juu Ya Ujenzi Wa Maghala Ya Kuhifadhi Mazao Ya Chakula

Pamoja na kupunguzwa kwa bajeti hiyo, uwezo wa kuhifadhi uliongezeka kwa tani 30,000 (kutoka tani 160,000 hadi 190,000) za ujazo,. Hii iliakisi ongezeko la tani za ziada zilizotengwa kwa maeneo kama Songea na Sumbawanga ambayo hayakuzingatiwa katika upembuzi yakinifu, lakini yalijumuishwa katika tathmini ya mradi, inayoonesha mbinu ya kina zaidi.

**Ninapendekeza kwamba NFRA ihakikishe kuwa upembuzi yakinifu unajumuisha makadirio sahihi ya gharama za uwekezaji na maelezo ya miradi itakayotekelezwa.**

### 9.2.2 Ripoti ya uchunguzi wa jiotekniki ya Mpanda kutoakisi hali halisi ya udongo, hali iliyosababisha kuongezeka kwa Sh. 683,911,461

Aya ya 1 ya Viwango vya Uingereza 5930:2015 inasema kuwa lengo la msingi la uchunguzi wa kijiotekniki(*geotecnic*) wa mchakato wa ujenzi ni kupanga njia bora ya ujenzi, kuona na kutoa njia ya kukabiliana na matatizo na ucheleweshaji unaoweza kutokea wakati wa ujenzi kutokana na hali ya ardhi, maji ya ardhini, na hali zingine za eneo husika, kuchunguza vyanzo vya nyenzo za kiasili kwa ajili ya matumizi ya ujenzi, na kuchagua maeneo ya kutupa taka au nyenzo za ziada.

Nilibaini kuwa mkandarasi M/s Unia Araj aliomba kulipwa fidia katika masuala ya fedha na muda kutokana na kukutana na hali tofauti za udongo na zile zilizobainishwa kwenye andiko la zabuni katika Mradi wa Mpanda. Zabuni ya awali ilibainisha kuwa mwamba ulianza kwenye kina cha mita 1.5 na ardhi yenye uwezo wa kipimo cha kilopaska (kPa)250 na udongo wa chini ambao mara nyingi hujumuisha mchanga na changarawe.

Hata hivyo, uchunguzi wa udongo wa mkandarasi uligundua mwamba ulikuwa hadi kwenye kina cha mita 12, ukiwa na ukomo wa wa juu wa kubeba uzito wa kilopasko (kPa) 155. Udongo wa chini ulikuwa umeundwa na udongo wa mfinyanzi na wa tiftufu wenye mchanga. Kutokana na hali hiyo, mkandarasi alipata dola za Marekani 299,567.85, sawa na Sh. 683,911,461, kwa ajili ya kuimarisha udongo na gharama zinazohusiana na mabadiliko ya usanifu. Hii inadhihirisha kuwa NFRA iliingia gharama zisizo za lazima ambazo zingeweza kuepukwa kwa kufanya shughuli za awali kwa usahihi.

**Ninapendekeza kwamba NFRA ifanye uchunguzi wa kijiotekniki unaoakisi hali halisi ya udongo katika siku zijazo ili kuepuka fidia wakati wa utekelezaji wa mradi.**



## Ukaguzi Wa Kiufundi Juu Ya Ujenzi Wa Maghala Ya Kuhifadhi Mazao Ya Chakula

### 9.2.3 NFRA kuondoa dhamana ya benki isiyo kuwa na masharti kwa ajili ya malipo ya awali ya Sh. 17,925,650,697

Kifungu cha 53.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) kwa mikataba yote kati ya NFRA na wakandarasi (Feerum S.A. na Unia Araj) kilimtaka mwajiri kulipa malipo ya awali ya 15% ya bei ya mkataba baada ya kuwasilisha dhamana ya benki isiyo na masharti.

Dhamana ya benki isiyo na masharti kwa ajili ya malipo ya awali iliondolewa katika mkataba wa nyongeza uliosainiwa kati ya NFRA, Feerum S.A., na Unia Araj tarehe 13 Februari 2017 na 15 Mei 2017. Kuondolewa huku kulisababisha NFRA kulipa malipo ya awali ya dola za Marekani 4,971,118.77 (sawa na Sh. 11,120,392,688) kwa Feerum S.A na dola za Marekani 3,042,135.90 sawa na Sh. 6,805,258,008 kwa M/s. Unia Araj bila dhamana. Jumla ya malipo ya awali ya dola za Marekani 8,013,254.67 (sawa na Sh. 17,925,650,697).

Licha ya kusitisha mkataba na M/s. Feerum S.A. na M/s. Unia Araj, ikiwa katika kipindi cha matazamiao ya mradi, NFRA haikuweza kurejesha dola za Marekani 1,672,617.63 na dola za Marekani 12,209.64 (sawa na jumla ya Sh. 3,741,645,638) kutoka kwa wakandarasi hao mtawalia, kutokana na msamaha huo wa dhamana. Urejeshaji kupitia njia zingine, kama vile kesi au mahakama, unachukuliwa kuwa ni wa gharama kubwa na inaotumia muda mwingi; hata hivyo, kwa M/s. Unia Araj, malipo yake ya awali yanaweza kurejeshwa wakati wa utayarishaji wa hati za mwisho za malipo ya kazi za ujenzi baada ya kipindi cha matazamiao ya mradi.

Ninapendekeza kwamba NFRA itekeleze matumizi ya dhamana za benki yasiyo na masharti kwa malipo ya awali kama dhamana kwa wakandarasi wote na kurejesha malipo ya awali yaliyosalia ya Sh. 3,741,645,638 kutoka kwa wakandarasi, huku ikihakikisha dhamana ya malipo ya awali inaotolewa kabla ya malipo.

### 9.3 Ujenzi wa vihenge vya chuma

#### 9.3.1 Malipo ya Sh. 315,812,546 kwa kazi za ujenzi ambazo hazikutekelwa kwa Vipande vya Songea na Shinyanga

Kipengele cha 39.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) kati ya M/s. Feerum S.A. na NFRA kinahitaji malipo kwa mkandarasi yafanywe kwa kazi zinazotekelezwa kwa kiwango kilichobainishwa kwenye makadirio ya gharama za mradi kwa kila kazi.

Mapitio ya Hati za Malipo ya Muda (IPCs) yalifichua kuwa mkandarasi alilipwa dola za Marekani 141,176.82 (Sh. 315,812,546). Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika katika eneo la mradi kwa kazi zilizofanyika ulifichua kuwa mkandarasi hakuwapo katika eneo la kazi. Hakukuwa na ulinzi kwa kazi zilizokuwa zimesalia, zikiwamo kuta, kazi za saruji za fremu, zege la asili, uimarishaji wa miundo ya mifereji ya maji, uchimbaji na udongo kwa ajili ya mashimo ya taka katika miradi ya Songea na Shinyanga. Maelezo ya gharama ya kazi ambazo hazikutekelezwa kwa kila mkoa yamewasilishwa katika **Jedwali 27**, wakati maelezo ya kazi zilizosalia yamewasilishwa katika **Kiambatisho Na. VII**.

**Jedwali 27: Kiasi kilicholipwa kwa kazi ambazo hazijatekelezwa**

Eneo la Mradi	Kiasi Kilicholipwa (dola za Marekani)
Songea	30,660.30
Shinyanga	110,516.52
<b>Jumla</b>	<b>141,176.82</b>

**Chanzo:** *Tathmini ya Ukaguzi ya Hati za Malipo na Uhakiki wa Ukaguzi Eneo la Mradi*

Jedwali namba 39 linaonesha kuwa takribani dola za Marekani 141,176.82 (sawa na Sh. 315,812,546) zilithibitishwa na kulipwa kwa mkandarasi kwa kazi ambazo hazikutekelezwa. Maafisa wa NFRA walisema kuwa suala la malipo ya kazi ambazo hazikufanyika lilikuwa nje ya uwezo wao na majukumu waliyopewa. Hii inaonesha kuwa NFRA ilitoa dola za Marekani 141,176.82 (sawa na Sh. 315,812,546) kwa kazi ambazo hazikufanyika kutokana na kutokuwapo kwa mkandarasi, na hakukuwa na ulinzi wa vifaa vya ujenzi.

Pia, nilibaini kuwa makadirio ya gharama za ujenzi za mradi kwa ajili ya mradi wa Shinyanga ilikusudiwa ujenzi mpya, siyo kazi za ukarabati kama ilivyotekelezwa na mkandarasi. Hivyo, malipo yaliakisi kazi za makadirio ya gharama za mradi wa ujenzi mpya, ilihali hakukuwa na makadirio ya gharama za ujenzi za mradi yaliyosahihishwa ili kuendana na kazi halisi za ukarabati. Kwa hiyo, malipo yaliyofanywa hayakuakisi usahihi kiasi cha kazi zilizotekelezwa, ikimaanisha kuwa gharama za mradi zilitarajiwa kupungua.

**Ninapendekeza NFRA ihakikishe kuwa malipo yanafanywa kwa ajili ya kazi halisi zinazotekelezwa pekee.**

### 9.3.2 Malipo ya Sh. Milioni 10.86 kwa vifaa vilivyofikishwa bila kusimikwa

Kipengele cha 39.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) kati ya M/s Feerum S.A na NFRA kinahitaji makadirio ya gharama za mradi kuwa na vipengele vya kazi ya ujenzi, ufungaji, upimaji, na kufanya uzinduzi. Pia, kipengele cha 39.2 kinataka malipo kwa mkandarasi yafanyike kwa kazi zinazotekelezwa kwa kiwango cha makadirio ya gharama za mradi kwa kila kipengele.

Katika mapitio ya hati za malipo na uhakiki niliufanya katika eneo la mradi, nilibaini kuwa NFRA ililipa dola za Marekani 4,853,039.42 (sawa na Sh. 10,856,249,183) kwa ajili ya usambazaji wa vifaa na ufungaji kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. VIII**. Hata hivyo, vifaa vya ujenzi vilivyoletwa vilibakia bila kusimikwa, kwani mkandarasi alitelekeza mradi tangu Desemba 2020. Malipo hayo yalifanywa kikamilifu bila M/s Feerum kutoa mchanganuo wa gharama, ikionesha gharama za usambazaji, ufungaji, upimaji, na uagizaji. Pia, meneja wa mradi aliidhinisha malipo hayo bila kufanya mchanganuo wake.

Madhara ya kuwasilisha vifaa bila kusimikwa, kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. VIII** ni uzembe wa kiutendaji wa kazi, ucheleweshaji wa mradi, na upotevu wa fedha, kwani manufaa yaliyokusudiwa ya kifaa hayatafikiwa hadi kisimikwe na kukabidhiwa. Pia, kitendo hiki kinazua wasiwasi kuhusu kutenga fedha kwa ajili ya vifaa visivyofanyiwa kazi, ikionesha uwezekano wa matumizi mabaya ya rasilimali, kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali 28**.

**Jedwali 28: Orodha ya maeneo na thamani ya vifaa vilivyolipiwa bila kusimikwa**

Sehemu mradi ulipotekelezwa	Kiasi katika dola za Marekani
Songea	1,1720,522.73
Mbozi	574,321.84
Dodoma	849,743.33
Makambako	1,132,219.93
Shinyanga	576,231.59
<b>Jumla</b>	<b>4,853,039.42</b>

**Chanzo:** Tathmini ya Hati za Malipo na Uhakiki wa Eneo la Mradi 2022/23

Hii inaonesha kuwa takribani dola za Marekani 4,853,039.42 (Sh. 10,856,249,183) zilizithibitishwa na kulipwa kwa M/s. Feerum S. A kwa ajili ya usambazaji, usimikaji, upimaji, na gharama za uzinduzi. Hata hivyo, kazi za ufungaji, upimaji na makabidhiano hazikufanyika.

Natoa rai kwa menejimenti ya NFRA kuhakikisha kuwa meneja wa mradi na wataalamu wakuu katika kusimamia ujenzi, ufungaji, upimaji na makabidhiano ya vihenge wanashirikishwa kikamilifu kama ilivyoelezwa kwenye mkataba. Pia, malipo yazingatie ushiriki wa wataalamu.

### 9.3.3 Ongezeko la gharama la Sh. bilioni 1.26 kutokana na mabadiliko ya eneo la ujenzi

Katika hatua za awali za utekelezaji wa mradi, NFRA ilimuagiza mkandarasi, M/s Unia Araj, kubadilisha maeneo ya ujenzi wa Sumbawanga na Babati. Tarehe 14 Februari 2019, lilitolewa agizo la kuhamisha eneo kutoka Mazwi hadi Kanondo kwa ajili ya eneo la Sumbawanga. Vilevile, kwa eneo la mradi wa Babati,



## Ukaguzi Wa Kiufundi Juu Ya Ujenzi Wa Maghala Ya Kuhifadhi Mazao Ya Chakula

maagizo ya mabadiliko yalitolewa tarehe 26 Februari 2019. Mfuatano wa matukio umefafanuliwa kwa kina katika **vielelezo Na. 2 na 3.**

### Kielelezo 2: Mfuatano wa matukio ya mabadiliko ya eneo la ujenzi Sumbawanga



**Chanzo:** Uchambuzi wa Wakaguzi kwa kutumia data ya taarifa za mradi, 2023

### Kielelezo 3: Mfuatano wa matukio ya kubadilisha eneo la ujenzi Babati



**Chanzo:** Uchambuzi wa Wakaguzi kwa kutumia data ya taarifa za mradi, 2023

Uamuzi wa kuhamisha eneo la Sumbawanga ulitokana na kuhamishwa kwa eneo la viwanda hadi eneo la Kanondo. Kwa upande wa Babati, kulikuwa na mwingiliano wa njia ya kusafirisha umeme mkubwa iliyokuwa katika mpango wa TANESCO. Kutokana na mabadiliko hayo ya eneo, wakandarasi walilipwa jumla ya fidia ya dola za Marekani 551,017 (sawa na Sh. 1,261,277,913<sup>2</sup>), yaani dola za Marekani 250,486.62 (sawa na Sh. 573,363,873) kwa eneo la Sumbawanga na dola za Marekani 300,530.31 (sawa na Sh. 687,913,880) kwa eneo la Babati.

Hii ina maana kwamba NFRA iliingia gharama ya dola za Marekani 551,017 (sawa na Sh. 1,261,277,913) ambazo zingeweza kuepukika kama ingefahamu mpango wa mapema wa eneo la ujenzi na kuchukua hatua kwa wakati.

**Ninapendekeza NFRA, kwa kushirikiana na mamlaka za mipango miji, ithibitisha kwamba eneo la ujenzi halina matumizi mengine shindani ili kuepuka usumbufu na gharama za ziada zinazotokana na kuhamishwa eno la ujenzi.**

<sup>2</sup> Kiwango cha ubadilishaji fedha kilichotumika kilikuwa sawa na Benki Kuu ya Tanzania kufikia tarehe 23 Januari 2018



## Ukaguzi Wa Kiufundi Juu Ya Ujenzi Wa Maghala Ya Kuhifadhi Mazao Ya Chakula

### 9.3.4 Malipo ya Sh. milioni 252.95 yalilipwa kwa TBA bila kuajiri wataalamu wa maghala katika shughuli za mradi zilizopendekezwa

Kipengele cha 1 cha makubaliano kati ya NFRA na mshauri elekezi, TBA, kilieleza kuwa mshauri huyo, baada ya kuthibitisha kwa mwajiri (NFRA) kwamba wana ujuzi wa kitaalamu, wafanyakazi, na rasilimali za kiufundi zinazohitajika, wakala (TBA) umekubali kutoa huduma kwa masharti yaliyobainishwa katika mkataba huo.

Niligundua kuwa NFRA ilikubaliana na TBA kuajiri mtaalamu wa vihenge kwa ajili ya shughuli mbalimbali kwa gharama za Sh. 254,150,000. Shughuli hizi ni pamoja na ukaguzi wa uchunguzi wa hali, ripoti fupi ya mbunifu na uanzishwaji, usanifu wa awali na usanifu wa kina, pamoja na ukaguzi wa hati ya zabuni, kazi za utangulizi kwenye mradi, na usimamizi wa ujenzi. Sambamba na makubaliano hayo, TBA uliingia mkataba na mtaalamu wa vihenge na maghala kwa ajili ya usimamizi wa mkataba ambao unamtaka mtaalamu kulipwa Sh. 600,000 kwa kila siku anayotumia katika eneo la mradi; na kikomo cha malipo cha juu cha mkataba kikiwa ni Sh. 127,200,000. Hata hivyo, NFRA ulilipa TBA Sh. 254,150,000 kwa ajili ya gharama ya kumwajiri mtaalamu wa vihenge na maghala aliyehusika katika shughuli za miradi kwa siku mbili ambazo ni sawa na Sh. 1,200,000 kwa mujibu wa kanuni na masharti ya mkataba.

Hii inaashiria kuwa TBA uliitoza NFRA Sh. 252,950,000 zaidi kwa wataalamu wa vihenge bila kushiriki katika shughuli zilizopendekezwa.

**Ninapendekeza kwamba NFRA irejeshe Sh. 252,950,000 ambazo zililipwa kwa TBA kama gharama iliyohusishwa na mtaalamu wa vihenge na maghala ambaye hakufika kwenye eneo la kazi.**

### 9.3.5 Kutokamilika kwa mradi wa Songea, Mbozi, Makambako, Shinyanga na Dodoma kwa muda wa miezi 44

Kipengele cha 1.1 cha mkataba kati ya NFRA na M/s Feerum S.A, uliotiwa saine tarehe 28 Desemba 2016 kinasema kuwa muda wa mkataba wa usanifu, ujenzi, usambazaji, upimaji na kukabidhi na uanzishwaji wa majengo ya maghala ya Songea, Mbozi, Makambako, Shinyanga, na Dodoma utakuwa miezi 17 tangu siku ya kuanza kwa mradi huo.

Kwa mujibu wa programu ya kazi iliyorekebishwa, miradi ya Songea, Mbozi, Makambako, Shinyanga na Dodoma ilicheleweshwa kwa muda wa miezi 44 kuanzia tarehe ya kuanza kwa mkataba, Juni 2018, hadi tarehe 7 Septemba 2023 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 29.

### Jedwali 29: Miradi ambayo haijakamilika

Eneo mradi ulipotekelezwa	Tarehe ya Kuanza kulingana na Mpango (A)	Tarehe ya Kukamilika inayopendeke zwa (B)	Miezi ya Muda wa Mradi (B-A)	Kuchel ewa (Mwezi C-B)	Hali ya Kukamilika kwa tarehe ya ukaguzi.
Dodoma	12 <sup>th</sup> Jun-2018	11 <sup>th</sup> Dec-2019	17	44	Haujakamilika
Songea	6 <sup>th</sup> Jun-2018	5 <sup>th</sup> Dec-2019	17	45	Haujakamilika
Mbozi	10 <sup>th</sup> Jun-2018	9 <sup>th</sup> Dec-2019	17	44	Haujakamilika
Makambako	8 <sup>th</sup> Jun-2018	7 <sup>th</sup> Dec-2019	17	45	Haujakamilika
Shinyanga	12 <sup>th</sup> Jul-2018	11 <sup>th</sup> Jan-2020	17	43	Haujakamilika

Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi wa Maendeleo ya Juni 2021

Hadi kukamilika kwa ukaguzi huu, tarehe 19 Januari 2024, miradi hii ilikuwa imeachwa na haijakamilika. Kutokana na upungufu unaohusiana na usimamizi wa muda, NFRA ilipata matokeo yafuatayo:

**(a) NFRA ilitumia Sh. 1,263,315,300 kwa ajili ya kukodi maghala ya ziada ya kuhifadhi kutokana na kuchelewa kukamilika kwa miradi ya Songea, Makambako, Shinyanga na Dodoma kwa miezi 44**

Kutokana na kuchelewa kukamilika kwa miradi ndani ya muda uliopangwa, NFRA ilikuwa na upungufu wa maeneo ya kuhifadhi mazao kwa asilimia 64.7. Hii ilisababisha matumizi ya Sh. 1,263,315,300 kwa kukodisha maghala ya ziada ya kuhifadhi mazao.

**(b) Uchakavu wa vifaa vya ujenzi wa vihenge ambavyo vilitelezwa nje**

Katika ziara ya ukaguzi katika eneo la kazi, niliona vifaa vya ujenzi wa ghala vikiwa vimetelekezwa kwenye eneo la mradi, vikipigwa na mvua na jua, na kusababisha kutu na kuharibika. Uamuzi wa NFRA wa kutoa vipande vitano vya kazi venye thamani ya juu kwa mkandarasi mmoja aliye na uwezo duni ikilinganishwa na uzoefu wa zamani katika kazi kama hizo ulihatarisha utekelezaji wake.

Wahandisi wa mradi walionesha kuwa vifaa vilivyo kwenye eneo la mradi kutokana na kuchelewa kutatua migogoro kati ya mwajiri na mkandarasi vilikuwa katika hatari ya kutofaa kwa ujenzi, hivyo kulazimika kubadilishwa. Ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusuluhisha ukiukwaji wa mkataba kwa njia za kidiplomasia haukubainishwa katika makubaliano kati ya serikali na serikali au mkataba, jambo lililozidisha ugumu.

Vifaa vya ujenzi kama vile makarai ya lifti yalikuwa na kutu na vifaa vingine vilipatikana katika maeneo ya mradi ya Shinyanga na Dodoma. Vifaa hivyo

vilivyoharibika viligharimu dola za Marekani 451,731.60, hivyo vinaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama za mradi (tazama Kielelezo Na. 4).

**Kielelezo 4: Vifaa vya ujenzi vilivyotelekezwa na kuharibika**

*Picha iliyopigwa na wakaguzi tarehe 13 Oktoba 2023 katika eneo la ujenzi Dodoma*



*Picha iliyopigwa na wakaguzi tarehe 27 Oktoba 2023 katika eneo la ujenzi Shinyanga*

**Ninapendekeza NFRA ukamilishe vipande vitano (vya Songea, Dodoma, Mbozi, Shinyanga na Makambako) vilivyobaki ili kuepusha uchakavu zaidi wa vifaa vilivyotelekezwa katika eneo la ujenzi na kuepuka gharama ya kukodi maghala.**

# SURA YA KUMI

## UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA VYUO VYA MAFUNZO (VETA) KATIKA MIKOA NA WILAYA



### 10.1 Utangulizi

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali ilitenga Shilingi 40 bilioni kwa ajili ya ujenzi wa Vituo 25 vya Ufundi Stadi vya Wilaya, na nyongeza ya Shilingi 28.7 bilioni kutoka katika Mpango wa Kuu Uchumi na Kukabiliana na Ugonjwa wa UVIKO-19 (TCRP) kwa ajili ya kukamilisha ujenzi na kuweka samani. Aidha, katika mwaka 2022/23, Shilingi bilioni 100 zilitengwa kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya kujenga vyuo 63 vya ziada vya Ufundi Stadi nchi nzima, kikiwemo chuo cha Mkoa wa Songwe.

Ukaguzi wa Kiufundi ulitathmini usimamizi wa MOEST na VETA wa ujenzi wa Vituo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi, kwa kuzingatia upangaji wa miradi, ununuzi, usimamizi wa fedha, na kuzingatia viwango vya mazingira na usalama. Ukaguzi ulifanya mapitio ya vituo vitatu vya Ufundi vya Mkoa ya Njombe, Geita, Songwe) na Wilaya tisa (Korogwe, Lushoto, Uyui, Igunga, Chemba, Bahi, Njombe, Bukombe na Songwe), kuanzia kipindi cha utekelezaji wa 2019/20 hadi 2023/24.

Mapitio ya nyaraka, mahojiano na uhakiki wa hali halisi, ukaguzi ulibaini matokeo yafuatayo ya ujenzi wa vituo vya mafunzo vya VETA katika mikoa na wilaya kama ifuatavyo:

### 10.2 Upangaji na usanifu wa ujenzi wa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi

#### 10.2.1 Kutotoa vifaa vya utambuzi na kupambana na moto katika vyuo 25 vya mafunzo ya ufundi stadi ngazi ya Wilaya vilivyojengwa

Kanuni ya 248(1) ya Kanuni za Zimamoto na Uokoaji za mwaka 2015 inataka kupata ushauri kutoka kwa mamlaka ya zima moto kabla ya kuidhinisha mipango ya jengo, upanuzi au mabadiliko ya usanifu ili kuhakikisha uzingatiaji wa usalama wa moto.



## Ukaguzi Wa Kiufundi Wa Ujenzi Wa Vyuo Vya Mafunzo (Veta) Katika Mikoa Na Wilaya

Mapitio yangu ya michoro ya vituo 25 vya mafunzo ya ufundi stadi (VETA) ngazi ya wilaya yalionesha kuwa vifaa vya kuzimia moto kama vile kengele za kuashiria hatari ya moto, vitambuamoto na vitambuamoshi vilikuwa vimewekwa kwenye michoro ya usanifu ya jikoni na kwenye karakana. Hata hivyo, orodha ya vifaa ilionesha kuwa, ni vizimamoto pekee vilivyokuwa vimejumuishwa, lakini havikuwekwa kwenye vituo vya mafunzo ya ufundi stadi ngazi ya wilaya husika. Gharama ya makadirio ya vifaa vya kuzima moto ambavyo havikufungwa ilikuwa Sh. 10,000,000 kwa kila kituo na kufanya jumla ya Sh. 250,000,000 kwa vituo vyote 25.

Hii inamaanisha kwamba, hakukuwa na vifaa vya kuzima moto vilivyowekwa kwenye vyuo vya ufundi stadi vya wilaya 25 vilivyojengwa kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi wa kuhalalisha sababu hii. Kutofungwa kwa vifaa hivyo vya kuzimia moto katika vituo 25 vya mafunzo ya ufundi stadi ngazi ya wilaya vilivyojengwa kunapunguza uwezekano wa kudhibiti maafa ikiwa majanga ya moto yatatokea. Pia, hii inamaanisha kwamba Sh. bilioni 2.6 zilizowekezwa katika ujenzi wa kituo kimoja kimoja cha mafunzo ya ufundi stadi ngazi ya wilaya zitakuwa hatarini endapo janga la moto litatokea.

**Ninapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na VETA waimarishe michakato ya usanifu wa mradi na kuhakikisha kuwa orodha za vifaa zinaonesha hali halisi ya mradi na kujumuisha mahitaji ya usalama wa moto.**

### 10.3 Usimamizi wa mikataba ya ujenzi wa vituo vya ufundi stadi (VETA)

#### 10.3.1 Kuchelewa kukamilika kwa mradi wa Vituo vya mafunzo ya ufundi stadi na kusababisha gharama ya miradi kuzidi kwa Sh. milioni 175.62

Aya ya 2.0 ya waraka wa mradi wa mwaka 2019 wa ujenzi wa vituo 25 vya mafunzo ya ufundi stadi ngazi ya wilaya katika wilaya inataka kazi hizo zikamilike ifikapo tarehe 30 Juni 2023 kwa kutumia rasilimali au uwezo wa ndani.

Nilibaini ucheleweshaji wa vituo vya ufundi stadi kati ya miezi 32 na 44 kuanzia tarehe 03 Machi 2020 hadi 30 Novemba 2023 kwa vituo vitano kati ya sita. Ni chuo cha mafunzo ya ufundi stadi wilaya ya Igunga pekee ndicho kilichokuwa kimekamilika kufikia tarehe 30 Novemba 2023. Sababu kuu ya ucheleweshaji huu ni VETA kusuasua katika utoaji wa fedha ambao hauendani na hatua muhimu za mradi, hivyo kukwamisha kukamilika miradi kwa wakati.

Kutoendana huko kwa utoaji wa fedha na hatua muhimu za mradi kulisababisha kuongezeka kwa gharama, hususani kwa madirisha ya aluminiamu katika vituo vya mafunzo ya ufundi stadi wilaya za Chemba, Bahi, Igunga, Korogwe, na Lushoto. Mchanganuo wa gharama za ujenzi wa madirisha ya aluminiamu ulionesha kuwa kazi zilikadiriwa kutekelezwa kwa Sh. 231,734,647. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji, gharama zilizotumika kwa kazi za aluminiamu ilikuwa Sh. 407,350,839. Hii ilionesha ongezeko la Sh. 175,615,952 kama inavyooneshwa katika **Jedwali 30**.

**Jedwali 30: Ongezeko la gharama kwa madirisha ya aluminiamu**

Mradi	Eneo la kazi za alumini (m <sup>2</sup> )	Bei iliyokadiriwa katika ratiba ya vifaa kwa kila m <sup>2</sup> (Sh)	Bei iliyolipwa wakati wa Utekelezaji halisi (Sh)	Ongezeko la Bei/m <sup>2</sup> (Sh)	Kiasi Kilichoongezwa (Sh)
Chuo cha VETA Bahi	155	106,977	221,987	115,010	17,826,534
	129.4	106,977	215,000	108,023	13,978,150
Chuo cha VETA Chemba	26.4	106,977	220,000	113,023	2,983,802
	243	106,977	215,000	108,023	26,249,540
Chuo cha VETA Korogwe	737.32	106,977	169,805	62,828	46,324,053
Chuo cha VETA Lushoto	79.34	106,977	200,000	93,023	7,380,429
Chuo cha VETA Igunga	795.75	106,977	183,475	76,498	60,873,442
<b>Jumla</b>					<b>175,615,952</b>

**Chanzo:** Agizo la Ununuzi wa Ndani na mabadiliko ya gharama za bidhaa

Bei ya mita moja ya mraba ya aluminiamu ilikadiriwa kuwa Sh. 106,977. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji, bei ya aluminiamu iliongezeka. Ongezeko la juu zaidi lilipatikana katika kituo cha mafunzo ya ufundi stadi cha Bahi, ambapo mita ya mraba ya dirisha iliongezwa kwa Sh. 115,009, na ongezeko la chini la bei lilibainika katika kituo cha mafunzo ya ufundi stadi ngazi ya wilaya ya Korogwe kikiwa na nyongeza ya Sh. 62,827.6 kwa kila mita ya mraba ya madirisha ya aluminiamu.

**Ninapendekeza** Wizara ya Elimu, sayansi na teknolojia na VETA wauimarisha usimamizi, kuhakikisha utoaji wa fedha mara moja, kuagiza wahandisi waliosajiliwa kwa ajili ya uangalizi wa ujenzi, na kudumisha ubora wa kazi ili kuzuia gharama za ziada za mradi.

# SURA YA KUMI NA MOJA

## UKAGUZI WA KIUFUNDI WA NJIA YA KUSAFIRISHA UMEME KUTOKA BWAWA LA KUFUA UMEME LA JULIUS NYERERE HADI CHALINZE NA UJENZI WA KITUO CHA KUPOOZEA UMEME CHA CHALINZE



### 11.1 Utangulizi

Kuanzia mwaka 2017, Serikali ya Tanzania ilianza mradi mkubwa unaolenga kuimarisha miundombinu ya umeme nchini. Mradi huu ulihusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP) hadi kituo cha kupoozea umeme cha Chalinze, ikijumuisha uwekaji wa kituo chenye uwezo mkubwa wa kupoozea umeme na njia nyingi za kusambaza umeme kwa ufanisi wa usafirishaji umeme.

Ujenzi wa Mtambo wa Umeme wa Maji cha Julius Nyerere (JNHPP), wenye uwezo wa kuzalisha MW 2,115, una maendeleo makubwa. Kwa sasa mtambo huu umekamilika kwa zaidi ya 90% na unatarajiwa kufanya kazi kikamilifu ifikapo mwisho wa 2024.

### 11.2 Hatua za Maendeleo katika Uzalishaji wa Nishati

Njia za kuhamisha umeme kwa JNHPP pia zinaendelea vizuri. Njia ya msingi ya kusafirisha umeme kutoka JNHPP hadi Chalinze inakaribia kukamilika, na kituo chenyewe cha Chalinze kimekamilika kwa 85%. Njia za usafirishaji umeme kutoka Chalinze hadi Dodoma, Kinyerezi (DSM), na Segera (Kanda ya Kaskazini) zote zinaendelea kutengenezwa.

Ni vyema kutambua jitihada za Serikali katika mradi huu ambapo Januari 2024, Wizara ya Fedha ilitenga TZS 111.50 bilioni kwa ajili ya kuanzisha njia ya kusambaza umeme ya 400kV kutoka Chalinze hadi Dodoma. Ujenzi wa njia za msongo wa kV 400 kutoka Chalinze hadi Kinyerezi (DSM) na Chalinze hadi Segera (Kanda ya Kaskazini) unaendelea.

**Pamoja na hatua iliyofikiwa hadi sasa, bado napendekeza TANESCO kuongeza juhudi katika kukamilisha kwa wakati njia za kusambaza umeme ili kutumia kikamilifu nishati inayozalishwa.**



## **Ukaguzi Wa Kiufundi Wa Njia Ya Kusafirisha Umeme Kutoka Bwawa La Kufua Umeme La Julius Nyerere Hadi Chalinze Na Ujenzi Wa Kituo Cha Kupoozea Umeme Cha Chalinze**

### **11.3 Usimamizi wa ununuzi**

#### **11.3.1 Kuchelewa kumpata Mhandisi Mshauri kwa muda wa miezi minane na kumlipa Mhandisi mshauri huyo kazi ambazo hazikutekelezwa**

Nilibaini ucheleweshwaji wa kumwajiri mhandisi mshauri kwa kazi ya ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme ya msongo wa kV 400 na kituo cha kupoozea umeme cha Chalinze kwa miezi minane baada ya wakandarasi husika wakiwa tayari wameanza kazi.

Mhandisi mshauri aliajiriwa baada ya kuanza kwa mradi. Alisimamia njia ya kusafirishia umeme ya msongo wa kV400 na mradi wa kituo cha kupoozea umeme cha Chalinze, huku asilimia 14% za usanifu wa nia ya kusafirishia umeme zikiwa tayari zimekamiliwa. Pamoja na hayo, TANESCO halikurekebisha mkataba na kupunguza asilimia 14 ya kazi iliyofanyika kabla ya ushirikishwaji wa mshauri. Kiasi hicho ni sawa na dola za Marekani 94,934 na Sh. 87,127,600 sawa na Sh. 308,087,434. Barua ya tarehe 11 Aprili 2023 ilithibitisha mshauri kuidhinisha dola za Marekani 112,469.04 kwa kazi mbalimbali za usanifu wa njia ya usafirishaji, lakini hakukuwa na ushahidi kama kazi hizi za usanifu zilitekelezwa.

Ninapendekeza TANESCO lifuate mfumo wa malipo unaozingatia utendaji kazi kwa mikataba ya washauri; na kubainisha malipo na malipo yaliyoainishwa kwa kila hatua ya kazi iliyokamilika. Pia, TANESCO linapaswa kurejesha 14% ya gharama ya kazi ya awali ya mshauri Sh. milioni 308.09. TANESCO pia ihakikishe washauri wanalipwa kwa kazi iliyokamilika tu, pamoja na kifungu cha kuzuia malipo ikiwa hatua muhimu hazijafikiwa.

### **11.4 Usimamizi wa muda, gharama na ubora wa kazi**

#### **11.4.1 Kuchelewa kukamilika kwa njia ya kusafirishia umeme na kituo kidogo cha kupoozea umeme cha Chalinze**

Mnamo tarehe 31 Oktoba 2022, Mkandarasi alipokea nyongeza ya muda wa miezi 3.5, ambapo kikomo kilikuwa tarehe 28 Februari 2023 kama ilivyobainishwa kwenye barua yenye nambari ya kumbukumbu DMD PRI/DRIP/MP/PM JNHPP/L/22/PE514. Licha ya nyongeza hii, mkandarasi hakukamilisha kazi hadi wakati wa ukaguzi (30 Novemba 2023). Hii ilisababisha kuchelewa kukamilika mradi kwa miezi 14 kutoka tarehe iliyokusudiwa kukamilika kwa mradi, yaani tarehe 31 Oktoba 2022.



## **Ukaguzi Wa Kiufundi Wa Njia Ya Kusafirisha Umeme Kutoka Bwawa La Kufua Umeme La Julius Nyerere Hadi Chalinze Na Ujenzi Wa Kituo Cha Kupoozea Umeme Cha Chalinze**

Mnamo tarehe 21 Februari 2023, mkandarasi aliomba tena kuongezewa muda kutokana na masuala kadhaa. Miongoni mwayo ni: uhaba wa askari wa TANAPA ambao wangemsaidia kulinda wafanyakazi wake kipindi cha ujenzi eneo la hifadhi; mabadiliko ya hali ya hewa na ubovu wa barabara; changamoto za uchimbaji wa mawe magumukipindi cha uchimbaji wa msingi; kukosekana kwa meli za usafirishaji mizigo; kucheleweshwa kwa malipo; kuharibika kwa mitambo; mlipuko wa UVIKO-19 nchini China; kucheleweshwa kwa fidia za eneo la kazi; pamoja na kucheleweshwa kwa hati za makabidhiano eneo la ujenzi. Licha ya kuweka malengo ya kumaliza mradi hadi mnamo Novemba 2022 kwa kazi iliyobaki, kama ilivyobainishwa kwenye taarifa ya robo mwaka sehemu namba 5 ya Septemba 2023, mradi ulikuwa bado haujakamilika hadi tarehe 30 Novemba 2023.

Kwa upande mwingine, nilibaini kuwa kituo cha kupoozea umeme cha Chalinze kilicheleweshwa kwa muda wa miezi 10 kuanzia muda kuongezwa hadi wakati wa ukaguzi (29 Januari 2024). Licha ya ongezeko la muda liliotolewa kuanzia tarehe 11 Januari 2023 hadi 30 Novemba 2023, mradi ulikuwa bado haujakamilika. Hadi tarehe 30 Desemba 2023, mradi ulikuwa umefikia maendeleo ya 85.50%.

Ucheleweshaji wa mradi wa kituo cha kupoozea umeme cha Chalinze ulichangiwa hasa na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 ambao ulisababisha kuahirishwa majaribio ya kuwasha umeme.

**Ninapendekeza TANESCO iboreshe usimamizi wa mikataba na kushughulikia kwa haraka matukio yoyote na changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi, kwa kuzingatia kuongeza kasi ya kukamilika kwa kituo cha kupoozea umeme na kuhakikisha utengenezaji na utoaji wa vifaa vya umeme na vya kielektromekaniki kwa wakati.**

### **11.4.2 Kucheleweshwa kwa malipo ya mkandarasi na mshauri elekezi kwa muda wa kuanzia siku 1 hadi 264**

Malipo kwa mkandarasi na mshauri yalitakiwa kufanywa ndani ya siku 90 kwa mkataba wa mkandarasi na siku 60 kwa huduma za ushauri, mtawalia, kwa mujibu wa kipengele cha 12.1 caha matakwa ya mkataba wa njia ya kusafirishia umeme ya msongo wa kV400 na kipengele cha 57.2 cha mkataba mpya wa kituo cha kupoozea umeme cha MVA 250 na hadidu za rejea za Mshauri sambamba na mara tu baada ya kupokelewa kwa ankara na nyaraka za usaidizi, kulingana na masharti ya mkataba.



## **Ukaguzi Wa Kiufundi Wa Njia Ya Kusafirisha Umeme Kutoka Bwawa La Kufua Umeme La Julius Nyerere Hadi Chalinze Na Ujenzi Wa Kituo Cha Kupoozea Umeme Cha Chalinze**

Niligundua kuwa malipo kwa mkandarasi wa laini ya kusambaza umeme, M/s Larsen na Toubro Ltd, yalicheleweshwa kati ya siku 1 na 264 zaidi ya siku 90 zilizoainishwa. Hii ilisababishwa hasa na mgao wa polepole wa fedha kutoka Wizara ya Fedha kwa fedha za mradi. Kwa hivyo, hii iliathiri mtiririko wa pesa za mradi, na kuzuia maendeleo yake na kusababisha kuongezwa kwa muda wa ujenzi kwa miezi 10.

Vile vile, nilibaini ucheleweshwaji kwa malipo ya mshauri kwa muda wa kati ya siku 25 na 124. Ucheleweshaji wa malipo uliathiri mtiririko wa kifedha wa mshauri. Walakini, hakuna sababu ya kucheleweshwa kwa malipo iliyoripotiwa. Ucheleweshaji huu wa malipo unaweza kusababisha madai ya riba ya mshauri.

**Napendekeza TANESCO ihakikishe malipo kwa Mkandarasi na Mshauri yanafanyika kwa wakati ili kuepusha usumbufu wa maendeleo na madai ya baadaye kutoka kwa wakandarasi na washauri.**

### **11.4.3 Uwekaji duni na ushindilaji duni wa vifusi katika miguu yote ya Minara ya njia za usafirishaji umeme wa kV400**

Kipengele cha 7 cha Kifungu cha 1.17.1 cha matakwa na vigezo vya viwango vya kiufundi pamoja na matakwa ya mwajiri kwa ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme ya msongo wa kV 400 kinamtaka mkandarasi kuhakikisha kazi zote za miradi zinafanywa na watu wazoefu, kwa kutumia vifaa vya ujenzi vyenye ubora na viwango; na kuhakikisha kuwa ubora na viwango unafikiwa kutokana na vigezo vya viwango vilivyowekwa katika mkataba na vile vya kimataifa.

Uhakiki wa ukaguzi wa kazi zilizofanyika, uligundua kuwa miguu na misingi yote ya minara na nguzo za umeme iliyotathminiwa kando ya njia ya usafirishaji wa umeme kuikushindiliwa vyema. Mifano ya miguu ya minara au nguzo hizo ni DE 01 (TT2), DE 02 (TAP01/1), NS 03 (TAP01/2), na HA 04 (TCIC/01). Pia, niliona kuwa hadi tarehe 26 Oktoba 2023, hakukuwa na mgandamizo wa udongo wa kutosha kuzunguka miguu ya mnara/nguzo za umeme, kama inavyoonekana kwenye **Picha Na. 5**.

11

## Ukaguzi Wa Kiufundi Wa Njia Ya Kusafirisha Umeme Kutoka Bwawa La Kufua Umeme La Julius Nyerere Hadi Chalinze Na Ujenzi Wa Kituo Cha Kupoozea Umeme Cha Chalinze

**Kielelezo 5: Ujazaji duni wa vifusi kwenye misingi ya Minara ya umeme**



*Chanzo: Ukaguzi wa uwandani, tarehe 20 Oktoba 2023*

Ushindiliaji wa udongo duni ulitokana na usimamizi usiojitosheleza wa mshauri elekezi kwa mkandarasi (M/s Larse & Turbo). Ingawa baadaye mshauri elekezi aliagiza kuongeza idadi ya wasimamizi wa mradi, maagizo yalikuja kwa kuchelewa, hivyo kusababisha kushindwa kuzingatia mpango wa udhibiti wa ubora na mpango wa uhakikisho wa ubora wa mradi.

Ninapendekeza TANESCO liongeze uhakiki na udhibiti wa ubora wa mradi wa njia ya usafirishaji umeme wa msongo wa kV400 na kituo cha kupoozea umeme cha Chalinze kwa kuhakikisha kuwa wakandarasi wanazingatia viwango, vipimo, na masharti ya kimkataba. Aidha, TANESCO lihakikishe mshauri elekezi anatimiza wajibu wake kama ilivyobainishwa katika hadidu za rejea.

# SURA YA KUMI NA MBILI

## UKAGUZI WA KIUFUNDI JUU YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI



Ukaguzi wa kifundi wa miradi inayotekelezwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kuanzia 2021/22 hadi 2022/23 umefanyika ili kutathmini matumizi ya fedha na ufanisi katika utekelezaji wa miradi nane ambayo imetekelezwa katika mikoa ya Iringa, Dodoma, Tabora, Arusha, Rukwa, Singida, Manyara na Mwanza. Taarifa za miradi ya umwagiliaji iliyokaguliwa zimeoneshwa katika **Jedwali 31**.

**Jedwali 31: Ujenzi wa miradi ya umwagiliaji hadi tarehe 30 septemba 2023**

Jina la Mradi	Hatua ya Mradi (%)	Hatua ya malipo (%)	Muda uliotu mika (%)	Muda wa Mradi		Gharama (Sh. Bilioni)
				Muda wa kuanza	Muda wa kukamilika	
Miundombinu ya Umwagiliaji ya Eyasi Mkoa wa Arusha	8	15	29	21 Aprili 2023	20 Oktoba 2024	38.43
Miundombinu ya Umwagiliaji ya Lyamalagwa - Mkoa wa Tabora	6	15	25	16 Mei 2023	15 Novemba 2024	29.96
Miundombinu ya Umwagiliaji ya Magulukenda - Sukuma - Mkoa wa Mwanza	86	51	106	27 Septemba 2022	27 Septemba 2023	40.1
Miundombinu ya umwagiliaji ya Mkombozi - Kipande cha I - Mkoa wa Iringa	57	28	72	01 Septemba 2022	29 Februari 2024	8.12
Skimu ya umwagiliaji ya Mkombozi - Kipande cha II - Mkoa wa Iringa	31	15	72	01 Septemba 2022	29 Februari 2024	13.46
Skimu ya umwagiliaji ya Mkombozi - Kipande cha III - Mkoa wa Iringa	30	15	72	01 Septemba 2022	29 Februari 2024	15.92
Skimu ya umwagiliaji ya Mkombozi - Kipande cha IV mkoa wa Iringa	44	15	72	01 <sup>st</sup> Septemba 2022	29 Februari 2024	18.00
Skimu ya umwagiliaji ya Ilemba - mkoani Rukwa	7	15	18	22 Juni 2023	22 Desemba 2025	21.02
Bwawa la Membe - mkoani Dodoma	84	62	117	01 Septemba 2022	30 Agosti 2023	10.96
Bwawa la Msagali - mkoani Dodoma	55	56	83	12 Oktoba 2022	12 Aprili 2024	27.96

Jina la Mradi	Hatua ya Mradi (%)	Hatua ya malipo (%)	Muda uliotu mika (%)	Muda wa Mradi		Gharama (Sh. Bilioni)
				Muda wa kuanza	Muda wa kukamilika	
Skimu ya Umwagiliaji ya Msingi - Mkoa wa Singida	1	15	17	14 Juni 2023	14 Desemba 2024	29.18
Skimu ya umwagiliaji ya Tlawi - Mkoa wa Manyara	75	31	75	15 Februari 2023	14 Dec, 2023	6.42

**Chanzo:** Mikataba, hati za malipo na taarifa za utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji

### 12.2 Upembuzi yakinifu usio na maelezo ya kina

Kifungu cha 20 (3) (g) cha Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2013 na aya ya 9 ya Mwongozo Kabambe wa Maendeleo ya Mtandao wa Umwagiliaji, Juzuu la 2, Toleo la nne 2019, imeweka vigezo maalumu vya kufanya upembuzi yakinifu wa kina wa miradi ya umwagiliaji.

Mambo yanayotakiwa katika miradi ya umwagiliaji ni pamoja na uchunguzi wa udongo, uchunguzi wa miamba, tafiti za hali ya maji zinazojumuisha usawa wa maji na upatikanaji wake, na uchanganuzi wa udongo wa kilimo unaojumuisha uchunguzi wa kina na tathmini za uwezo wa ardhi. Vigezo hivi vinahakikisha upangaji kamili na usalama wa kazi za umwagiliaji.

Ukaguzi wa ulibaini kuwa, katika miradi ya umwagiliaji ya Eyasi, Lyamalagwa, Mkombozi na Magulukenda - Sukuma, upembuzi yakinifu uliofanywa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ulikuwa na upungufu hususan kukosa tathmini za kina ambazo zilikuwa muhimu kwa utekelezaji wa miradi hiyo.

#### Tathmini ya Udongo (kijioteknolojia) haikufanyika sehemu ya kuchukulia maji ya umwagiliaji na kando ya mifereji wa umwagiliaji

Kifungu cha 2.2 cha Mwongozo wa Usalama wa Mabwawa wa Wizara ya Maji unahitaji upembuzi yakinifu kujumuisha ripoti za uchunguzi wa kijiojiojia na kijioteknolojia sehemu ya kuchukulia maji ya umwagiliaji na kando ya mfereji.

Tathmini ilibaini kuwa miradi hiyo ya umwagiliaji ilikosa uchunguzi muhimu wa kijiografia—sehemu ilipojengwa miundombinu ya kuchukulia maji ya umwagiliaji na kando ya mfereji. Hali hiyo ilisababishwa na Tume ya umwagiliaji kutokuwa na ufahamu wa umuhimu wa taarifa hizo. Kasoro hiyo ilisababisha kufungwa kwa mashine ili kushughulikia maji yaliyokuwa yanatoka ardhini katika mtandao wa umwagiliaji wa Magulukenda - Sukuma. Jambo hili lilitokana na kupuuza tathmini za awali za jioteknolojia.

**Hali halisi ya wingi wa maji yanayopatikana haikuzingatiwa wakati wa utafiti wa hali ya maji**

Ukaguzi ulibaini kuwa tafiti za kihaidrolojia katika miradi yote ya umwagiliaji zilitegemea zaidi modeli ya mafuriko yatokanayo na kiwango cha juu cha mvua kwa miaka 50 bila kuhakiki au kuthibitisha na taarifa za wingi halisi wa maji yanayotiririka katika chanzo cha maji. Hii ilisababishwa na vyanzo vya maji kutokuwa na rekodi zinazoonesha wingi wa maji yanayopatikana. Modeli hii inahatarisha ustahimilivu wa mitandao ya umwagiliaji kwani inaweza kusababisha usanifu wa miundombinu yenye uwezo usioendana na wingi halisi wa maji yaliyopo.

**Tafiti za awali za uchunguzi wa udongo zilikuwa na uhaba wa taarifa na mapendekezo**

Niligundua kuwa utafiti unaofanywa kwenye udongo haukotoa taarifa za virutubishi vyote vya udongo. Pia, sampuli chache zilikuchuliwa kwa eneo kubwa, ambapo sampuli tatu tu ziliwakilisha eneo la hekta 500 katika mradi wa Magulukenda - Sukuma. Zaidi, hazikuwa na maelezo maalumu ya mahali ambapo kila sampuli ilichukuliwa.

Taarifa zinazokinzana katika upembuzi yakinifu zinaweza kusababisha maamuzi yanayopotosha uboreshaji wa udongo. Hali hiyo inaweza kusababisha matokeo yasiyotarajiwa kama vile mabadiliko ya pH ya udongo na chumvi inayoweza kuathiri uzalishaji wa mashamba yanayoandaliwa.

**Ninapendekeza kwamba, ili kuepuka matatizo na kuhakikisha matokeo bora ya umwagiliaji, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ifanye upembuzi yakinifu unaojumisha uchunguzi wa kina wa matabaka ya udongo na maji yatakayo tumika katika umwagiliaji kulingana na vigezo na viwango vya kubuni miradi ya umwagiliaji.**

### **12.3 Usanifu wa skimu ya umwagiliaji haukufanyika ipasavyo**

Chini ya kipengele cha usanifu wa skimu ya umwagiliaji, mambo yafuatayo yalionekana:

**Kutokuwapo kwa usanifu wa ukomo wa matumizi ya miradi**

Aya ya 20 ya Mwongozo Kabambe wa Ukuzaji wa Skimu ya Umwagiliaji, Juzuu la 2, Toleo la nne 2019, inasisitiza umuhimu wa kuzingatia vipengele vyote muhimu vya mradi, ukiwamo ukomo wa maisha ya miradi na miundombinu

muhimu kama vile barabara za mashambani, na ukomo wa maisha ya miradi uliotakiwa kufanyika wakati wa usanifu wa mradi.

Ukaguzi ulibaini upungufu mkubwa katika ripoti za usanifu kwa sampuli za mitandao ya umwagiliaji zilizokaguliwa, kuwa hazikujumuisha ukomo wa matumizi ya miradi. Mkengeuko huu wa usanifu wa miradi (wa kutofafanua wazi muda wa uendeshaji wa mradi na muda wa kudumu kwake) unaleta mashaka kuhusu uendelevu na ufanisi wa gharama ya mtandao wa umwagiliaji.

Kutokuwapo kwa kipengele cha ukomo wa matumizi ya miradi katika usanifu kunachangia kutokuwapo kwa mpango kabambe wa muda wa matengenezo ya miradi hiyo, hali inayoweza kusababisha kuongezeka kwa gharama za kuendesha miradi hiyo na kushindwa kufanya kazi.

#### **Kutokuwapo kwa Usanifu wa barabara za shambani**

Licha ya mahitaji yaliyobainishwa katika aya ya 20 ya Mwongozo Kabambe wa Maendeleo ya skimuya umwagiliaji, ukaguzi umebaini kuwa barabara za skimu za umwagiliaji za Mkombozi, Eyasi, na Magulukenda-Sukuma hazijafanyiwa usanifu kama matakwa ya mwongozo namba 20 unavyotaka.

Kutofanyika kwa usanifu wa barabara za mashambani kunaweza kusababisha ujenzi wa barabara wenye viwango duni, na kuathiri vibaya ufanisi na utendaji kwa ujumla wa mitandao/skimu za umwagiliaji; hivyo kuhatarisha mafanikio ya malengo ya mradi.

**Ninapendekeza kwamba ripoti za usanifu zibainishe muda wa ukomo wa matumizi ya mradi. Pia, zijumuishe usanifu wa barabara za mashambani kwa ajili ya skimu za umwagiliaji kwa kufuata taratibu na viwango bora vya usanifu wa mradi.**

#### **12.4 Kiwango duni cha uimara wa zege**

Kifungu cha 3 (309) cha mahitaji ya mkataba uliopitishwa kwa ajili ya utekelezaji wa mabwawa ya umwagiliaji kinataka kiwango cha chini cha uimara wa zege kuwa ni  $25 \text{ N/mm}^2$  ambacho kinatakiwa kufikiwa katika siku 28 toka kumwangwa kwa zege hilo.

Matokeo ya vipimo vya zege vilivyofanyika wakati wa ukaguzi kwa kuhusisha Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) na AES Material Lab kwenye skimu za umwagiliaji za Mkombozi na Magulukenda - Sukuma, mwezi Oktoba 2023,

yalioneshwa kuwa sehemu 4 kati ya 17, sawa na asilimia 24, hazikukidhi viwango vya uimara wa zege. Matokeo hayo yameoneshwa atika Jedwali 32.

**Jedwali 32: Vipimo vya zege kwa mradi wa Magulukenda -Sukuma na Mkombozi Skimu**

Sehemu ya mradi/Jina la Mradi	Kilichopimwa	Kiwango kilichowekwa (N/mm <sup>2</sup> )	Kiwango kadiri ya Usanifu (N/mm <sup>2</sup> )	Kipimo halisi	Maoni
				(N/mm <sup>2</sup> )	
Skimu ya umwagiliaji ya Magulukenda - Sukuma	Daraja kwa ajili ya mifugo	25	25	21	Halijakidhi kiwango
	Daraja la watembea kwa miguu	25	25	22	Halijakidhi kiwango
Skimu ya Umwagiliaji ya Mkombozi	Msingi wa zege (Mtiririko wa chini)	25	25	24	Halijakidhi kiwango
	Mfereji mdogo Na. 01	25	25	23	Halijakidhi kiwango

*Chanzo: Matokeo ya majaribio ya zege yaliyofanywa na TANROADS na AES Material Lab, 2023*

Hali hii ilichangiwa na kutokuwapo kwa udhibiti wa ubora na uhakiki wa ubora kipindi cha ujenzi. Ilibainika zaidi kuwa hapakuwa na mwongozo wa kuonesha jinsi kazi madhubuti zinavyopaswa kufanywa. Hii ilisababisha udhaifu katika ubora wa ujenzi, na kuibua wasiwasi juu ya uimara na usalama wa miundombinu hiyo.

Ninapendekeza kwamba NIRC itekeleze hatua thabiti za kudhibiti ubora; na ipate taarifa za kina kuhusu mbinu za kuhakikisha kazi ya ujenzi wa skimu inakuwa imara na yenye ubora ili kuzuia udhaifu unaoweza kutokea katika ubora wa ujenzi. Pia, ihakikishe uimara na usalama wa muda mrefu wa miundombinu.

### 12.5 Upungufu katika ushindiliaji wa udongo na uhakikisho wa ubora

Kifungu cha 7 (705) cha maelezo ya mkataba kilichokubaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa mabwawa ya umwagiliaji kinasisitiza kuwa malighafi zote za ujenzi lazima zishindiliwe hadi 95% ya kiwango cha juu zaidi cha msongamano mkavu.

Ukaguzi wa ujenzi katika skimu za umwagiliaji za Mkombozi na Magulukenda - Sukuma ulibaini kuwa, katika baadhi ya sehemu muhimu za miundombinu ya umwagiliaji, udongo ulishindiliwa kwa kiwango kilichokuwa chini ya viwango vilivyowekwa. Matokeo ya vipimo vya viwango yaliyofanywa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji yameoneshwa katika Jedwali 33.

**Jedwali 33: Matokeo ya ushindiliwaji wa udongo katika skimu ya umwagiliaji ya mkombozi**

Sehemu	Ubora unao takiwa (%)	Matokeo (%)	Matokeo
Kuweka kifusi katika mfereji wa TC 5 - SC 22	95	83.8	Haujakidhi kiwango
Mfereji namba 16 - Barabara ya changalawe	95	93.3	Haujakidhi kiwango
Mfereji namba 12 - uwekaji wa kifusi kwenye mfereji	95	97.0	Umekidhi kiwango
Mfereji namba 8 - kwenye barabara ya vumbi	95	95.3	Umekidhi kiwango
Sehemu za juu za zinazowekwa kifusi kwenye mfereji namba 16	95	89.6	Haujakidhi kiwango

**Chanzo:** Uchambuzi wa matokeo ya majaribio, 2023

Hii inaonesha kuwa kulikuwa na viwango tofauti katika kufikia ubora wa kushindiliwa kwa udongo katika maeneo tofauti ndani ya Skimu ya Umwagiliaji ya Mkombozi. Kati ya sehemu tano za sampuli zilizochukuliwa, tatu hazikukidhi ubora unaotakiwa, na mbili zilikidhi.

**Jedwali 34: Matokeo ya majaribio ya kushindilia udongo katika skimu ya umwagiliaji ya Magulukenda - Sukuma**

Sehemu inayofanyiwa jaribio	Ubora unaotakiwa (%)	Matokeo (%)	Matokeo
Sehemu Na. 1	95	93.8	Haujakidhi kiwango
Sehemu Na. 2	95	99.8	Umekidhi kiwango
Sehemu Na. 3	95	95.9	Umekidhi kiwango

**Chanzo:** Uchambuzi wa matokeo ya majaribio, 2023

Ukiukaji huu ulihusishwa na kukosekana kwa uhakiki wa ubora wa kutosha na usimamizi wa ujenzi. Hii inaashiria hatari katika uimara wa miundombinu ya umwagiliaji, yakiwamo matuta katika mabwawa. Upungufu katika ushindiliaji unafanya udongo kutokuwa na ugumu wa kutosha, hivyo kushindwa kuwa na uwezo wa kuhimili mzigo. Hali hii inaweza kusababisha kubomoka kwa miundombinu.

Ninapendekeza kuwa uongozi wa NIRC uboreshe usimamizi wa miradi ili kuhakikisha ushindiliaji wa udongo katika ujenzi wa barabara ndani skimu unafikia 95% ya kiwango cha juu cha ushindiliaji wa udongo.

## 12.6 Mapungufu katika usimamizi wa muda wa mradi ya umwagiliaji

Kanuni ya 5(2)(c) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kinataka taasisi nunuzi kuhakikisha kwamba kazi zinakamilika kwa wakati kulingana na vipaumbele vya taasisi nunuzi.

Ukaguzi ulibaini usimamizi duni wa muda katika miradi yote ya umwagiliaji iliyokaguliwa, huku maendeleo ya miradi yakiwa nyuma ya muda uliopangwa, kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali 35**.

**Jedwali 35: Asilimia ya maendeleo ya kazi za miradi na hali ya kifedha dhidi ya muda uliopita**

Jina la Skimu ya umwagiliaji	Hatua ya ujenzi wa mradi (%)	Fedha zilizotumika (%)	Muda uliotumika (%)	Pengo la Hatua ya Utekelezaji lililopo (%)
Eyasi	8	15	29	21
Lyamalagwa	6	15	25	19
Magulukenda - Sukuma	86	51	106	20
Mkombozi Kipande cha I	57	28	72	15
Mkombozi Kipande cha II	31	15	72	41
Mkombozi Kipande cha III	30	15	72	42
Mkombozi Kipande cha IV	44	15	72	28

**Chanzo:** Uchambuzi wa wakaguzi, 2023

Maendeleo ya miradi katika mabwawa yote ya umwagiliaji yalikuwa chini ya muda uliotakiwa kukamilika, huku Mkombozi Kipande cha III na Mkombozi kipande cha I zikiwa ziliongoza kuchelewa kwa asilimia 42 na 15 mtawalia. Hii ilitokana na kucheleweshwa kwa malipo ya awali kwa wakandarasi, kuchelewa kuanza kwa kazi, pamoja na uidhinishaji wa mabadiliko ya kazi. Kuchelewa huku kutaathiri huduma za umwagiliaji kwa wanufaika wa miradi hiyo. Kwa hiyo, ucheleweshaji wa kukamilika kwa miradi unaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama, migogoro ya kimkataba, na changamoto katika kufikia malengo ya jumla ya mradi. Pia, ucheleweshaji wa mradi, unawaathiri moja kwa moja watumiaji wa mwisho wa mradi huo.

**Napendekeza NIRC ihakikishe utekelezaji wa mradi unaendana na ratiba iliyopangwa ili kuondoa ucheleweshaji.**

### 12.7 Ujenzi na usimamizi duni wa barabara za mashambani

Kifungu cha 6.2.5 cha Mwongozo wa Usanifu na Malighafi za Barabara wa Wizara ya Ujenzi wa mwaka 1999 kinataka malighafi za udongo zinazotumika baada ya kuondoa tabaka bovu ziwe zile zitakazokidhi ubora; pia udongo unaotakiwa uwe wenye asilimia 15 ya kiwango cha plastiki (*Plasticity Index [PI]*), yaani uwezo wa udongo wa kubadilika umbo kama plastiki bila kupata mipasuko) ambao utatolewa sehemu ya nyingine karibu na eneo la mradi.

Nilibaini barabara za mashambani ndani ya miradi ya umwagiliaji ya Mkombozi III na Magulukenda - Sukuma zilijengwa kwenye udongo dhaifu wa mfinyanzi.

Hii ni kwa sababu udongo wa sehemu hiyo ambao unasinyaa na kutanuka (mfinyanzi) haukuondolewa kabla ya kuweka udongo mwingine juu yake kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo 6**.

### Kielelezo 6: Barabara ya shambani iliyojengwa juu ya udongo dhaifu



**Chanzo:** Picha ilipigwa katika skimu ya umwagiliaji ya Mkombozi tarehe 24 Oktoba 2023

Vilevile, barabara za Magulukenda - Sukuma zilijengwa bila kuzingatia sehemu ya kuondoa maji barabarani kwenda kwenye mifereji ya pembeni. Kwa hiyo, ujenzi wa barabara bila kubadilisha udongo dhaifu wa mfinyanzi, pamoja na kutokuwapo kwa sehemu za kuondoa maji barabarani kulisababisha barabara kuhabika mapema, kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo 7**.

Hali hii inaweza kufanya barabara kutopitika, hasa nyakati za mvua; hivyo kusababisha changamoto katika usafirishaji wa mazao ya shambani kwenda kwenye masoko.

**Kielelezo 7: Kuharibika kwa Barabara ya Magulukenda - Sukuma**

**Chanzo: Picha ilipigwa katika Bwawa la Sukuma tarehe 27 Oktoba 2023**

Usimamizi duni wa mradi ulichangia kuwapo kwa kasoro hizo. Hii inatokana na kwamba wasimamizi wa mradi kutokuwapo katika eneno la mradi katika kipindi chote cha ujenzi.

**Ninapendekeza Tume ya Umwagiliaji ihakikishe yafuatayo: kiwango bora cha barabara kinafikiwa kwa ufuatiliaji wa kazi zilizofanyika; barabara zishindiliwe hadi kufikia 95% ya msongamano wa juu; kulinganisha utekelezaji wa miradi na muda uliopangwa ili kuondoa ucheleweshaji wa mradi; kuzingatia vipimo vya ujenzi wa barabara, hasa katika maeneo yenye changamoto, kwa kuhusisha wataalamu; na kuimarisha usimamizi wa miradi ili kuhakikisha ubora wa miundombinu unafikiwa.**

# SURA YA KUMI NA TATU

## UKAGUZI WA KIUFUNDI KUHUSU USIMAMIZI WA UBORA WA MAJI KWA MATUMIZI YA NYUMBANI



### 13.1 Utangulizi

Dhumuni la langu la ukaguzi wa kiufundi kuhusu usimamizi wa ubora wa maji kwa matumizi ya nyumbani. lilikuwa ni kutathmini kama Wizara ya Maji inahakikisha vya kutosha kuwa usambazaji wa maji kwa matumizi ya nyumbani unakidhi viwango vya ubora wa maji vilivyowekwa. Ukaguzi huu unahusisha miaka mitatu ya fedha (2020/21, 2021/22 na 2022/23). Ukaguzi ulifanyika katika mamlaka za maji za miji minane (8) ambayo ni Lindi, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Mbeya, Dodoma, Kigoma, Mwanza na Singida. Zifuatazo ni kasoro kubwa zilizobainika:

### 13.2 Programu duni ya ufuatiliaji wa ubora wa maji katika mamlaka za maji (UWSSAs)

Kifungu cha 5 cha Mwongozo wa Ufuatiliaji Ubora wa Maji na Majitaka wa EWURA wa mwaka 2020 kinataka kila mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira kuanzisha programu ya ufuatiliaji wa ubora wa maji ya matumizi ya nyumbani mara kwa mara. Programu ilipaswa kufafanua mpango wa ufuatiliaji wa utendaji kazi wake, ratiba ya kuweka dawa (kutibu maji), vigezo vya upimaji wa ubora wa maji, na vigezo vya uwekaji sampuli kulingana na mwongozo wa EWURA.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa ingawa mamlaka za maji zilitengeneza programu ya kufuatilia ubora wa maji, programu hizizilikuwa na kasoro. Hii ilitokana na kutokuzingatia kikamilifu miongozo ya EWURA; hivyo kusababisha kutokuwa na vipengele vya ufuatiliaji wa utendaji kazi. Licha ya kufanya ufuatiliaji wa kiutendaji, bajeti ya kipengele hiki haikujumuishwa katika mpango wao wa kufuatilia ubora wa maji (WQMP).

Ukaguzi ulibaini kuwa programu zilizoandaliwa na mamlaka ya maji jijini Mwanza (MWAUWASA) hazikuwa na ramani ya usambazaji wa maji katika sehemu husika na kipengele cha ufuatiliaji wa utendaji kazi. Pia, Mamlaka ya Usambazaji Maji safi na majitaka Jijini Dodoma (DUWASA) ilikosa ufuatiliaji wa kiutendaji na ramani ya usambazaji maji. Kadhalika, LUWASA haikuwa na



## Ukaguzi Wa Kiufundi Kuhusu Usimamizi Wa Ubora Wa Maji Kwa Matumizi Ya Nyumbani

ramani inayoonesha sehemu za kuchukua sampuli za maji. KUWASA haikuwa na mpango wa ufuatiliaji wa utendaji kazi. Mipango ya MUWSA na SUWASA haikufuata miongozo ya EWURA kwa kutobainisha sehemu za kuchukua sampuli kwa ajili ya kupima ubora wa maji. Hivyo basi, kulikuwa na hatari kubwa kwa sehemu kubwa ya mitandao kutochukuliwa sampuli.

Programu ya DAWASA ilifuata miongozo ya EWURA. Hata hivyo, haikuzingatia sehemu za kuchukua sampuli kutoka kwa visima binafsi wala vihatarishi vya uchafuzi wa mazingira. Aidha, vipengele vya ufuatiliaji wa utendaji vilikosekana. Kwa Mbeya, mpango wa UWSA ulitegemea tu vigezo vya idadi ya watu; haukuzingatia athari za uchafuzi wa mazingira wala mpango wa ufuatiliaji wa uendeshaji wake. Kwa ujumla, matokeo haya yanaonesha upungufu katika ufuatiliaji wa ubora wa maji katika mamlaka mbalimbali za maji; hivyo kuibua wasiwasi kuhusu ufanisi wa UWSSA katika kuhakikisha maji safi na salama kwa umma.

**Ninapendekeza yafuatayo kwa Wizara ya Maji: ihakikishe mamlaka za maji zinafanya ufuatiliaji wa ubora wa maji kwa matumizi ya nyumbani kwa kuzingatia programu zilizoandaliwa kutokana na miongozo ya EWURA; na ihakikishe kuwa vigezo vyote vya ufuatiliaji wa ubora wa maji vilivyopangwa vinazingatiwa kikamilifu katika utendaji kazi wa Mamlaka za Maji.**

### **13.3 Mamlaka za Maji saba kati ya nane hazikuwa na taratibu nzuri za utendaji katika kukusanya, kutunza na kuhifadhi sampuli zinazotumika kutathmini ubora wa maji**

Kifungu cha 2.1.2 cha kiambatisho Na. 1 cha Mwongozo wa EWURA wa mwaka 2020 kinaitaka mamlaka za maji kuandaa taratibu za uendeshaji mzuri wa kutathmini ubora wa maji, hususani kwa kuchangua sampuli, kukusanya, utunzaji na uhifadhi wa sampuli hizo.

Kati ya mamlaka za maji safi na majitaka nane (8) zilizofanyiwa tathmini, saba (7) zilikosa utaratibu stahiki za uendeshaji wa tathmini ya ubora wa maji, yaani ukusanyaji, utunzaji, na uhifadhi wa sampuli zitumikazo kutathmini ubora wa maji. Mamlaka hizo ni LUWASA, DAWASA, MWAUWASA, KUWASA, DUWASA, SUWASA, na Mbeya UWSA. Ukaguzi ulibaini kuwa MUWSA pekee ndiyo ilikuwa na utaratibu wa uendeshaji mzuri wa kupata sampuli kwa kina pamoja na ukusanyaji, utunzaji, na uhifadhi wa sampuli.

Ukaguzi pia ulibaini kuwa, licha ya kukosa utaratibu wa utendaji wa kutunza na kuhifadhi sampuli, DAWASA ilikuwa na utaratibu kwa ajili ya usimamizi wa usafi wa mazingira. MWAUWASA ilitegemea taratibu za mifumo ya usimamizi wa

ubora katika shughuli mbalimbali. Kwa ujumla, kutokuwapo kwa utaratibu wa utendaji wa kuhifadhi, kutunza na kukusanya sampuli za kupima ubora wa maji kunatia shaka juu ya upimaji wa usalama na ubora wa maji uliofanywa na mamlaka hizi.

**Ninapendekeza kwa Wizara ya Maji kuhakikisha kwamba Mamlaka zote za Maji zote zinatengeneza na kutekeleza taratibu za uendeshaji wa shughuli za kupima usalama na ubora wa maji , uwekaji wa kemikali, njia sahihi za kupata sampuli, taratibu za utunzaji na uhifadhi ili kuhakikisha uthabiti, usahihi na uzingatiaji wa viwango vinavyotambulika kwenye usalama na ubora wa maji kwa matumizi ya nyumbani.**

### 13.4 Kutofuata ipasavyo taratibu za upimaji wa maji katika maabara kupitia tathmini ya sampuli za maji

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4.1.2.4 cha Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Utoaji Taarifa za Ubora wa Maji ya Kunywa wa mwaka 2018, ni sharti kila mamlaka iwe na maabara yake ambayo itakuwa na mahitaji yote muhimu ya kupima na kuchambua sampuli za maji. Mahitaji haya ni pamoja na kuwa na idadi ya kutosha ya wafanyakazi ili kuweza kuchukua sampuli, kupima, na kuripoti matokeo. Aidha, kuhakikisha kuwa wale wanaofanya kazi kwenye maabara wana vifaa vya kinga. Aidha, miongozo inaeleza kuwa maabara inatakiwa kuwa na vifaa vyote muhimu na kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara.

Ukaguzi wangu kuhusu mbinu za kupima ubora wa maji kwa mamlaka mbalimbali za usambazaji maji nchini Tanzania ulibaini upungufu kadhaa.

Nilibaini kuwa DUWASA haikufuata ipasavyo taratibu za kimaabara, wafanyakazi hawakufuata tahadhari za usalama na hawakuwa na vifaa vya kinga binafsi. Uhaba wa watumishi na vitendea kazi katika mitambo ya kusafisha maji kwa Mzakwe ulichangia kutokidhi taratibu. SUWASA haikuwa na maabara yake; ilitegemea vifaa kutoka maeneo mengine. Hivyo, kusababisha kushindwa kufanya ufuatiliaji wa uendeshaji kuhusu ubora wa maji.

MWAUWASA ilijumuisha mbinu zilizopendekezwa katika mipango yake, zikiwamo taratibu za mifumo ya usimamizi wa ubora wa shughuli mbalimbali. LUWASA haikufanya upimaji wa sampuli ya maji katika mamlaka hiyo kwa kuwa hapakuwa na maabara ya ubora wa maji. Pia, haikuwa na taratibu za kufanya tathmini ya ubora na usalama wa maji na uchunguzi wa bakteria katika maji.



## Ukaguzi Wa Kiufundi Kuhusu Usimamizi Wa Ubora Wa Maji Kwa Matumizi Ya Nyumbani

Licha ya kuwa na taratibu za uendeshaji wa ubora wa maji zilizopo, Mamlaka ya Maji ya Moshi ilishindwa kuzingatia taratibu hizo. Aidha, wafanyakazi wa mamlaka hiyo hawakuwa na vifaa vya kujikinga. Zaidi, mamlaka hiyo ilikuwa inatumia vifaa vya kupima maji ambavyo havijafanyiwa marekebisho ya usomaji matokeo ya vipimo kwa usahihi.

KUWASA haikuwa na maabara yake, na ilitegemea vifaa kutoka sehemu nyingine. Hali hiyo iliyosababisha upungufu katika kufanya vipimo vya ubora wa maji. DAWASA ilitumia mbinu zilizopendekezwa; hata hivyo, ilikosa utaratibu wa ufanyaji wa vipimo kwa vile wafanyakazi wake hawakutumia vifaa vya kujikinga wakati wa shughuli ya kupima maji na walikosa tahadhari za usalama wao wakiwa kazini.

Hivyo, matokeo haya yanaleta wasiwasi kuhusu usahihi na kuaminika kwa upimaji wa ubora wa maji unaofanywa na mamlaka hizi.

**Ninapendekeza Wizara ya Maji ihakikishe kuwa Mamlaka zote za Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (UWSSA) zinaboresha programu zao za ufuatiliaji ubora wa maji ili kuendana kwa karibu zaidi na miongozo ya EWURA. Pia, ihakikishe kunakuwa na mifumo ya ufuatiliaji wa kina na yenye usahihi ili kuimarisha ubora wa maji na afya ya watumiaji.**

### **13.5 Uchukuaji wa sampuli na upimaji usiojitosheleza katika mamlaka za maji**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 3.3 cha Mwongozo wa ufuatiliaji wa ubora wa maji wa EWURA kwa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira (2020), uchukuaji wa mara kwa mara wa sampuli za maji zinazofanyiwa vipimo unapaswa kuzingatia mahitaji na Viwango vya Tanzania vya ubora wa Maji ya kunywa (*Tanzania standard 789*). Bila kujali idadi ya watu, aina zote za maji zinapaswa kupimwa angalau mara mbili kwa mwaka—mara moja kipindi cha kiangazi na mara nyingine katika kipindi cha masika.

Tathmini ya programu za kufuatilia ubora wa maji kwa mamlaka mbalimbali za usambazaji maji inaonesha upungufu. Linapokuja suala la ufuatwaji wa programu za kufuatilia ubora wa maji kwa mamlaka mbalimbali za usambazaji wa maji uchukuaji wa sampuli na upimaji wa maji, DUWASA, DAWASA, MWAUWASA, Mbeya - UWSA, MUWSA, KUWASA, LUWASA, na SUWASA hazijakidhi vigezo.



## Ukaguzi Wa Kiufundi Kuhusu Usimamizi Wa Ubora Wa Maji Kwa Matumizi Ya Nyumbani

Mbeya - UWSA pekee ndiyo iliyoonesha kufuata vigezo vilivyowekwa, ikiwamo kuchukua sampuli kabla na baada ya tangi la kuhifadhi, huku mamlaka nyingine hazikufanya hivyo. Mamlaka nne kati ya nane zilizokaguliwa zilifuata vigezo vya kuchukua sampuli katika mtandao wa usambazaji maji. Mamlaka hizo ni DUWASA, MWAUWASA, Mbeya-UWSA, na MUWSA

Ingawa mamlaka hizi kwa ujumla zilizingatia kigezo cha idadi ya watu katika kupima maji, kulikuwa na tofauti katika mgawanyo wa maeneo ya kuchukua sampuli katika mtandao wa mabomba. DUWASA ndiyo mamlaka pekee iliyokidhi kigezo hiki, huku DAWASA, MWAUWASA, Mbeya - UWSA, MUWSA, KUWASA, LUWASA na SUWASA zikiwa hazikukidhi matakwa ya Mwongozo.

**Ninapendekeza Wizara ya Maji ihakikishe kuwa Mamlaka zote za Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (UWSSA) zinaboresha programu zao za ufuatiliaji ubora wa maji ili kuendana kwa karibu zaidi na miongozo. Pia, kuhakikisha kuna mifumo ya ufuatiliaji wa kina na sahihi wa ubora wa maji kwa ajili ya usalama wa afya za watumiaji.**

### 13.6 Kutozingatia mahitaji ya kiwango cha mabaki ya klorini kwenye maji

Mwongozo wa EWURA wa Ufuatiliaji Ubora wa Maji na Majitaka kwa Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira, Toleo la Pili la mwaka 2020, unataka maji yaliyosafishwa kuwa na kiasi cha mabaki ya klorini kati ya 0.2 mg/L na 0.5 mg/L.

Tathmini ya kiwango cha mabaki ya klorini katika mamlaka za maji zilizotembelewa kwa mujibu wa mapitio ya ripoti za ufuatiliaji wa ubora wa maji kwa mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2022/23 ulionesha idadi ya sampuli ambazo hazikukidhi kiwango kinachohitajika cha mabaki ya klorini kati ya jumla ya sampuli zilizokusanywa na kupimwa.

Uchambuzi wangu ulibaini kuwa, mbali na MUWSA, mamlaka nyingine hazikuwa zikifanya vizuri. Mamlaka saba kati ya nane za maji zilizokaguliwa, hazikuzingatia mahitaji ya kiwango cha mabaki ya klorini katika maji.

KUWASA ilikuwa na kiwango cha juu zaidi cha kutokidhi kiwango hicho kwa 65%, wakati DUWASA ilikuwa na kiwango cha chini cha kutokidhi cha 7%. Mwaka 2020/21, MWAUWASA ilikuwa na kiwango cha juu zaidi cha kutokidhi kiwango hicho kwa 58%, Mbeya - UWSSA ilikuwa na kiwango cha chini cha kutokidhi cha 17%. Mwaka 2022/23, DAWASA ilikuwa na kiwango cha juu zaidi cha kutokidhi cha 48% na KUWASA ilikuwa na kiwango cha chini cha kutokidhi cha 24%.

Kwa kuzingatia hatari zinazohusiana na kutozingatia kiasi cha mabaki ya klorini kwenye maji, DAWASA ilifanya vibaya zaidi kwa 2022/23, huku MWAUWASA ilifanya vibaya zaidi kwa mwaka 2021/22. Hii ni kwa kuwa walikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu walio katika hatari ya kutumia maji yaliyowekwa klorini kinyume na taratibu.

**Ninapendekeza Wizara ya Maji iweke taratibu za kuhakikisha kuwa vifaa vya ufuatiliaji wa ubora wa maji vinavyotumiwa na mamlaka za maji vinafanya kazi ipasavyo ili kutoa matokeo ya uhakika ya ubora wa maji.**

### 13.7 Upungufu wa nguvu za kikemikali zinazotumika kutibu maji katika mamlaka za maji zilizokaguliwa

Kanuni ya 56(1) na (2) ya Kanuni za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira (Leseni na Ubona wa Huduma) za mwaka 2020 inataka mamlaka za maji zilizopewa leseni ya kutoa huduma ya maji kuhakikisha kuwa kemikali za kusafisha maji zinapimwa na kuthibitishwa na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali au wakala aliyeidhinishwa kwa mujibu wa masharti ya sheria zinazotumika. Leseni inataka kuwe na rekodi sahihi za kemikali zilizotumika kusafisha maji na uidhinishaji wa matumizi ya kemikali hizo.

Ukaguzi ulibaini mamlaka za maji saba kati ya nane zilizokaguliwa zilikuwa na kemikali za “*Calcium hypochlorite*” zenye nguvu kidogo; hivyo kuhatarisha ufanisi wa kuu viini vya vijidudu katika maji. Uchambuzi wa ripoti za ufuatiliaji wa operesheni kwa miaka ya fedha 2020/21 hadi 2022/23 ulibaini kuwa, mbali na MUWSA, 88 mamlaka za maji zilizosalia (88%) hazikuzingatia mahitaji ya kiwango cha mabaki ya klorini kisichotakiwa kubaki kwenye maji. KUWASA ilikuwa na kiwango cha juu zaidi cha kutokidhi mwaka 2020/21, wakati MWAUWASA ilikuwa na kiwango cha juu zaidi cha kutokidhi kwa mwaka 2021/22 na DAWASA ilikuwa na kiwango cha juu zaidi cha kutokidhi mwaka 2022/23.

**Ninapendekeza Wizara ya Maji ihakikishe kila mamlaka ya maji inahakiki ubora wa kemikali zinazotumika kutibu maji kabla ya kutumika ili kuhakikisha dozi inafanyika kwa kuzingatia ubora wa kemikali hizo zilizounuliwa.**

### 13.8 Utendaji duni wa Mtambo wa Kusafisha Maji kwa MWAUWASA

Ukaguzi ulibaini kuwa shughuli za kusafisha maji hazikukidhi mwongozo namba 789 wa Shirika la Viwango la Tanzania, yaani kiwango cha chini na juu ni 0.2mg/lita - 0.5 mg/lita, mtawalia. Ukaguzi ulipitia matokeo ya vipimo vilivyofanywa na MWAUWASA. Ulibaini kuwa asilimia 12.6 ya sampuli za matokeo ya vipimo hivyo vya MWAUWASA yalikuwa juu ya kiwango

kinachotakiwa cha klorini kwa 0.5mg/lita. Aidha, asilimia 36.33 ilikuwa chini ya kiwango kinachohitajika cha 0.2 mg/lita.

Pia masuala muhimu yaliyobainishwa wakati wa ukaguzi katika mtambo wa kusafisha maji wa Magu ni pamoja na kuharibika kwa sehemu ya kuchuja na kukausha tope kutokana na mtambo huo kufunikwa na maji kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 8** ambayo imeonesha kufunikwa kwa mtambo huo. Chujio lipo chini ya maji, hivyo kushindwa kuchuja kwa usahihi. Kina cha maji katika Ziwa Victoria kiliongezeka na kufikia mita 13.42 mnamo Mei 2020, hivyo kusababisha hali hii. Kwa hiyo, chujio la tope linakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa nafasi ya kuchuja na kukausha tope hilo kwa usahihi. Hali hii inasababisha tishio kwa ufanisi wa usafishaji wa maji hayo. Kuna uwezekano wa tope kumwagwa moja kwa moja ziwani bila ya kukaushwa, hivyo kusababisha uharibifu wa mazingira.

Aidha, umwagwaji wa tope katika ziwa hilo unamaanisha ubora wa maji yanayoingia kwa ajili ya kusafishwa ni hatari zaidi na kufanya iwe gharama zaidi kuyasafisha maji hayo. **Kielelezo 8** inaonesha matope yaliyojaa kwenye mtambo wa kusafisha maji wa Magu.

### **Kielelezo 8: Matope yaliyofurika kwenye mtambo wa kusafisha maji wa Magu**



*Chanzo: Picha ilipigwa uwandani na wakaguzi tarehe 23/10/2023*

Ninapendekeza Wizara ya Maji ihakikishe mamlaka zote za maji zinakuwa na matangi ya klorini kwenye mtambo wa kutibu na kusafisha maji ili kuhakikisha uwekaji wa kutosha wa klorini. Pia, ziwe na miundombinu ya kupima ubora wa maji yanayoingia kwenye mtambo wa kutibu na kutoka eneo la kuwekea dawa. Zaidi, zitie taarifa ubora wa maji kabla na baada ya matibabu.



### **13.9 Utendaji duni wa kifaa cha kuondoa taka katika Mamlaka ya Maji ya DAWASA**

Kulingana na Mwongozo wa Usanifu, Usimamizi wa Ujenzi, Uendeshaji na Matengenezo (DCOM) wa mwaka 2020, mitambo ya kusafisha maji lazima iwe na kifaa cha kuondoa taka kinachofanya kazi vizuri ili kusaidia katika uondoaji mzuri wa taka wakati wa mchakato wa kusafisha maji.

Ilibainika kuwa vifaa vya kuondoa taka kwenye mtambo wa Wami havifanyi kazi ipasavyo kwa sababu vilikuwa chakavu. Hii inapunguza ufanisi wa usafishaji maji na uzalishaji wa maji kwa wakati kwa sababu kuna nyakati ambapo kifaa kimoja kinasimamishwa kufanya kazi ili kuruhusu kisafishwe kwanza chenyewe.

**Ninapendekeza Wizara ya Maji ihakikishe ratiba za uendeshaji na matengenezo ya mara kwa mara ya vifaa na mitambo ya kutibu na kusafisha maji yanaandaliwa, kuwekewa bajeti ya kutosha ya matengenezo, na kutekelezwa kwa kuzingatia hatua za kulinda vifaa hivyo. Pia, ihakikishe mifumo ya usambazaji maji inafanya kazi ipasavyo na maji yanayozalishwa kwa matumizi ya nyumbani yanakidhi viwango vya ubora.**

# SURA YA KUMI NA NNE

## UKAGUZI WA KIUFUNDI KUHUSU UJENZI WA MIRADI YA BARABARA



### 14.1 Utangulizi

Sura hii inahusu udhibiti wa gharama katika ujenzi wa barabara. Lengo lilikuwa ni kubainisha sababu zinazopelekea kuongezeka kwa gharama, kuhakiki usahihi na uhalali wa gharama, kuibua mapungufu katika mifumo ya utekelezaji miradi na kutoa mapendekezo ya kiboresha uandaji wa bajeti, mipango and mifumo ya kudhibiti gharama. Ukaguzi unajumuisha miradi kumi ya barabara, mitano ikitekelezwa na TANROADS na mitano mingine ikitekelezwa na TARURA. Hii inajumuisha miradi ya ujenzi iliyokamilika na inayokaribia kukamilika kwa miaka sita ya fedha kuanzia 2016/17 hadi 2021/22. Mapitio yangu ya miradi ya barabara yalibaini mapungufu makubwa kama ifuatavyo:

### 14.2 Upangaji na Usanifu

#### 14.2.1 Upembuzi yakinifu na usanifu duni ulisababisha kuongezeka kwa gharama kiasi cha Sh. bilioni 64.78

Aya ya 3.3 ya Mwongozo wa Usanifu wa Kijiometri wa Barabara wa Wizara ya Ujenzi (2011) kinamtaka msanifu kuzingatia kwa makini masuala mbalimbali ambayo yanaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa matokeo ya usanifu katika kupanga na kutathmini miradi ya barabara. Mwongozo unasema zaidi kwamba usanifu, ujenzi na matengenezo ya barabara huathiriwa sana na aina ya eneo ambalo barabara inapita. Pia, tofauti za jiolojia na mteremko huathiri sana usanifu wa barabara.

Mapitio ya ripoti za usanifu wa miradi 10 yalibaini mabadiliko makubwa wakati wa utekelezaji wa miradi, hivyo kusababisha ongezeko la kazi. Hii ilisababishwa na:

- Upembuzi yakinifu haukuonesha ipasavyo hali halisi za eneo ambalo barabara itajengwa kama vile topografia, hali ya udongo, na hali ya maji. Ukaguzi ulibaini kuwa mabadiliko makubwa wakati wa utekelezaji wa mradi yalisababishwa na upembuzi yakinifu usiotosheleza, hivyo kuongeza wigo wa ongezeko la kazi. Katika mradi wa barabara ya Kidatu - Ifakara, ilibainika kuwa kulikuwa na ongezeko la nguzo 10 kwenye ujenzi wa daraja kutokana

na kutofanyika kwa uchunguzi wa kutosha wa matabaka ya udongo. Vilevile, ilisababishwa na kutofanyika kwa uchunguzi wa kutosha wa udongo, gharama za kusafisha eneo la mradi, kuchimbua na kuondoa tabaka bovu la udongo ziliongezeka.

- Miradi ya barabara iliathiriwa na ongezeko la gharama wakati wa utekelezaji kutokana na kutorekebisha kwa dosari katika usanifu wa awali kabla ya kusaini mkataba. Ukaguzi ulipitia taarifa za usanifu wa mradi wa barabara ya Kikusya - Matema na kubaini kuwa usanifu huo ulifanyiwa marekebisho na Timu ya Usimamizi (M/s TECU) wakati wa utekelezaji wa mradi. Ulibainika upungufu mkubwa katika usanifu wa awali, hususani katika usanifu wa mifereji ya maji. Upungufu huo ulibainika kutokana na mvua kubwa iliyonesha mwezi Aprili 2016 na kusababisha mafuriko makubwa na kufunika barabara. Hali hiyo ilisababishwa na kutofanyika kwa utafiti wa kutosha wa hali ya maji na hali ya mwinuko wa ardhi katika usanifu wa mradi huo.
- Mapitio yangu yalibaini ongezeko la gharama katika ujenzi wa barabara mbili, Kikusya-Matema na Mpemba-Isongole lililosababishwa na utayarishaji usiofaa wa gharama za makadirio ya ujenzi wa mradi: Hali hiyo ilisababishwa na mkanganyiko wa lami aina ya AC14 na lami aima ya 35/50 moja kuwekwa kwenye mahitaji ya viwango na nyingine gharama za makadirio ya ujenzi kuwa zitumike na kuleta mkanganyiko. Pia, usimamizi wa ubora usiojitosheleza katika mapitio ya ukokotoaji wa makadirio ya gharama za ujenzi wa mradi na uelewa wa viwango vinavyo hitajika. Mapungufu haya yalibainishwa wakati wa utekelezaji, hivyo kupotosha mamlaka za kutoa vibali kwa viwango vya mahitaji ambayo siyo sahihi kwa mradi.

Ongezeko la Gharama lililotokana na upembuzi yakinifu, usanifu na mapitio ya makadirio ya ya gharama usiotosheleza yameoneshwa katika **Jedwali 36**.

**Jedwali 36: Ongezeko la gharama kutokana na mapungufu ya upembuzi yakinifu na usanifu**

Jina la mradi	Kasoro zilizosababisha ongezeko la gharama (Sh. Biloni)			Jumla (Sh. Biloni)
	Ukosefu wa taarifa muhimu za eneo la mradi	Upungufu wa Usanifu wa awali	Kasoro za uandaaji wa makadirio	
<b>Barabara nne na daraja moja chini ya utekelezaji wa TANROADS</b>				
Mikumi - Kidatu	5190	10,490	0.00	15,680
Kikusya - Matema	0.00	7,150	2,200	9,350
Mpemba - Isongole	4,470	1,080	3,490	9,040
Wami Bridge	690	0.00	0.00	690
Maswa - Mwigumbi	9,410	800	760	10,210
<b>Jumla Ndogo</b>	<b>19,760</b>	<b>18,720</b>	<b>6,450</b>	<b>44,970</b>
<b>Barabara tano chini ya utekelezaji wa TARURA</b>				
Government City	15,110	3,600	0.00	18,710
Mkwajuni Road	0.00	1,140	0.00	1,140
<b>Jumla ndogo</b>	<b>15,110</b>	<b>4,740</b>	<b>0.0</b>	<b>19,850</b>

Jina la mradi	Kasoro zilizosababisha ongezeko la gharama (Sh. Bilioni)			Jumla (Sh. Bilioni)
	Ukosefu wa taarifa muhimu za eneo la mradi	Upungufu wa Usanifu wa awali	Kasoro za uandaaji wa makadirio	
Jumla	34,870	23,460	6,450	64,780

Chanzo: *Mapitio ya Hati za Malipo (IPCs) na Marekebisho ya Mkataba*

Mabadiliko ya usanifu yalisababisha ongezeko la Sh.64.78 bilioni ongezeko la gharama hilo lilitokana na maandalizi duni ya upembuzi yakinifu, Kasoro za uandaaji wa gharama za makadirio ya ujenzi wa barabara, kasoro za usanifu wa awali, pamoja na makosa ya vipimo kwenye mkataba.

Ninapendekeza TANROADS na TARURA watenge muda wa kutosha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa kina na wenye tija, usanifu wa miradi ufanyiwe mapitio yakutosha na wataalamu wa ndani au wa kujitegemea kabla ya kuanza utekelezaji wa mikatba, makadirio sahihi ya gharama za mradi yaandaliwe vizuri kabla ya kutangaza zabuni. Aidha, washirikishe washauri elekezi kusimamia miradi kabla ya mikataba ya wakandarasi kuanza ili kuhakikisha usanifu uliofanywa umekaguliwa kabla ya mkandarasi kuanza kazi, hatimaye kudhibiti gharama na ubora wa kazi ufanyike.

### 14.3 Usimamizi wa Mikataba

#### 14.3.1 Fidia kwa mkandarsi kiasi cha Sh. bilioni 29.87 kutokana na kuchelewa kukamilika kwa mradi

Kifungu kidogo cha 49.1 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba (GCC) ya miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Tanzania kinasema kuwa gharama za mkataba zitarekebishwa kwa mujibu wa kikokotoo cha marekebisho ya bei iliyotolewa katika mkataba huo. Vilevile, Kifungu cha 35 na 55 cha Masharti ya Jumla ya mikataba ya kazi inayofadhiliwa na fedha za maendeleo kutoka Umoja wa Nchi za Ulaya kinabainisha kuongezwa kwa muda wa utekelezaji wa kazi na madai ya malipo ya ziada kutokana na ongezeko la muda.

Mapitio ya hati za malipo ya kazi za ujenzi na marekebisho ya mikataba kwa miradi mitano ya barabara iliyotekelezwa na TANROADS yalibaini kuwa wakandarasi walilipwa Sh bilioni 29.87 kama fidia kutokana na kuchelewa kukamilika kwa mradi. Kinyume chake, katika miradi 5 ya barabara iliyotekelezwa na TARURA hakukuwa na fidia kwa mkandarasi kutokana na kuchelewa kwa utekelezaji wa mradi. Ukaguzi ulibaini sababu kuu za ucheleweshaji wa mradi zilikuwa:

**(i) Kuchelewa kulipwa kwa malipo ya awali kwa mkandarasi**

Mapitio ya nyaraka za mradi wa Barabara ya Mpemba - Isongole yalibaini kuwa Mkandarasi aliwasilisha dhamana ya utendaji kazi na dhamana ya malipo ya awali. Awamu ya kwanza ya malipo ya dhamana ya utendaji yaliwasilishwa tarehe 5 Juni 2017 na ya awamu ya pili yaliwasilishwa tarehe 12 Novemba 2018. Hata hivyo, awamu ya kwanza ya malipo ya awali kwa mkandarasi yalitakiwa kulipwa tarehe 5 Juni, 2017 lakini yalilipwa tarehe 12 Februari 2018 na awamu ya pili ya malipo ya awali yalitakiwa kulipwa tarehe 11 Desemba 2018 lakini yalilipwa tarehe 10 Juni 2019. Ucheleweshaji huu wa malipo ya awali yalisababisha nyongeza ya muda na gharama kwa mkandarasi kiasi cha Sh. 2,522,953,330.22.

**(ii) Ongezeko la gharama kwa ajili ya kusogeza mbele muda wa dhamana utendaji kazi**

Ukaguzi ulibaini kuwa kiasi cha mkataba wa awali kilichoombwa na mkandarasi kama dhamana ya utendaji kwa mkataba wa barabara ya Kikusya - Ipinda - Matema kilikuwa ni Sh. 2,792,000,000. Hata hivyo, kukamilika kwa mradi kulicheleweshwa kwa miezi 28.5. Pia, dhamana iliongezwa kutoka tarehe ya kuanza kwa mradi hadi mwisho wa Kipindi cha matazamiao ya mradi kilichorekebishwa. Ilibainika kuwa gharama za dhamana zilizoongezeka kwa mkandarasi zililipwa na mwajiri na kusababisha ongezeko la gharama ya dhamani hiyo kwa Sh. 5,235,000,000. Hii iliongeza gharama ya ziada ya Sh. 2,443,000,000.

**(iii) Ucheleweshaji wa mwajiri katika kutoa misamaha ya kodi kwenye vifaa vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi, mitambo/vifaa, mafuta na vilainishi**

Ukaguzi wa hati ya maridhiano Na.1 na 2 ya mradi wa barabara wa Kidatu-Ikafara ulibaini kuwa mkandarasi alilipwa fidia kwa muda na gharama zinazohusiana na ucheleweshaji wa mwajiri (Wizara ya Fedha na Mipango) katika kutoa misamaha ya ushuru kwa bidhaa zinazoingizwa nchini kama vile mitambo/vifaa, mafuta na vilainishi. Ukiukaji huu wa mwajiri ulisababisha kuongezeka kwa gharama ya Sh. bilioni 11.88. Kiasi hicho kililipwa kwa mkandarasi kama gharama za kusimamisha kazi kutokana na kuchelewa kutoa tangazo la misamaha hiyo ya kodi.

**(iv) Marekebisho ya bei**

Mapitio ya Hati ya Malipo Na. 23 ya mradi wa Barabara ya Mpemba - Isongole yalionyesha kuwa TANROADS ilimwongezea mkandarasi siku 485 kuanzia tarehe 22 Agosti 2019 hadi tarehe 19 Desemba 2020, sawa na miezi 19.

Ongezeko hili la muda lilisababisha mkandarasi kulipwa jumla ya Sh. 3,062,893,818.00 kama gharama ya ziada kutokana na mfumuko wa bei wakati wa nyongeza.

**(v) Hasara na gharama zilizolipwa kwa mkandarasi kama fidia**

Mapitio ya Nyaraka za Mkatoba wa mradi wa Barabara ya Mpemba - Isongole yalionesha kuwa mkandarasi aliwasilisha madai saba (7). Miongoni mwa madai hayo, dai la saba lilihusu fidia ya gharama za ziada zilizochangiwa na kuongezwa kwa muda kwa siku 485, ambazo mwajiri aliidhinisha kupitia madai namba 2, 3 na 4 jumla ya Sh. 2,454,035,216.82.

**Jedwali 37** linaonesha jumla ya miezi iliyocheleweshwa na mambo yaliyochangia gharama ya miradi kuzidi kutokana na ongezeko la muda wa ziada wa mradi.

**Jedwali 37: Gharama iliyozi kwa sababu ya kuchelewa kukamilika kwa miradi**

Jina la Mradi	Muda ulioch elewe shwa (Miezi )	Mambo yaliyo sababisha ongezeko la gharama (SH. TZ. Bilioni)					Jumla (Sh. bilioni)
		Kusogeza mbele muda wa dhamana ya utendaji kazi (Sh. bilioni)	Kuchele wa kwa malipo ya awali (Sh. bilioni)	Mareke bisho ya bei (Sh. bilioni)	Hasara na gharama za mkandarasi kutokana na ongezeko la muda (Sh. bilioni)	Uondoaji wa miundom binu ya Huduma	
Mikumi - Kidatu	42	0.00	0.00	0.00	11.01	0.00	11.01
Kikusya - Matema	28.5	2.44	0.00	2.01	0.08	1.61	6.14
Mpemba - Isongole	19	0.00	2.52	3.06	2.45	0.00	8.03
Daraja la Wami	25.49	0.00	0.00	3.08	0.00	0.00	3.08
Maswa - Mwigumbi	11.17	0.00	0.00	1.61	0.00	0.00	1.61
<b>Jumla</b>	<b>126.16</b>	<b>2.44</b>	<b>2.52</b>	<b>9.76</b>	<b>14.41</b>	<b>1.61</b>	<b>29.87</b>

**Chanzo:** *Hati za malipo na marekebisho ya mkatoba*

Tathmini inaonesha sababu mbali mbali za kuchelewa kwa miradi zilichangia ongezeko la gharama za miradi. Miradi ilichelewa kwa jumla ya miezi 126.16, na kusababisha ongezeko la gharama za miradi kwa jumla ya Shilingi bilioni 29.87.

Ninapendekeza TANROADS na TARURA wahakikishe wanalipa malipo ya awali kwa wandarasi katika muda uliopangwa kwenye mkataba, kuzingatia taratibu za msamaha wa kodi zinafanyika mapema kabla ya kusaini mkataba na kuweka udhibiti mzuri wa marekebisho ya bei ya mkataba, kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati ili kuzuia ongezeko la gharama kutokana na kuongeza muda wa dhamana ya utendaji kazi na fidia kwa mkandarasi kutokana na ucheleweshaji wa mradi.

### 14.3.2 Riba kutokana na kuchelewa kwa malipo ya kazi za ujenzi kwa wa kandarasi jumla ya Sh. bilioni 44.48

Kifungu cha 45 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba wa miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Tanzania kimebainisha kuwa mwajiri atamlipa mkandarasi kiasi kilichothibitishwa na meneja wa mradi ndani ya siku 28 tangu tarehe ya kila hati ya malipo. Ikiwa mwajiri atamlipa malipo mkandarasi kwa kuchelewa, mkandarasi atalipwa riba kwa malipo yaliyocheleweshwa katika malipo yanayofuata.

Ukaguzi wa hati za malipo ya kazi za ujenzi katika miradi iliyokaguliwa ulibaini kuwa miradi minne ya barabara iliyotekelezwa na TANROADS na mradi mmoja uliotekelezwa na TARURA haikuwalipa malipo wakandarasi kwa wakati kama ilivyobainishwa kwenye mkataba.

Sababu ya kucheleweshwa malipo ni: TANROADS kuchelewa kuomba fedha kwa Wizara ya Ujenzi; Wizara ya Ujenzi kuchelewa kuomba fedha kwa Wizara ya Fedha; na Wizara ya Fedha kuchelewesha kutoa fedha kwa Wizara ya Ujenzi. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa TANROADS, baada ya kupokea fedha kutoka Wizara ya Ujenzi, ilivalipa wakandarasi kwa wakati.

Hii kuchelewa kulipa wakandarasi kulisababisha ongezeko la gharama kwa Sh. bilioni 44.48 ikiwa ni riba iliyolipwa kwa wakandarasi kama fidia, kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali 38**.

**Jedwali 38: Ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi uliopo kiba riba**

Jina la Mradi	Riba kwa kuchelewa kulipwa mkandarasi (Sh. bilioni)	Riba kwa kuchelewa kulipwa Mshauri elekezi (Sh. bilioni)	Jumla (Sh. bilioni)
Kikusya - Matema	26.37	0.00	26.37
Mpemba - Isongole	5.26	0.00	5.26
Daraja la Wami	1.51	0.23	1.74
Maswa - Mwigumbi	9.43	0.00	9.43
Mji wa Kiserikali	1.68	0.00	1.68
<b>Jumla</b>	<b>44.25</b>	<b>0.23</b>	<b>44.48</b>

Chanzo: Malipo ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi

Kutofuata matakwa ya mkataba ya kuwalipa wakandarasi malipo ya hati kwa kazi zilizofanyika, kwa miradi minne ya TANROADS na mradi mmoja wa TARURA, kumesababisha ongezeko la gharama za miradi hiyo kwa shilingi bilioni 44.48. Ongezeko ilo likiwa kama riba ambazo zimelipwa kwa wakandarasi kwa sababu ya kuchelewesha malipo.

Ninapendekeza TANROADS na TARURA kuwalipa wakandarasi kwa wakati, kuweka mfumo bora wa utaratibu wa malipo, pia kufuatilia kwa karibu tarehe za malipo ili kuzuia malipo ya riba yasiyo ya lazima. Hii itahakikisha maendeleo mazuri ya utekelezaji wa miradi na uzingatiaji wa bajeti.

### 14.3.3 Malipo ya ziada ya Sh. bilioni 10.44 kwa mshauri elekezi kutokana na kuchelewa kukamilika kwa mradi

Kifungu kidogo cha 47.1 ya Masharti ya Jumla ya Mkataba wa miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Tanzania kimebainisha kwamba bei inayotozwa kwa huduma za mshauri elekezi itarekebisha kwa mujibu wa utaratibu wa marekebisho ya bei kutokana na ongezeko la muda.

Ukaguzi ulibaini kuwa, kutokana na kuchelewa kwa mradi kukamilika, washauri elekezi wa miradi waliongezewa muda wa kusimamia utekelezaji wa mkataba, pamoja na nyongeza ya gharama. Nyongeza ya gharama kwa washauri elekezi ilitokana na marekebisho ya bei zilizokuwa kwenye mkataba, fidia ya gharama zilizoingwa na washauri elekezi hao kutokana na ongezeko la muda wa kusimamia mradi, pamoja na gharama za kuchelewesha kukamilisha mradi. Gharama iliyolipwa kutokana na kuongezwa kwa muda wa mkataba kwa washauri elekezi ilikuwa Shilingi bilioni 10.44, kama inavyoonekana kwenye **Jedwali 39**.

**Jedwali 39: Hali ya malipo ya washauri elekezi**

Jina la Mradi	Marekebisho ya bei za mkataba (Sh. bilioni)	Gharama zilizotokana na kuchelewesha kwa miradi (Sh. bilioni)	Jumla (Sh. bilioni)
<b>Miradi ya Barabara nne na Daraja moja chini ya utekelezaji wa TANROADS</b>			
Mikumi - Kidatu	0.00	4,463.00	4,463.00
Kikusya - Matema	0.00	749.58	749.58
Mpemba - Isongole	0.00	432.83	432.83
Daraja la Wami	120.04	2,858.24	2,978.28
Maswa - Mwigumbi	57.79	195.55	253.34
<b>Jumla TANROADS</b>	<b>177.83</b>	<b>8,699.20</b>	<b>8,877.03</b>
<b>Miradi mitano chini ya utekelezaji wa TARURA</b>			
Mji wa Kiserikali	0.00	779.82	779.82
<b>Jumla TARURA</b>	<b>0.00</b>	<b>779.82</b>	<b>779.82</b>
<b>Jumla</b>	<b>177.8364</b>	<b>10,258.84</b>	<b>10,436.67</b>

**Chanzo:** *Malipo ya Washauri elekezi na ripoti za mradi*

Kuchelewa kukamilika kwa mradi kulisababisha gharama ya ziada ya Shilingi bilioni 10.44 kulipwa kwa washauri elekezi katika miradi ya TANROADS na TARURA iliyokaguliwa.

**Ninapendekeza TANROADS na TARURA kuimarisha usimamizi na uzingatiaji wa muda wa kumaliza kazi kimkataba ili kupunguza ongezeko la gharama na fidia kutokana na ucheleweshaji wa miradi kukamilika.**

#### **14.3.4 Malipo ya Sh. bilioni 3.99 bila mkataba kati ya TECU na Wizara ya Fedha**

Kanuni ya 233(1) na (2) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 inataka pale zabuni inapokubaliwa na Afisa Masuuli wa taasisi, ataingia mkataba rasmi na Mzabuni aliyeshinda na mkataba utafuata muundo uliowekwa na kujumuisha masharti ya mkataba na vifungu vilivyoainishwa kwenye nyaraka za zabuni.

Ukaguzi wangu umebaini kuwa baada ya kumalizika kwa muda wa mkataba kati ya M/s Nicholas O'Dwyer na Wizara ya Fedha kwa mradi wa Barabara ya Mikumi-Iyakara, TECU ilichukua nafasi ya ushauri elekezi bila mkataba rasmi na malipo ya shilingi 3,987,276,185.38 yalilipwa.

TECU kusimamia mkataba wa mkandarasi bila yenye mwenyewe kuwa na mkataba kunaashiria hatari, kwani kukosekana kwa mkataba, kunafanya kazi alizopewa TECU kutokuwa wazi, na kupelekea ugumu katika kutatua mgogoro, na kushindwa kudhibiti gharama anazolipwa TECU kwa kukosa muongozo wa malipo yake.

**Ili kupunguza vihatarishi na kuhakikisha uzingatiaji wa Kanuni za ununuzi, Wizara ya fedha inatakiwa kurasimisha usimamizi wa TECU katika mradi kwa kuingia mkataba na kuzingatia taratibu za manunuzi.**

# SURA YA KUMI NA TANO

## UKAGUZI WA KIUFUNDI KUHUSU UDHIBITI WA GHARAMA ZA MIRADI YA BARABARA

### 15.1 Utangulizi

Ukaguzi ulitathmini miradi ya ujenzi wa barabara iliyosimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kuanzia mwaka 2011/12 hadi 2023/24 ikilenga miundombinu ya kimkakati mikoa ya Katavi, Kigoma na Tabora na miundombinu ya kuboresha utalii katika hifadhi za Taifa za TANAPA. TANROADS ilipokea jumla ya Sh. bilioni 182 kutoka serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi barabara ikiwemo Barabara ya Tabora - Koga ili kusaidia azma ya Tanzania kuwa kitovu cha viwanda katika eneo la Afrika Mashariki. TANAPA ililenga katika kuboresha miundombinu ya utalii katika hifadhi za taifa, ikiwa na mipango ya ujenzi wa kilomita 500 za barabara mpya na ukarabati wa kilomita 10,500 kupitia mradi wa REGROW uliofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Ukaguzi ulitathmini mipango, usimamizi wa kifedha, ununuzi, na utekelezaji wa miradi, ili kuhakikisha miradi inakidhi malengo ya maendeleo ya miundombinu ya kimkakati na kuchangia katika ukuaji wa sekta ya usafirishaji na utalii nchini Tanzania.

#### 15.1.1 Upembuzi yakinifu na utafiti wa hali halisi ya barabara usio na ufanisi

Sehemu ya 3.3 ya Mwongozo wa Usanifu wa Kijometri wa Barabara wa Wizara ya Ujenzi wa mwaka 2011 inasisitiza umuhimu wa kuzingatia masuala mtambuka katika upangaji wa barabara, ujenzi, na matengenezo na ushawishi wa ardhi, jiolojia na mteremko kwenye muundo wa barabara, gharama za ujenzi na uteuzi wa ukanda wakati wa upembuzi yakinifu na matengenezo.

Nimebaini kuwa miradi ya TANROADS na TANAPA haikuwa na upembuzi yakinifu na utafiti wa kina kuhusu hali halisi ya Barabara. Ni mradi mmoja tu ulikuwa umefanyiwa upembuzi yakinifu kwa ufanisi. Miradi mingine ilikuwa na tathmini zisizo kamili ambazo zilikosa tathmini muhimu kama vile tathmini ya uhandisi, tathmini ya vyombo vinavyotumia barabara, tathmini ya kiuchumi na tathmini ya hali ya kijamii kama inavyoonekana katika **Jedwali 40**.

Upungufu mahsusi ulijumuisha kutowekwa kwa tabia za kijiografia, maelezo ya jiolojia, na vipengele vya mazingira vinavyohitajika na Mwongozo wa Usanifu wa Kijometri wa Barabara wa mwaka 2011.

**Jedwali 40: Miradi ambayo upembuzi yakinifu haukufanyika kwa ufanisi na kusababisha gharama za ziada**

Jina la Mradi	Upembuzi Yakinifu/Utafiti wa Hali Halisi ya Barabara	Gharama za Ziada Zilizosababishwa (Sh.)
Ujenzi wa Barabara ya Malagarasi - Uvinza (kilomita 51.1)	Upembuzi yakinifu haukufanyika kabisa	730,783,864
Ujenzi wa Barabara ya Kaliua - Malagarasi - Ilunde (Kilomita 156); Sehemu ya 1: Barabara ya Kaliua - Kazilambwa (kilomita 56) na Sehemu ya 2: Kipande cha Chagu - Kazilambwa (kilomita 36)	Upembuzi yakinifu haukufanyika kwa ufanisi	19,905,638,467
Ujenzi wa Barabara ya Tabora - Koga - Mpanda (Kilomita 356); Sehemu ya 1: Kipande cha Tabora - Sikonge (Usesula) (Kilomita 30)	Upembuzi yakinifu haukufanyika kwa ufanisi	3,812,864,042
Ujenzi wa Kipande cha Usesula - Komanga (Kilomita 108); Sehemu ya 1: Kipande cha Mji wa Sikonge (Kilomita 7.36) na Barabara ya Mkondo wa Sikonge (Kilomita 2.21); Sehemu ya 2: Kipande cha Komanga - Kasinde (Kilomita 108) na Barabara ya Mkondo wa Inyonga (Kilomita 4.8); na Sehemu ya 3: Kipande cha Kasinde - Mpanda (Kilomita 105.39) na Kipande cha Mji wa Uruwira (Kilomita 2.29)	Upembuzi yakinifu ulifanyika kwa ufanisi	16,712,992,434
Ujenzi wa Barabara katika Hifadhi za Taifa	Utafiti wa hali halisi ya barabara haukufanyika kwa ufanisi	496,479,720
<b>Jumla</b>		<b>41,658,758,528</b>

**Chanzo:** Tathmini ya Wakaguzi juu ya Upembuzi Yakinifu, tathmini ya hali halisi ya barabara, na Mabadiliko ya Gharama za Miradi, mwaka 2024

Upembuzi yakinifu usio na tija na uchunguzi wa hali halisi ulisababishwa na taarifa zisizotosheleza za kutathmini uwezekano wa mradi kutekelezwa. Upembuzi yakinifu usio na ufanisi ulisababisha makadirio yasiyo sahihi ya wahandisi. Upungufu huu ulisababisha gharama za ziada za miradi za takribani ya Sh 41,658,758,528.

Ninapendekeza TANROADS ifanye upembuzi yakinifu wa kina ili kuhakikisha miradi inafanyika kwa ufanisi, hatimaye kupunguza mabadiliko wakati wa ujenzi. Pia, TANAPA ifanye tathmini ya hali halisi ya barabara kwa kina ili kuepuka mabadiliko makubwa ya usanifu wakati wa ujenzi.

### 15.1.2 Usimamizi duni wa ubora wa kazi

Kifungu cha 114 cha Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kinataka Taasisi Nunuzi yahakikishe usimamizi mzuri wa kazi kwa kufuatilia ubora, gharama, kuhakikisha utoaji wa bidhaa na huduma kwa wakati, na kukamilisha kazi kulingana na masharti ya mkataba.

Uhakiki wa miradi iliyochaguliwa ulibaini kuwapo kwa mabadiliko katika ubora, hasusani kwa wakandarasi wa barabara za Hifadhi za Taifa, ambapo udongo wa asili usiofaa ulitumika badala ya udongo ulioelekezwa kutoka sehemu zilizoelekezwa kutumika ulioghharimu Sh. 44,838,500. Aidha, udongo dhaifu na changarawe dhaifu zilitumika katika ujenzi, hali iliyosababisha gharama za ziada za Sh. 309,017,500. Ujenzi wa Kipande cha Usesula - Komanga na miradi yake ya ziada, kwa kiasi kikubwa, ulikidhi viwango vya ubora, isipokuwa Barabara ya Mkondo wa Sikonge ambayo ilikuwa na mifereji ya pembeni isiyokidhi mahitaji. Udongo wa asili usiofaa umeoneshwa katika **Kielelezo 9**.

#### Kielelezo 9: Udongo asilia usio na ubora



*Chanzo: Wakaguzi walipotembelea eneo la mradi*

Miradi ya barabara na madaraja iliyosimamiwa na TANROADS ilikumbana na matatizo. Mathalani, Daraja la Koga lenye urefu wa mita 120 lilikuwa na nyufa kutokana na kukosa mianya ya kupumulia. Aidha, kulikuwa na maji yaliyotuma kwenye mifereji ya Barabara ya Sikonge Spur, kiasi cha kuhatarisha afya.

**Kielelezo 10: Maji yaliyotuma katika mitaro ya maji pembezoni mwa barabara**



**Chanzo:** Ukaguzi wa tarehe 27 Oktoba 2023

Hali hii ilisababishwa na mteremko usiotosheleza kuruhusu maji kutiririka yenyewe kupitia karavati linalokatisha barabara na kuunganisha mifereji iliyojengwa kando ya barabara.

**Ninapendekeza kwamba TANROADS na TANAPA wahakikishe wanafanya usimamizi mzuri wa wakandarasi na washauri kulingana na mikataba ya kazi.**

### 15.1.3 Ongezeko la gharama kutokana na usimamizi duni wa muda na kucheleweshwa kwa miradi

Kifungu cha 114 cha Kanuni za Ununuzi ya Umma za mwaka 2013 kinahitaji mashirika yanayonunua kuhakikisha kunakuwa na usimamizi mzuri wa kazi kwa kutoa bidhaa na huduma kwa wakati na kukamilisha kazi kulingana na masharti ya mkataba.

Ukaguzi wa nyaraka za miradi ulibaini kucheleweshwa kwa utekelezaji wa miradi. Kucheleweshwa huko kulisababisha gharama za ziada ya Sh. 7,530,695,811 kutokana na nyongeza za mkataba wa kazi kama inavyooneshwa katika Jedwali 41.

### Jedwali 41: Nyongeza za muda wa utekelezaji wa miradi na gharama zake

Mradi	Sababu ya Ongezeko la Utekelezaji wa Mradi	Gharama Zilizosababishwa (Sh.)
Ujenzi wa Barabara ya Kaliua - Malagarasi - Ilunde (Kilomita 156); Sehemu ya 1: Kipande cha Barabara ya Kaliua - Kazilambwa (Kilomita 56) na Sehemu ya 2: Kipande cha Kazilambwa - Chagu (Kilomita 36)	<p>Nyongeza ya muda kutoka tarehe 14 Machi 2016 hadi 10 Septemba 2016 na nyongeza nyingine kutoka tarehe 10 Septemba 2016 hadi 18 Septemba 2017 ambayo inafanya jumla ya siku 553 za kuchelewa kwa mkataba wa kazi kutokana na kuchelewesha kukabidhi eneo la mradi kwa mkandarasi na kuchelewa kutoa na kuhuisha vibali vya msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Hali hii ilisababisha ongezeko la gharama za Sh. 523,428,087.64. Pia, ilisababisha nyongeza ya muda kwa mkataba wa huduma za ushauri na gharama za ziada zinazofikia Sh. 590,504,932.08.</p> <p>Nyongeza ya muda wa mkataba wa kazi kwa siku 62 kutoka 6 Septemba 2015 hadi 7 Novemba 2015 kutokana na kuchelewa kukabidhi eneo la kazi kwa mkandarasi kutokana na kutolipa kwa wakati fidia kwa Mali Zilizoathiriwa na Mradi (PAPs), hivyo kusababisha gharama za ziada za Sh. 1,388,191,895.67.</p> <p>Nyongeza ya muda kwa siku 180 kutoka 27 Julai 2022 hadi 23 Januari 2023 kwa ajili ya kukamilisha kazi na gharama za kufanya kazi kwa muda mrefu na gharama za ziada kufikia Sh. 191,772,926.82 ili kufidia gharama za awali na za jumla.</p>	2,103,392,910.13
Ujenzi wa Barabara ya Tabora - Koga - Mpanda (Kilomita 356); Sehemu ya 1: Kipande cha Tabora - Sikonge (Usesula) (Kilomita 30) na Ujenzi wa Sehemu ya Usesula - Komanga (Kilomita 108); Sehemu ya 1: Kipande cha Mji wa Sikonge (Kilomita 7.36) na Barabara ya Mkondo wa Sikonge (Kilomita 2.21); Sehemu ya 2: Kipande cha Komanga - Kasinde (Kilomita 108) na Barabara ya Mkondo wa Inyonga (Kilomita 4.8); na Sehemu ya 3: Kipande cha Kasinde - Mpanda (Kilomita 105.39) na Kipande cha Mji wa Uruwira (Kilomita 2.29)	<p>Nyongeza ya muda kwa Mkataba wa Huduma za Ushauri ili kufidia muda ulioongezeka kwa katika Mkataba wa Kazi uliosababisha gharama za ziada za Sh. 1,269,236,370 kwa Sehemu ya 1.</p> <p>Nyongeza ya muda wa mkataba wa kazi kwa Sehemu ya 2: Kipande cha Barabara ya Komanga - Kasinde (Kilomita 108) na Kipande cha Mji wa Inyonga (Kilomita 4.18) iliongeza gharama kwa Sh. 4,158,066,531.68.</p> <p>Gharama za nyongeza kwa ajili ya huduma za ushauri zilizoongezeka kwa gharama zinazofikia Dola za Marekani 982,754.52, sawa na Sh. 2,287,370,972.85 kwa Sehemu ya 3.</p>	5,427,302,901.68
<b>Jumla</b>		<b>7,530,695,811.81</b>

**Chanzo:** Tathmini ya wakaguzi kwenye malipo, mawasiliano na maamuzi kwa ajili ya nyongeza ya muda wa kazi

Kucheleweshwa huku kulitokana na malipo kucheleweshwa, kucheleweshwa kwa kukabidhi eneo la kazi kwa makandarasi, na ucheleweshwaji wa utoaji wa vibali vya msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Kufuatia hivyo, mikataba ya huduma za ushauri iliongezewa muda, hali iliyosababisha gharama za ziada za jumla ya Sh. 4,147,112,274.

Ninapendekeza kwamba TANROADS ihakikishe inafanya kwa wakati makadirio ya mahitaji ya fedha, malipo, na matumizi ili kuzuia kucheleweshwa kwa malipo na kusimamishwa kwa kazi. Pia, isimamie muda kwa ufanisi na kupitisha nyongeza kwa haraka kwa washauri na wakandarasi ili kuepuka gharama zaidi. Zaidi, ifanye tathmini za mali na fidia kwa wakati kwa ajili ya kukabidhi eneo la kazi kwa wakandarasi kwa wakati.

### 15.1.4 Usimamizi duni wa gharama za mradi

Kifungu cha 114 cha Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kinahitaji mashirika yanayonunua kuhakikisha usimamizi mzuri wa kazi kwa kufuatilia gharama za bidhaa na huduma na kukamilisha kazi kulingana na masharti ya mkataba.

Mapitio ya nyaraka za mradi yalibaini kuzidi kwa gharama za miradi kwa jumla ya Sh. 21,435,565,394, ambapo TANROADS ililipa Sh. 21,024,537,374 na TANAPA Sh. 411,028,020 zaidi kama inavyooneshwa katika **Jedwali 42**.

**Jedwali 42: Gharama za ziada kwa makandarasi na washauri**

Mwajiri	Jina la Mradi	Bidhaa au Huduma Iliyotolewa	Gharama Zilizohusika (Sh.)
TANROADS	Ujenzi wa Barabara ya Kaliua - Malagarasi - Ilunde (Kilomita 156); Sehemu ya 1: Kipande cha Barabara ya Kaliua - Kazilambwa (Kilomita 56) na Sehemu ya 2: Kipande cha Kazilambwa - Chagu (Kilomita 36)	Gharama ya ziada ya Sh. 118,494,377.80 ilisababishwa na makosa katika kuhesabu malipo ya riba kutokana na malipo yaliyocheleweshwa. Malipo kwa mkandarasi kwa muda ambao huduma za kununua mafuta na matengenezo ya magari kwa ajili ya mshauri na wafanyakazi wake hazikutolewa na kusababisha gharama za ziada za Sh. 180,671,798.	299,166,175
	Ujenzi wa Barabara ya Tabora - Koga - Mpanda (Kilomita 356); Sehemu ya 1: Kipande cha Tabora - Sikonge (Usesula) (Kilomita 30).	Fidia ya Sh. 1,735,055,600 ilitokana na kazi kucheleweshwa kuanza kwa kuwa malipo ya awali yalicheleweshwa na TANROADS.	1,735,055,600

Mwajiri	Jina la Mradi	Bidhaa au Huduma Iliyotolewa	Gharama Zilizohusika (Sh.)
	Ujenzi wa Sehemu ya Usesula - Komanga (Kilomita 108); Sehemu ya 1: Kipande cha Mji wa Sikonge (Kilomita 7.36) na Barabara ya Mkondo wa Sikonge (Kilomita 2.21); Sehemu ya 2: Kipande cha Komanga - Kasinde (Kilomita 108) na Barabara ya Mkondo wa Inyonga (Kilomita 4.8); na Sehemu ya 3: Kipande cha Kasinde - Mpanda (Kilomita 105.39) na Sehemu ya Mji wa Uruwira (Kilomita 2.29)	Kosa la kihisabati linalosababisha malipo ya ziada yenye thamani ya Sh. 376,583,391. Nyongeza ya gharama kutokana na mabadiliko ya bei ya soko kwa Sehemu ya 1 kutokana na utekelezaji wa mradi kuchelewa, hivyo kusababisha ongezeko la gharama za mradi la Sh. 9,944,247,016.37 Nyongeza ya gharama kutokana na mabadiliko ya bei ya soko kwa Sehemu ya 2 kutokana na kuchelewa kutekeleza mradi, hivyo kusababisha gharama za mradi kuongezeka kwa kiasi cha Sh. 8,669,485,191.64	18,990,315,599
	<b>Jumla Ndogo</b>		<b>21,024,537,374</b>
TANAPA	Ujenzi wa Barabara katika Hifadhi za Taifa	TANAPA ililipa kiasi kikubwa zaidi kwa kazi za kukwangua barabara, ujenzi wa tuta la barabara, kuweka changarawe barabarani, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua, madaraja madogo, na kiasi cha zege kama ilivyobainishwa katika hati za malipo zilizotolewa. TANAPA ililipa ziada ya Sh. 411,028,020 kwa makandarasi	411,028,020
	<b>Jumla Ndogo</b>		<b>411,028,020</b>
<b>Jumla Kuu</b>			<b>21,435,565,394</b>

Chanzo: Tathmini ya ukaguzi wa mahesabu ya malipo na uhakiki wa kazi katika maeneo ya miradi

Malipo ya ziada yalisababishwa na makosa katika kukokotoa na ukosefu wa uhakiki wa malipo yaliyothibitishwa na mwajiri pamoja na washauri. Makosa haya yalitokana na gharama za nyongeza zilizosababishwa na kucheleweshwa kwa malipo ya awali pamoja na mikataba ya huduma za ushauri kuongezewa muda; hivyo kuchelewa kuanza kwa miradi. Vivile, kulikuwa na gharama zilizosababishwa na riba iliyotozwa kwenye malipo yaliyocheleweshwa kwa wakandarasi kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali 43**.

### Jedwali 43: Gharama za riba kutokana na malipo yaliyocheleweshwa

Jina la Mradi	Riba (Sh.)
Ujenzi wa Barabara ya Malagarasi - Uvinza (Kilomita 51.1)	18,446,987
Ujenzi wa Barabara ya Kaliua - Malagarasi - Ilunde (Kilomita 156); Sehemu ya 1: Kipande cha Barabara ya Kaliua - Kazilambwa (Kilomita 56) na Sehemu ya 2: Kipande cha Kazilambwa - Chagu (Kilomita 36)	12,542,906,084
Ujenzi wa Barabara ya Tabora - Koga - Mpanda (Kilomita 356); Sehemu ya 1: Kipande cha Tabora - Sikonge (Usesula) (Kilomita 30)	1,370,076,595



## Ukaguzi Wa Kiufundi Kuhusu Udhhibiti Wa Gharama Za Miradi Ya Barabara

Jina la Mradi	Riba (Sh.)
Ujenzi wa Sehemu ya Usesula - Komanga (Kilomita 108); Sehemu ya 1: Kipande cha Mji wa Sikonge (Kilomita 7.36) na Barabara ya Mkondo wa Sikonge (Kilomita 2.21); Sehemu ya 2: Kipande cha Komanga - Kasinde (Kilomita 108) na Barabara ya Mkondo wa Inyonga (Kilomita 4.8); na Sehemu ya 3: Kipande cha Kasinde - Mpanda (Kilomita 105.39) na Sehemu ya Mji wa Uruwira (Kilomita 2.29)	7,142,601,016
<b>Total</b>	<b>21,074,030,683</b>

**Chanzo:** Tathmini ya ukaguzi kuhusu Malipo ya Utekelezaji wa Miradi ya Barabara na Uhakiki katika Maeneo ya Miradi, 2024

Hali hii ilichangiwa na Hazina kutotoa fedha kwa wakati. Pia, kulitokana na kucheleweshwa kwa malipo ya kazi, hivyo kusababisha kusimamishwa kwa kazi pamoja na madai ya mkandarasi kuhusu kuongezewa muda wa kazi.

Ninapendekeza kwamba TANROADS idhibiti ongezeko la gharama za miradi kwa kusimamia riba kutokana na kucheleweshwa kwa malipo, mabadiliko ya bei, madai yanayohusiana na kuchelewesha, na kuharakisha mchakato wa utoaji wa vibali vya msamaha wa VAT. Pia, washirikiane na Wizara za Fedha na Mipango pamoja na wadau wengine ili kukabiliana na kucheleweshwa kwa malipo.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho I: Msingi wa kutoa hati zenye shaka

Na.	Jina la Mradi	Watekelezaji	Misingi ya kutoa hati isiyoridhisha
1	Mradi wa kujumuisha malengo katika kupambana na athari za Mazingira, Umaskini na Jinsia katika Kuleta Maendeleo Endelevu na Kuondoa Umaskini	Taasisi ya Mipango ya Maendeleo Vijijini Kituo cha Kanda ya Ziwa, Mwanza	Taarifa ya Gharama (CDR) ilishindwa kujumuisha Dola za Kimarekani 266,468.10 zilizopokelewa kupitia risiti Na. 00T10081DR2300005 ya tarehe 22 Agosti 2022, iliyotumika kwa shughuli za mradi ndani ya mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Desemba 2022. Kwa sababu hiyo, Taarifa ya Gharama CDR inakadiriwa kuwa pungufu kwa dola 266,468.10.

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23

## Kiambatisho II: Kuchelewa kusainiwa kwa mikataba miwili kwa zaidi ya siku 82

Na.	Jina la Mtekel ezaji	Na. ya Zabuni	Maelezo	Kiasi (Sh.)	Tarehe ya Taarifa ya Tuzo (A)	Tarehe ya kusaini mkataba (B)	Jumla ya Siku (B-A)	(D) Muda wa kuwasilisha kwa mwanasheria mkuu(siku)	(E) Muda wa Kupeku a (Siku)	Muda uliochelewa (C-(D+) siku)
1.	TPDC	ISP-DRM-NRG/TZ/ AfDB/CS 02/QCBS /2018	Huduma za Ushauri kwa ajili ya Utafiti na Mapitio ya Mkataba wa Kushiriki Uzalishaji wa Mfano (MPSA).	485,384,000	09/11/2022	27/02/2023	110	3	21	86
2.	TPDC	ISP-DRM-NRG/TZ/ AfDB/G1 1/ICB/20 20 Lot 1	Ziada kwa Ugavi, Ufungaji, Usanidi, Upimaji na Uagizaji wa Seva, Miundombinu ya Uhifadhi, Vifaa vya Mtandao kwa Kituo cha Takwimu cha Msingi cha TeSWS	5,753,219,987	06/12/2022	22/03/2023	106	3	21	82
Jumla				6,238,603,987						

## Kiambatisho III: Utekelezaji wa shughuli za ujenzi wenye thamani ya Sh. bilioni 1.53 zilizofanyika bila kusaini mkataba

Jina la fundi	Maelezo	Gharama za ujenzi (Sh.)	Tarehe ya kuanza	Tarehe ya kutembelea mradi	Hatua ya ujenzi
<b>Halmashauri ya Wilaya ya Mtama</b>					
Hamis Y. Mdabulachi	Ujenzi wa nyumba ya watumishi 2 katika eneo la Chiponda SS-Mtama	8,800,000	15/09/2023	21/09/2023	Msingi kabla ya kuundwa kwa slab
<b>Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa</b>					
Shokwaman Enterprises LTD	Ujenzi wa madarasa na miundombinu mingine ya shule katika eneo la Namatungutungu-Kilwa	547,093,524	10/09/2023	18/09/2023	Kibali cha ujenzi na uhamasishaji wa vifaa

Ally Salum Mtotela	Ujenzi wa madarasa na miundombinu mingine ya shule katika eneo la Mavuji-Kilwa	550,000,000	15/09/2023	18/09/2023	Kibali cha ujenzi na uhamasishaji wa vifaa
Mwanaamin B. Chakaas	Ujenzi wa nyumba ya watumishi 2 katika eneo la Ngome S/S-Kilwa	94,430,200	08/09/2023	18/09/2023	Msingi kabla ya slab
Halmashauri ya Manispaa ya Lindi					
Ambapo Ahmed Kindaukile	Ujenzi wa nyumba 2 katika 1 ya Watumishi Kilangala SS-Lindi MC	13,500,000	20/08/2023	13/09/2023	Lintel (Kazi Programu haipatikani)
Mafundi mbalimbali wa ndani	Majengo 11 kwa awamu ya pili yanafanya kazi Lindi Girls-Lindi MC	220,000,000	Julai 2023	13/09/2023	Msingi (Mkataba na Programu ya kazi)
<b>Jumla</b>		<b>1,528,253,924</b>			

Chanzo: Ripoti ya Utendaji na ziara ya tovuti - Novemba 2023

#### Kiambatisho IV: Kuchelewa kukamilika kwa miradi na kutokudai tozo ya kuchelewesha kazi za mradi

Wizara	Mradi	Maelezo ya Kuchelewa	Kiasi (Sh.)	Muda wa Kuchelewa
Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu Na. 68)	Mradi wa Tanzania Kidijitali (DTP) - Huduma za Ushauri	Huduma za ushauri kwa tathmini juu ya uanzishwaji wa Taasisi ya Teknolojia ya Digital Zonal Soft na vituo vya ukarabati wa vifaa vya TEHAMA.	824,852,000	Miezi ya 6
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST)	Mpango wa ESPJ - Ujenzi wa Mabalanga na Nkasi DVTC	Shughuli za ujenzi wa Mabalanga na Nkasi DVTC chini ya Mpango wa Elimu na Ujuzi kwa Ajira za Uzalishaji.	565,439,840	Miezi hadi 6 <sup>2</sup>
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST)	Mradi wa LANES II - Ujenzi wa shule 22 za msingi	Kutokamilika kwa ujenzi wa shule 22 za msingi katika halmashauri 16 chini ya Mpango wa Kimataifa wa Elimu - Kusoma na Kuhesabu.	1,267,075,000	Haijaanza
Wizara ya Maliasili na Utalii	Mradi wa Usimamizi wa Maliasili kwa Utalii na Ukuaji (REGROW)	utoaji wa usanifu wa kina, maandalizi ya nyaraka za bidding na usimamizi wa ujenzi wa ofisi 10 za shirika la wamwagiliaji katika miradi ya umwagiliaji juu ya Bonde la Usagu	117,359,600	Mwezi mmoja
Wizara ya Nishati	Upanuzi wa Umeme Vijijini Tanzania Programu ya (TREEP)	Kuchelewa kutoa huduma za ushauri	733,860,862	Miezi minne
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST)	Usafi wa Mazingira na Usafi wa Mazingira shuleni (SWASH)	Kuchelewa kufanya uhakiki huru		Miezi saba
Shirika la Wakala wa Meli Tanzania	Mradi wa Mawasiliano na Usafiri wa Bahari ya Ziwa Victoria (Mlvmct)	Kuchelewa makabidhiano ya tovuti	998,817,336	Miezi 3
Wizara ya Afya	Taasisi ya Susan Thomson Buffet	kuchelewa kupokea bidhaa za kuokoa maisha ya SRH / MNCAH	878,308,245	Miezi mitano
<b>Jumla</b>			<b>5,385,712,883</b>	

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23

#### Kiambatisho V: Riba iliyotozwa kwa kuchelewesha malipo

Na	Jina la Mradi	Mtekelezaji	Maelezo	Kiasi (Sh.)
1	Mradi wa Mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) - Awamu ya II	TANROADS	Riba inayolipwa kwa sababu ya malipo yaliyochelewesha	223,417,684
2	Mradi wa Kuboresha Barabara ya Kimataifa ya Rumonge - Gitaza (km 45) na Kabingo - Kasulu -Manyovu (km 260.6)	TANROADS	Riba ya kulipwa kwa malipo yaliyochelewesha	214,024,716

3	Mradi wa barabara ya Kimataifa ya: Bagamoyo - Horohoro/Lunga Lungu - Malindi	TANROADS	Maslahi ya Kushtakiwa kwa Malipo ya Kuchelewa	11,345,677
4	Mradi wa barabara ya Kimataifa ya: Bagamoyo - Horohoro/Lunga Lungu - Malindi	TANROADS	Kujitolea kwa sababu ya shughuli zilizotekelezwa zilizopangwa za mradi	57,302,196
5	Usimamizi wa Maliasili kwa Utalii na Ukuaji	Wizara ya Maliasili na Utalii,	Malipo ya riba kwa malipo ya kuchelewa ya kiasi cha mapema	47,851,268
6	Programu ya Msaada wa Sekta ya Usafiri (TSSP)	TANROADS	Ongezeko la riba kutokana na kuchelewa kushughulikia madai ya mkandarasi	160,311,244
7	Mradi wa Pili wa Kusaidia Sekta ya Maji	Wizara ya Maji	Adhabu ya kucheleweshwa kwa malipo ya IPCs ya mkandarasi	25,004,367
8	Barabara ya Ring ya Jiji la Dodoma ya nje ya Jiji la Dodoma hadi Bitumen Standard (112.3 km)	TANROADS	Malipo ya riba kutokana na kucheleweshwa kwa malipo ya mkandarasi	208,595,036
9	Mradi wa kuunganisha Tanzania na Zambia (TAZA)	TANESCO	Kuchelewa kutumia kituo cha mkopo kinachovutia malipo ya ziada ya kujitolea	2,129,506,978
<b>Jumla</b>				<b>3,077,359,166</b>

**Chanzo:** Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23

#### Kiambatisho VI: Taarifa za shughuli ambazo hazikutekelezwa

Na	Jina la Mradi	Namba ya shughuli	Maelezo ya shughuli	Kiasi (Sh)
1	Mradi wa Kusaidia Sekta ya Maji	1	Utoaji wa huduma ya ushauri kwa mtaalamu wa mazingira katika utekelezaji wa Mradi wa WSSP II kwa Bonde la Wami/Ruvu (Cond ESIA kwa shughuli zinazopendekezwa)	346,500,000
		2	MAR Study	577,500,000
		3	Utoaji wa vifaa kwa jumuiya za watumiaji maji na mashine 15 za matofali	346,500,000
		4	Ujenzi wa ofisi 10 za jumuiya za watumiaji maji	231,000,000
		5	Uhuishaji wa maelezo ya jumuiya ya watumiaji maji, utayarishaji wa ramani za jumuiya ya watumiaji maji na uenezaji kwa jumuiya 11	232,119,310
		6	Ujenzi wa majiko ya bayogesi na nishati yaliyojengwa Uluguru NFR/kukuza matumizi ya teknolojia ya nishati mbadala iliyo nafuu na inayotumika na Uluguru NFR	140,847,000
		7	Kutoa vitalu vya miti kwa jumuiya ya umoja wa watumiaji maji, hasa katika vyanzo vilivyoharibiwa zaidi	251,096,445
		8	Kuwezesha utayarishaji wa mipango 30 ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 30	204,868,738
		9	Kuwezesha teknolojia za kilimo zilizoboreshwa kwa kuanzisha kilimo cha kontua, matuta, kilimo cha ukanda, kilimo cha misitu, mazao ya kufunika na kupanda mseto kwenye miteremko mikali.	756,407,051
		10	Ufuatiliaji na tathmini ya mradi	351,781,260
		11	Utekelezaji wa mipango ya hifadhi katika WRBWB	41,489,632
		12	Utekelezaji wa mipango ya IWRM katika WRBWB	509,425,062
		2	Taasisi ya Susan Thomson Buffet	13
14	Utekelezaji wa LRRP			924,000,000
2	Taasisi ya Susan Thomson Buffet	15	Uchapishaji wa mwongozo wa uzazi wa dharura na mwongozo wa rufaa ya utunzaji wa watoto wachanga	46,851,059
		16	Kuajiri wafanyakazi wenye ujuzi 34 katika hospitali 17 katika mikoa 17 katika maeneo ya mbali ili kuimarisha huduma za SRH (madaktari na wakunga)	517,704,203
3	Barabara ya Kimataifa: Rumonge -	17	Kusaidia mafunzo ya wajifunzaji tarajali 20 ili kuimarisha SRH (k.m. ukunga, obgy, watayarishaji programu).	423,920,000
		18	Ukarabati wa hospitali za Kibondo na Kasulu	450,450,000
		19	Masoko ya Makere na Manyovu	95,550,000
		20	Kituo kipya cha basi (Kibondo/Manyovu)	113,750,000

Na	Jina la Mradi	Namba ya shughuli	Maelezo ya shughuli	Kiasi (Sh)
	Gitaza (45km) and Kabingo - Kasulu - Manyovu (260km)	21	Ugavi wa maji na huduma za usafi wa mazingira, ikiwamo mipira ya maji ya kuzimia moto	1,581,125,000
		22	Ujenzi wa vituo vipya vya afya (Makere/Busunzu), yakiwamo magari ya kubebea wagonjwa	659,750,000
		23	Barabara ya kuingia katika Kituo cha Afya cha Busunzu	150,150,000
		24	Shule ya Sekondari (Bweni) - Buhigwe	539,175,000
		25	Shule ya msingi (Busunzu)	120,575,000
<b>Jumla</b>				<b>9,783,474,763</b>

#### Kiambatisho VII: Shughuli zilizolipiwa bila kutekelezwa

Kipengee Na (Item No.)	Shughuli ambazo hazijatekelezwa	Kiasi kilicholipwa (USD)
<b>Mradi wa Songea</b>		
Kipengele Na 8 (Bill Nr 8) Usanifu na ujenzi wa Jengo la kuhifadhi vifaa	Kuta na saruji ya sura hufanya kazi katika situ; uimarishaji wa miundo ya mifereji ya maji	2,150.00
Kipengele Na.9 Usanifu na Ujenzi wa Jengo la Bohari ya Kemikali mita za mraba 96	Uchimbaji na kazi ya ardhini kwa mashimo ya kuloweka	14,337.05
Kipengele Na.10 Usanifu na Ujenzi wa Jengo la Maabara 96 Sqm.	Uchimbaji na kazi ya ardhini kwa mashimo ya kuloweka	14,173.25
<b>Jumla ya Mradi wa Songea</b>		<b>30,660.3</b>
<b>Mradi wa Shinyanga</b>		
Kipengele Na.6 Usanifu na ujenzi wa Jiko na jengo la chumba cha kuoshea mita za mraba 143	Uchimbaji na kazi ya ardhini kwa mashimo ya kuloweka	31,381.81
	Kuta na saruji ya sura hufanya kazi katika situ; uimarishaji wa miundo ya mifereji ya maji	24,417.55
Kipengele Na.8 Usanifu na ujenzi wa jengo la duka la vifaa 96 Sqm.	Uchimbaji na kazi ya ardhini kwa mashimo ya kuloweka	10,875.41
	Kuta na saruji ya sura hufanya kazi katika situ; uimarishaji wa miundo ya mifereji ya maji	5,375.00
Kipengele Na.9 Usanifu na ujenzi wa jengo la duka la Kemikali mita za mraba 96.	Excavation and earthwork for soak pits	11,152.96
	Kuta na saruji ya sura hufanya kazi katika situ; uimarishaji wa miundo ya mifereji ya maji	6,020.00
Kipengel Na.10 Usanifu na ujenzi wa jengo la Maabara 96 Sqm.		11,014.64
	Uchimbaji na kazi ya ardhini kwa mashimo ya kuloweka	10,279.15
<b>Mradi wa Jumla Shinyanga</b>		<b>110,516.52</b>
<b>Jumla Kubwa</b>		<b>141,176.82</b>

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa IPCs na Uthibitishaji wa Tovuti, 2023

#### Kiambatisho VIII: Vifaa vilivyopokelewa na kulipiwa lakini havijasimikwa

Vipengee vilivyoondolewa	Kiasi	Bei kwa kila kitengo USD	Bei ya Jumla (USD)	Kiasi Kilicholipwa (USD)
<b>Mradi wa Songea Kipande Cha kwanza ( Lot 1)</b>				
Sehemu ya kuingizia mazao (intake hopper)	2	27,489.59	54,979.18	54,979.18
Mkanda wa kusafirishia mazao (conveyor Belt)	21	22,922.21	481,366.41	481,366.41
Lifti ya ndoo	13	22,189.36	288,461.68	288,461.68
Kifurushi cha mwendopaka (Catwalk package)	12	22,428.14	269,137.68	269,137.68
Vipuli vya njia mbili (two ways life)	15	993.07	14,896.05	14,896.05
Mkanda wa Visafirishaji unavyoweza kugeuzwa	1	111,045.51	27,558.67	27,558.67
Upande wa chini wa vihenge	1	121,249.16	121,249.16	121,249.16
chuma cha chini cha kihenge (Flat bottom) cha kuhifadhi	2	203,408.68	406,817.36	406,817.36
Kishikilia Pipa cha kwanza	2	28,028.27	56,056.54	56,056.54

<b>Jumla ya Mradi wa Songea</b>				<b>1,720,522.73</b>
<b>Mradi wa Mbozi kipande cha tatu (Lot 3)</b>				
Sehemu ya kuingizia mazao (Intake hopper)	2	26,829.19	53,658.38	53,658.38
Fagio	2	69,146.50	138,293.00	138,293.00
Kifurushi cha mwendopaka	6	23,233.04	139,398.24	139,398.24
Vipuri vya njia mbili (two-way-valve)	14	922.55	12,915.70	12,915.70
chuma cha chini cha kihenge (Flat bottom) cha kuhifadhia	1	175,981.18	175,981.18	175,981.18
(Kishikilia Pipa cha kwanza) Pre-holding bin	2	27,037.67	54,075.34	54,075.34
<b>Jumla ya Mradi kwa Mbozi</b>				<b>574,321.84</b>
<b>Mradi wa Dodoma Kipande Cha Sabba (Lot 7)</b>				
Mkanda wa kusafirishia mazao (conveyor Belt)	17	19,481.12	331,179.04	331,179.04
Lifti ya ndoo	12	18,822.15	225,865.80	225,865.80
Kifurushi cha mwendopaka (Catwalk package)	6	23,233.04	139,398.24	139,398.24
Vipuli vya njia mbili (Two-way valves)	14	1,317.92	18,450.88	18,450.88
Vipimo pipa (Weigher hopper bin)	1	51,137.02	51,137.02	51,137.02
Mkanda wa Visafirishaji vya ukanda unavyoweza kugeuzwa (Reversible belt conveyors)	1	26,898.27	26,898.27	26,898.27
Mlango wa kudhibiti (Regulating shutters)	16	3,550.88	56,814.08	56,814.08
<b>Jumla kwa Mradi wa Dodoma</b>				<b>849,743.33</b>
<b>Mradi wa Makambako Kipande Cha Pili (Lot 2)</b>				
Sehemu ya uiningizaji mazao (Intake hopper)	2	26,339.90	52,679.80	52,679.80
Mkanda wa kusafirishia mazao (Belt conveyor)	20	17,501.52	350,030.40	350,030.40
Lifti ya ndoo (Bucket elevator)	12	18,733.12	224,797.44	224,797.44
Kifurushi cha mwendopaka (Catwalk package)	6	23,151.50	138,909.00	138,909.00
Vipuli vya njia mbili (Two-way valves)	14	1,282.97	17,961.58	17,961.58
Sehemu ya chini ya kihenge (Hopper bottom silos)	1	114,351.02	114,351.02	114,351.02
Mlango wa kudhibiti (Regulating shutters)	16	3,428.56	54,856.96	54,856.96
chuma cha chini cha kihenge (Flat bottom) cha kuhifadhia	1	178,633.73	178,633.73	178,633.73
<b>Jumla Mradi wa Makambako</b>				<b>1,132,219.93</b>
<b>Mradi wa Shinyang Kipande Cha Sita (Lot 6)</b>				
Sehemu ya kutilia mazao (Intake hopper)	2	26,829.19	53,658.38	53,658.38
Lifti ya ndoo (Bucket elevator)	12	18,822.15	225,865.80	225,865.80
Kipimio cha pipa (Weigher hopper bin)	1	51,137.02	51,137.02	51,137.02
Mkanda wa Visafirishaji vya ukanda unavyoweza kugeuzwa (Reversible belt conveyors)	1	26,898.27	26,898.27	26,898.27
Sehemu ya chini ya kihenge (Hopper bottom silos)	1	117,286.76	34,013.16	34,013.16
chuma cha chini cha kihenge (Flat bottom) cha kuhifadhia	1	184,658.96	184,658.96	184,658.96
<b>Jumla ya Mradi wa Shinyanga</b>				<b>576,231.59</b>
<b>Jumla Kuu</b>				<b>4,853,039.42</b>

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa IPCs na Uthibitishaji wa Tovuti, 2023

# **RIPOTI KUU YA MWAKA YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi  
4 Barabara ya Ukaguzi,  
S.L.P 950,  
Tambukareli, 41104 Dodoma.

 +255 (026) 2161200

 [ocag@nao.go.tz](mailto:ocag@nao.go.tz)

 [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz)

